Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 23 Aprili, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

**Kutoridhisha kwa Hadhi ya Mkoa wa Dodoma**

**MHE. MOZA A. SAIDY** aliuliza:-

Pamoja na kuwepo kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA),* bado hadhi ya Mkoa wa Dodoma zikiwemo barabara hairidhishi:-

(a) Je, kuna tatizo gani katika Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)?*

(b) Je, ni lini barabara za Mji wa Dodoma za Ipagala, Ilazo, Kisasa, Swaswa, Makulu na kadhalika zitatengenezwa ili ziwe na hadhi inayoendana na dhana ya Makao Makuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Moza utahama hiyo *microphone*, Waziri Majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma ilianzishwa kwa lengo la kupanga na kuendeleza Mji wa Ddoma ili kuwa na hadhi ya Makao Makuu nchini. Ili kutekeleza kazi hii, mwaka 1976 uliandaliwa mpango kabambe (*Master Plan*) wa Mji Mkuu uliotenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Kwa mfano barabara, mfumo wa maji taka na maji safi, maeneo ya viwanja vya makazi, Huduma za Jamii, Biashara, Taasisi, Viwanda, maeneo ya wazi na kadhalika. Mwaka 2011 Mamlaka ilianza kufanya mapitio ya Mpango Kabambe ili uweze kwenda na wakati. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu haijafanikiwa kutekeleza mpango wake kama ilivyotarajiwa kutokana na tatizo kubwa la upatikanaji wa fedha za kutosha.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara za Ipagala, Ilazo na Swaswa kwa kiwango cha changarawe umeanza katika mwaka wa fedha 2010/2011 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Barabara za eneo la Kisasa zenye urefu wa kilomita 11.856 kama alivyoziulizia Mbunge, zinajengwa hivi sasa kwa kiwango cha lami na barabara za eneo la Makulu zinatarajiwa kuanza kuboreshwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi kabambe kuboresha barabara za Mjini Dodoma. Miradi hii itatekelezwa kwa awamu mbili kwa kisimamiwa na *CDA* pamoja na Manispaa ya Dodoma. Miradi hii kwa jumla itagharimu jumla ya *USD 37.7.* Mpaka sasa zaidi ya shilingi bilioni 6.3 zimekwisha kutumika tangu awamu ya kwanza ya utekelezaji wa miradi hii ilipoanza mwezi Agosti mwaka 2011, ambapo barabara za Kisasa na Chang'ombe zenye urefu wa Km.15.65 zinaendelea kujengwa ambapo asilimia 30 ya ujenzi umekamilika.

Pia ujenzi wa barabara za Mtendeni *Market*, Tembo, Tabora, Nkuhungu, Chamwino, Chang'ombe zenye urefu wa Km.11.17 zimekamilika kwa asilimia 23.87.

Katika kuboresha Miundombinu ya Maji Serikali hivi sasa inaendelea na mradi wa usambazaji mabomba ya Maji yenye urefu wa km.29 unaendelea katika eneo la Kisasa. Mradi huu unagharimu kiasi cha shilingi 846 milioni na unatarajiwa kukamilika kati ya mwezi Juni na Agosti, 2012. Aidha, ujenzi wa bomba la majitaka la urefu wa Km.6 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2 unaendelea.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri yasiyokuwa na matumaini, Kwa kuwa Serikali inatenga pesa ndogo ya kuweza kuendesha sekta hii ya *CDA.*

(a) Je, Serikali sasa hivi inaonaje kukitoa chombo hiki kwa kuwa kimeanza kwa muda mrefu bila mafanikio yeyote na kuwanyanyasa wananchi katika mji huu wa Dodoma na Watanzania kukitoa na kubaki kuwa Manispaa?

(b)Kwa kuwa, utekelezaji umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu, Je Serikali kweli ina dhamira ya kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma kwa utekelezaji wake ambao unadai miradi na miundombinu ambayo inatekelezwa mpaka sasa hivi hakuna viwanda hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea katika Mji huu wa Dodoma.

Je, Serikali inatuambia nini wananchi na Watanzania kwa ujumla kukitoa chombo kinachoitwa *CDA* ambacho kinawatenga wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU-SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Nataka kukiri kwamba tangu *CDA* imeanzishwa mambo mengi sana yamefanyika hapa Mjini na sisi Wabunge wengi ni mashahidi. Katika Mji angalau umepangika vizuri ukilinganisha na Miji mingi ya Tanzania ni Dodoma na hii kazi imefanywa vizuri tangu *CDA* ilipoanzishwa kutokana na utekelezaji wa *Master Plan*.

Kwa hiyo kusema kwamba hakuna kilichofanyika kabisa na hakuna matumaini hapo sasa kidogo tumetia chumvi. Yapo mambo makubwa yamefanyika hapa.

Mheshimiwa Spika, leo nakupa takwimu na ukifika pale Mjini utakuta kazi inaendelea. Kwa miaka miwili tu kuna kazi inafanyika ya dola milioni 37.7 niambie Wilaya gani nyingine Mjini hapa Tanzania hivi sasa ambayo inatekeleza miradi ya barabara tu ya dola milioni 37.7. Sasa jiulize kwanini Dodoma, ni kwa sababu ya madhumuni ya Dodoma ya kuwa Makao Makuu.

Kwa hiyo, kazi ya uimarishaji miundombinu na haiwezi kukamilika kwa mara moja. Chombo hiki hakiwezi kutoka mpaka kikamilishe kazi yake. Tuna *Master Plan* mpaka itakapokamilika ndiyo *CDA* itatoka, lakini kwa sasa haitatoka. Sasa hivi tunaimarisha marekebisho fulani tunayafanya ili kukipa nguvu zaidi na kujenga mahusiano ya karibu zaidi ya *CDA.*

Mheshimiwa Spika, kwa maswali yote aliyouliza Mbunge nataka kumhakikishia kwamba Serikali itaendelea kutenga pesa kwa kushirikiana na wadau wengine ili kutimiza lengo la *CDA* ambalo wananchi wa Tanzania waliamua. *(Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, mimi napenda kumwuliza Waziri, barabara za majengo katika Mji wa Dodoma ni mbaya sana, lakini pia kuna mtaro ambao unapita katikati ya soko mpaka kwenda Hospitali ya Mkoa ambayo ni mchafu umejaa taka na vinyesi, na unahatarisha maisha ya watu.

Je, ni nani anastahili kusafisha mtaro huu kati ya *CDA* na Mamlaka ya Manispaa ya Mji wa Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kazi ya *CDA* huwa ni kujenga miundombinu, ikishakamilika inakabidhi Manispaa, lakini nakuhakikishia nitakwenda kuagiza mamlaka inayohusika maana hapa siyo kutaja nani anayehusika, nafikiri Mbunge anataka kazi hiyo ya kusafisha huo mtaro wa kuondoa hicho kinyesi ifanyike. Kwa hiyo, nitahakikisha kwamba leo hii nitakwenda mamlaka zinazohusika kupitia Mheshimiwa Mwanri yupo hapa amesikia ili kazi hiyo ianze kufanyika leo. *(Makofi)*

Na. 121

**Upandishaji Hadhi Barabara Inayounganisha Wilaya**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara inayounganisha Wilaya za Igunga, Uyui na Singida Vijijini kupitia Vijiji vya Mwanzugi, Itumba, Mhamamoja, Seregei, Susujanda, Mswaki(Mpyagula), Loya hadi Iyumba ili iweze kuhudumiwa na *TANROADS* na kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika utaratibu wa kupandisha hadhi barabara za Wilaya kuwa za Mkoa na kuhudumiwa na *TANROADS* ni mapendekezo hayo kujadiliwa katika vikao vya Halmashauri, Kamati za Ushauri za Wilaya *DCC* na Bodi ya barabara ya Mkoa, maazimio ya Bodi ya Barabara ya Mkoa huwasilishwa katika Wizara ya Ujenzi ambayo inadhamana ya kupandisha hadhi barabara kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba vikao vya kisheria vinavyotakiwa kupitisha mapendekezo haya havijafanyika. Hivyo mapendekezo hayo yatakapopitishwa rasmi kwenye vikao hivyo yatawasilishwa katika Wizara ya Ujenzi yenye dhamana kwa mujibu wa sheria. Hivyo tunamshauri Mbunge aishauri Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ipitishe wazo hili katika vikao vilivyotajwa hapo juu ili uamuzi uweze kufanyika.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana, na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yenye maelekezo mazuri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba barabara hii inayounganisha Wilaya za Singida Vijijini, Uyui na Igunga ni barabara ambayo inatumika kubeba mazao ya mifugo na mazao ya kilimo kwenda kwenye soko Igunga na kwingineko hadi Dar es Salaam?

(b)Serikali itakuwa tayari basi kutekeleza mradi huo wa kupandisha barabara hiyo kuwa ya Mkoa endapo vikao vya *DCC* pamoja na Bodi ya Barabara itakapopeleka maombi huko Wizarani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, mimi nafahamu hivyo kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi. nafahamu kwamba mazao ya mifugo pamoja na mazao ya kilimo. nafahamu kwamaba binadamu wanapita kule, najua kabisa jambo hili wala sina tatizo kabisa na Mheshimiwa Kafumu kuhusu hili analosema.

Mimi ninachoweza kumWahidi hapa kwenye swali la pili la kusema kwamba tutapandisha daraja barabara ile utaratibu ni huo niliousema hapo. Waende katika *Road Board* ya Mkoa wakubaliane na baadaye sisi na yeye tutashirikiana ili kumshawishi Waziri wa Ujenzi ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kupitisha barabara hii na kuipandisha hadhi ili iweze kuwa katika hali hiyo anayoisema.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali lingine sikumwona mtu aliyesimama kabla, yaani linaloulizwa swali la pili ndiyo msimame akiwa amejibu halafu mnasimama hiyo hapana.

Na. 122

**Mashamba ya Kilimo Mgongola-Mvomero**

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (K.n.y. MHE. ABDULAZIZ ABOOD)** aliuliza:-

Mashamba ya Kilimo cha Mpunga yaliyoko Mgongolo Wilayani Mvomero, yalimilikiwa na wakulima tangu mwaka 1970. Lakini wakulima wamepokonywa mashamba hayo yamegawiwa kwa wafugaji. Viongozi walipopita waliamuru mashamba hayo yerejeshwe kwa wakulima na wafugaji waondolewe. Mpaka sasa hawakuondoka na badala yake wafugaji hao wamemilikishwa mashamba hayo:-

(a) Je, ni lini agizo la kuwarudishia wakulima mashamba hayo na kuwamilikisha litatekelezwa?

(b) Je, Serikali itawahakikishia usalama wakulima hao ili waendelee na shughuli zao bila bughudha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulaziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdulaziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mashamba ya kilimo cha mpunga Mgongola yenye ukubwa wa hekta 591.9 yanamilikiwa na wananchi wa vijiji vya Kambala, Kigugu, Mkindo na Dihombo Kata ya Hembeti, tarafa ya Mvomero, Wilayani Mvomero kuanzia miaka ya 1970 hadi sasa. Hakuna kumbukumbu zozote zinazoonesha kuwa wakulima hao walipokonywa mashamba yao na kugawiwa wafugaji.

Kumbukumbu zilizopo ni kuwa kijiji kimojawapo cha eneo la Mgongola kiitwacho Kambala kilisajiliwa kuwa Kijiji cha wafugaji mwaka 1993 na kupewa usajili *MG. KIJ.473,* lakini pamoja na kuanzishwa Kijiji hicho, wakulima wameendelea kutumia maeneo hayo kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilichosababisha mgogoro ni wakulima wanaotoka nje ya Kambala (Morogoro Mjini na sehemu zingine) waliokataa amri ya uongozi iliyowataka waache kulima eneo hilo. Hii ilipelekea wafugaji kufungua kesi Na. 25/2007 katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi. Uamuzi wa Mahakama bado haujatolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Adulaziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, enye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna wakulima waliopokonywa mashamba yao bali wanaendelea kuyatumia isipokuwa mashamba yaliyopo katika Kijiji cha Kambala yenye pingamizi la Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi na kesi hiyo bado haijatolewa uamuzi na Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo ambalo si la mgogoro katika bonde hili la Mgongola, wakulima wanaendelea kulima na Serikali siku zote inahakikisha usalama wa makundi ya wakulima na wafugaji kwa uongozi wa Wilaya ya Mvomero kuwakutanisha na kuwataka waishi kwa amani wakisubiri uamuzi wa Mahakama katika Kitengo cha Ardhi.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kuwa Naibu Waziri ametuhakikishia kwamba ni kweli wale wakulima wapo ukiachia nje ya wale ambao wapo katika mgogoro na ambao suala lao liko mahakamani. Wale waliopo sasa hivi, ni kwa nini Serikali isiamue kuliko kusubiri mpaka yatokee malumbano na matatizo.

Kwa nini Serikali isiamue kuwamilikisha kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge juu ya wananchi hao wenyeji wa maeneo hayo aliyoyataja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa kifupi sana hapa kwa sababu tusije tukachukua muda mwingi. Jambo hili lilitokea nyuma sana wakati wa mambo ya nguvu kazi ndiyo jambo hili lilitokea na ukiangalia mambo kihistoria unakuwa *scientific* katika maelezo yako na katika majibu yako.

Mgogoro huu umekwenda mpaka ukafika hapo ulipofika hivi sasa tunavyozungumza eneo linalolalamikiwa eneo hili, hili suala limekwenda Mahakamani na kama suala hili liko Mahakamani mimi hapa kwa kuheshimu sheria na taratibu za nchi nijibu swali sasa kwamba kwa nini hawakuamua kuwamilikisha wale, kwa sababu ni jambo kubwa ambalo mimi ninavyofahamu sasa hivi mimi nikianza kulieleza hapa utaniambia inatosha.

Niseme tu Mheshimiwa Spika kama anataka aje tutamweleza vizuri na sisi tuko tayari kushirikiana na uongozi pale Mvomero ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri Mkuu kuwaomba wananchi pale walipo watulie tusubiri maamuzi ya Mahakama, Mahakama ikishatuambia ni hawa sisi tutaenda kuwaambia kwamba Mahakama imesema ni hawa.

**SPIKA:** Ahsante sana, kama suala lenyewe lipo Mahakamani basi tusiendelee kulivuta vuta hapa, tunaenda Wizara ya Fedha Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, kwa niaba yake Mheshimiwa Christowaja.

Na. 123

**Kuhusu Fedha za Mikopo za *TIB***

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. LETICIA MAGENI NYERERE)** aliuliza:-

Serikali ilitoa kiasi cha shilingi trilioni 70 kwa *TIB* kwa ajili ya kutoa mikopo ya shughuli za kilimo:-

Je, Serikali ilichukua tahadhari gani kwenye Mkataba wake wa *TIB* za kuhakikisha udhibiti wa fedha hizo endapo makampuni yatashindwa kurudisha mkopo huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kiasi ambacho kimetolewa Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) kwa ajili ya ajili ya Dirisha la Kilimo ni shilingi bilioni

42.0 tu na siyo shilingi bilioni 70. Kupitia Ddirisha la Kilimo, *TIB* itatoa mikopo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwa masharti nafuu na kwa kuzingatia aina ya kilimo kinachoombewa mkopo. Hii ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha fedha zinazokopeshwa zinarejeshwa *TIB* kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu iliandaa mwongozo wa ukopeshaji *(Lending Framework).* Mwongozo huo unatoa dira ya makubaliano ya taratibu na shereia zikatazotumika katika utoaji na usimamizi wa mkopo huo.

Ili kuongeza marejesho, *TIB* itakopesha fedha kupitia vikundi vya wakulima kama vile *SACCOS*, VIKOBA, Vyama vya Ushirika, *Community Banks* na Vyama vya Wakulima wa nje *(Out Growers Associations).*

Mheshimiwa Spika, *TIB* itatumia pia mawakala kama vile wasambazaji wa matrekta na zana zingine za kilimo ili kuweza kuwafikishia wakulima wadogo wadogo vijijini na kuwapatia mikopo kirahisi. Mawakala wote watawajibika kutoa mafunzo kwa wakulima ili kuwajengea uwezo wa jinsi ya kutumia zana za kilimo pamoja na matengenezo yale. Pale itakapowezekana wakala atatakiwa kuwadhamini wakopaji ili waweze kupata mikopo kirahisi.

Mheshimiwa Spika, mkopaji atatakiwa kuandaa mchanganuo wa mradi *(Project Proposal)* kwa ajili ya uchambuzi kabla ya kupatiwa mkopo. Michanganuo ya miradi itachambuliwa kwa kuzingatia taratibu zote za mikopo zinazokubalika kibenki.

Aidha, *TIB* itatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha taarifa za kila robo ya mwaka za maendeleo ya Dirisha hilo kwa ajili ya uchambuzi na kubaini mafanikio, hatari, changamoto na uhimilivu wake. Ahsante sana.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Benki ya *TIB* ilipewa jukumu la kutoa mikopo kwa wakulima ili kutekeleza Sera ya Kilimo Kwanza. Bila kutafuna maneno wala maneno ya mchakato Waziri anatoa tamko gani mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba ni lini Serikali sasa itaanzisha Benki ya Wakulima ili iweze kutoa mikopo kwa wakulima wote bila ubaguzi?

(b) Kwa kuwa Makao Makuu ya Benki ya *TIB* yako Dar es Salaam Waziri anatuambia nini juu ya ufanisi wa Benki hii hasa kuwafikia wakulima wengi ambao wako vijijini katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya uanzishwaji wa Benki ya Wakulima au Benki ya Kilimo yanakamilika. Sasa hivi ina-*operate* kama dirisha kwenye Benki ya *TIB* lakini hivi ninavyoongeza tayari *application* ya leseni imeshakwenda *BREILA* na wakati wowote Benki hii itaanzishwa ikiwa pia tayari tumepata jengo kwa ajili ya kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwafikia wakulima, kwa kweli hivi sasa benki hii ina matawi manne, Dar es Salaam mawili, kuna Mwanza na Arusha. Hata hivyo tuko mbioni kuanzisha tawi la Mbeya nafikiri Mwezi ujao na tutaendelea kuanzisha matawi haya kama nafasi ya kifedha itakavyoruhusu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anatakiwa kukiri ukweli ambao uko mpaka sasa wa kwamba benki hii kwa kiasi kidogo sana imewafikia wakulima kupitia hivyo Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo anavyovisema na ushahidi huo ninao kwa sababu vyama vyangu vya Akiba na Ushirika na Mikopo vya Peramiho, Vya Magagula, vya Mbinga Muhalule vya Badaba vimehangaika sana kupata mikopo kupitia benki hiyo mpaka sasa mikopo hiyo haijapatikana.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari kufanya mapitio ya masharti ya Benki hiyo ili wakulima wetu kupitia vyama vya akiba vya Ushirika na Mikopo viweze kufaidika na hasa vyama vile vinavyowasimamia wakulima wa mazao ya vyakula? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Niko tayari kufanya mapitio kwa sababu wakulima ndio walengwa. Kama wakulima wanahisi bado kuna tatizo tuko tayari tuendelee kufanya

nao kazi kama wadau ili kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo. Benki hii haitatimiza malengo yake kama wakulima hawatafikiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ili kuongeza tija katika kilimo na uwekezaji nchini ilikubalika kwamba benki ya *TIB* itapata bilioni 5 kwa kipindi cha miaka 5 yaani 2010/2015. Na kwa kuwa mwaka huu wa fedha ambao tunaumaliza hakuna fedha yoyote ambayo imepelekwa katika benki hiyo.

Je, sasa Waziri ataliambia Bunge hili kuwa katika Bajeti hii tunayoianza shilingi bilioni 125 zitapelekwa katika benki hii ili kuongeza kasi ya uwekezaji nchini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Yaani tano mara tano.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Mpina, kama ifuatavyo:-

Najibu ndio. Tumeshaanza kutenga bilioni 100 kama ilivyo kwenye mpango wa miaka mitano wa maendeleo na zitatolewa.

**SPIKA:** Ukisema ndio maana yake ndio. Haya!

Na. 124

**Mpango wa MMAM wa Unenzi wa Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya Kwa kila Kata**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Mpango wa Serikali na MMAM ni kujenga Zahanati kwa kila Kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata, Wilaya ya Ngara ina Kata 20 na vijiji 72 lakini ina Vituo vya Afya vinne tu na Zahanati 43 tu:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya 16 na Zahanati 29 ili kutekeleza mpango wa MMAM hasa izingatia kuwa sekta ya afya haikuwekwa kwenye vipaumbele vya mpango wa kwanza wa maendeleo na Bajeti ya fedha ya mwaka 2011/2012? *(Makofi)*

**WAZIRI WA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazima, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ulianza mwaka 2007 na umepangwa kukamilika mwaka 2017 kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali. Ili kuwezesha utekelezaji wa mpango huu, Serikali imeweka mfumo wa kugharimia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya ambapo Wilaya husika hutakiwa kuingiza katika mahitaji mpango kabambe wa afya wa Halmashauri.

Halmashauri ndizo zenye uamuzi wa kuchagua vipaumbele na vituo gani vya kutolea huduma za afya vijengwe katika mwaka husika kwa kutumia fungu la *Local Government Capital Development Grant (LGDG).* Fungu hili hutolewa kwa kila Halmashauri ikiwamo ile ya Ngara, kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa vya uwingi wa watu, umbali wa vituo vya huduma za afya, kiwango cha umaskini na kiwango cha vifo vya watoto. Mpango wa MMAM unatekelezwa kwa kushirikiana kati ya jamii husika na Serikali yao kupitia Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza nguvu katika mapendekezo ya kujenga zahanati 29 na vituo vya afya 16 vilivyobaki kama ilivyoainishwa, Wizara inashauri kwamba Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara awasilishe mapendekezo hayo katika Halmashauri ambayo itawasilisha kwenye Baraza la Madiwani ambalo ndilo mamlaka ya Halmashauri katika kupitisha mapato na matumzi ya Halmashauri.

Mwisho napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuona umuhimu wa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kama ilivyoainishwa katika mpango wa MMAM na natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote waendelee kuhamasisha wananchi kujenga Zahanati na Vituo vya Afya ili kufanikisha malengo yaliyo katika Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi MMAM kama ilivyotarajiwa.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya Nyongeza.

(a) Mheshimiwa Waziri ananishauri niwasilishe mapendekezo yangu kuhusu ujenzi vituo vya afya na zahanati kwenye Baraza la Madiwani huko Ngara ambapo mimi mwenyewe ni Mjumbe. Je, Baraza litasaidia nini iwapo linapata fedha kidogo kutoka *CDG* na halipati fedha zozote kutoka mpango wa MMAM? (*Makofi*)

(b)Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania ina rasilimali za kutosha mahitaji yetu muhimu yote yaani *basic needs* hata kama tungekuwa watu milioni 100 lakini nchi hii ina rasilimali za kutosha ni ulafi wetu. Kama

rasilimali zilizopo zingegawanywa vizuri kwa Wilaya zote na Mikoa yote maendeleo yangekuwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, uliza swali.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, hiyo ilikuwa *introduction*. Swali Ngara ina Hospitali tatu kubwa, Hospitali ya Lulenga ambayo ni ya *Mission* ya Wakatoliki, Hospitali ya Murugwanza ambayo ni *Mission ya Anglican* ambayo ni *District Designated Hospital.* Lakini swali langu linakuja kwenye Hospitali ya Nyamiaga, Hospitali ya Nyamiaga ilikuwa ni kituo cha afya mpaka mwaka 2008 ambapo Mheshimiwa Rais alikwenda kukipandisha hadhi kituo hicho kikawa Hospitali kamili.

Sasa swali Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haijaitambua Hospitali hii ya Nyamiaga kuwa Hospitali kamili kutokana fedha kidogo inazozipeleka *MSD* kwa ajili ya mgao wa fedha. Sasa swali ni lini Wizara ya Afya itatoa fedha za kutosha na kuitambua hospitali hii kama ni hospitali kamili, ili hospitali ipate mgao mzuri kwa ajili ya madawa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Dokta nadhani umeshaelewa vizuri swali ujibu kwa kifupi hizo hotuba zake zingine ziache.

**WAZIRI WA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Ntukamazina, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama ulivyonielekeza kwamba nijibu kwa kifupi sana lakini pale itapobidi hajaridhia na majibu hapa nitamwomba Mheshimiwa Mbunge tukutane kwa sababu naona yuko *serious* sana na wananchi wake anaowawakilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, jibu mtaonana baadaye.

**WAZIRI WA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, jibu la kwanza kwamba tusaidieje? Kama nilivyosema Baraza lao likipitisha mpango ule wa afya katika Halmashauri husika na mpango ule unawasilishwe TAMISEMI na tunatengeneza Bajeti.

Kwa taarifa katika huu mfuko ambao nimeueleze katika jibu la msingi Wilaya ya Ngara wamepata tayari kwa mwaka wa fedha huu wamepata milioni 700. Katika hizo milioni 700 milioni 141 zimetengwa

katika sekta ya afya ambayo ikilengwa vile vile kutoa na kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Ngara.

Swali la pili, amezunguka lakini ni kwamba hiyo hospitali ya Nyamiaga kwamba inapata mgao mdogo kulingana na mahitaji halisi ili wahusika katika Wilaya Sekta ya Afya wamewasiliana na niliwaelekeza namna gani ya kuweza kulitatua hili tatizo. Habari njema ni kwamba tayari wameshawasilisha maombi yao na naomba nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba leo wako Wizarani wanaongea na viongozi husika pale, wameleta maelekezo zaidi, mahitaji yao kwamba yameongezeka kutegemea idadi ya watu na hiyo sisi tutaiangalia na tutawapa kama inavyostahili. *(Makofi)*

Na. 125

**Hitaji la Barabara Bora – Rungwe Magharibi**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaifanyia matengenezo ya uhakika barabara inayotoka Kyimo – Ikuti – Luswiswi hadi Itumba na inayoziunganisha Wilaya za Rungwe na Ileje ili kuwahakikishia usafiri wa uhakika?

(b) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utaanza?

(c) Je, ni lini Serikali itaunganisha vijiji vya Ipande na Masukulu kwa barabara hiyo ili kuchochea maendeleo katika eneo hilo na kuwapunguzia adha ya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. David Homel Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyimo – Ikuti – Luswiswi – Ibungu (km 68.5) ni barabara ya Mkoa ambayo inafanyiwa ukarabati na matengenezo mbalimbali kila mwaka kuanzia mwaka 2007/2008 kwa jumla ya shilingi milioni 2,299.6 barabara hiyo iko katika hali nzuri na inapitika.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Aidha, Wizara kupitia wakala wa barabara Mkoa wa Mbeya itaendelea kuifanyika matengenezo barabara hiyo kila mwaka ili kuhakikisha inapitika kwa urahisi wakati wote.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha vijiji vya Ipande na Masukulu ni ya Wilaya inayohudumiwa na Halmashauri za Wilaya za Rungwe na Kyela. Tunashauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika za Wilaya ili barabara hiyo iingizwe katika mipango ya maendeleo na kutengewa fedha.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu na nitazingatia ushauri kwamba niwasiliane na Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Kyela kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri yeye ndio Mbunge wa Kyela nadhani tungefanya kazi kwa pamoja tukafanikisha azma hii.

(a) Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo. Kwanza ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wamezunguka na kukagua barabara nyingi hapa nchini nilitaka kuuliza kama watakuwa tayari kuzikagua hizo barabara nilizoziomba ili wapate hali halisi na penginepo watakuwa na huruma wanapopanga vipaumbele vyao kule Wizarani?

(b) Mheshimiwa Spika, maswali mengi yanayoulizwa kuhusu barabara lakini hata huduma zenyewe za jamii hapa Bungeni wauliza maswali wanarejea ahadi za Rais. Nilitaka kuuliza kwa majimbo kama langu ambako hatuna ahadi kama hiyo, tukimbilie wapi kama tunataka kupata Mipango ya Maendeleo yetu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, kama ifuavyotavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwa kufuatilia kwa karibu masuala ya miundombinu katika Wilaya ya Rungwe, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Mwakyusa kuwa Wizara inatambua tatizo la uharibifu wa barabara za changarawe na udongo mara kwa mara hasa katika mazingira ya mvua nyingi za Wilaya kama Rungwe, Ileje na Kyela.

Kwa kweli ndio maana kila mwaka tunatenga mafungu ya fedha ya ukarabati wa hizo barabara na pale ambapo fursa inatokea mzigo

unapungua wa Serikali katika kujenga barabara za lami tunapoteua barabara mpya za kujenga kwa kweli tunatoa kipaumbele kwa maeneo kama hayo.

Pili, ningependa kumwomba Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwamba pale ambapo kuna mahitaji ya barabara yoyote mpya tungeomba tu wajenge hoja na Wizara yao itawasikiliza. *(Makofi)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa naomba kumwuliza Waziri wa Ujenzi, kuna ahadi ambayo ilitolewa na yeye mwenyewe hapa Bungeni kwamba Daraja la Mto Magala ambalo linaunganisha Wilaya ya Mbulu na Babati na Hifadhi ya Manyara ingeanza kujenga na fedha ilikuwa imeshatengwa.

Je, kwa nini mpaka leo hii hiyo kazi haijaanza wakati ahadi zile zingine za Serikali za kufungua Geti la Hifadhi upande wa Manyara imekamilika na sasa hivi hiyo barabara hatuwezi kuitumia hasa kipindi hiki cha mvua?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Soni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado azma ya kujenga daraja la Mto Magala ipo pale pale tunaomba wananchi watuelewe tu kumetokea hitilafu za kiufundi chache lakini bado tuko katika mchakato wa kujenga hilo daraja kama ambavyo tulivyodhamiria maana fedha tumeshatenga.

Na.126

**Ujenzi wa Barabara ya Kilwa**

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR** aliuliza:-

(a) Je, ujenzi wa barabara ya kilwa *(Kilwa Road)* kutoka Kurasini hadi Mbagala Rangi tatu kwa msaada wa Japan umeshakamilika?

(b) Je, Serikali imeshakabidhiwa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kilwa *(Kilwa Road)* kutoka Kurasini hadi Mbagala Rangi tatu kwa msaada wa Serikali ya Japan ulikamilika tarehe 30 Septemba, 2009 na kipindi cha utangulizi wa Mkandarasi kiliisha tarehe 30 Septemba, 2010.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikataa kupokea barabara hiyo kutokana na kujengwa chini ya kiwango na kumtaka Mkandarasi aliyejenga arudie kazi hiyo ili kurekebisha kasosro zote kwa gharama yake ndipo ipokelewe. Mkandarasi *KAJIMA Corporation* amekubali kuijenga upya kwa gharama zake mwenyewe barabara yote yenye urefu wa kilometa 5.1.

Aidha, Mhandisi Mshauri INGEROSEC amekubali kusimamia kazi za kuijenga upya barabara hiyo kwa gharama zake mwenyewe. Waziri wa Ujenzi na Balozi wa Japan nchini walisaini na kutoa taarifa ya pamoja tarehe 4 Januari, 2012 kuhusu makubaliano yaliyofikiwa ya kuijenga upya barabara ya Kilwa. Kazi ya kujenga upya barabara ya Kilwa itaanza mwezi Mei, 2012 na kukamilika kabla ya mwishoni mwa mwaka 20102. *(Makofi)*

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Katika jibu la msingi umesema barabara hiyo itatengenezwa upya kuanzia mwezi wa Mei, 2012. Mbona hivi sasa barabara hiyo inatoa viraka?

(b) Barabara hiyo tangu inaaza kutengenezwa ilionekana hafifu sana. Kwa nini Wizara yako kupitia ma-*engineer* wao wasiweze kuistopisha hiyo barabara isiendelee kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pengine niseme kwa kifupi sana katika utangulizi kwamba hii barabara tunayozungumzia, tumeijenga katika awamu tatu. Kipande cha kwanza ni kutoka Bendera Tatu mpaka Mtoni kwa Azizi Ali yenye urefu wa kilomita 5 na kipande cha pili ni kutoka Mtoni kwa Azizi Ali mpaka Mbagala rangu tatu. Lakini hatukuweza kufika Mbagala rangi tatu kutokana na mapungufu ya pesa ya ufadhili tuliopewa kwa hiyo kilomita moja na nusu nyuma tukaweza kufikia hapo. Ni kipande hiki cha pili

ambacho kilionyesha udhaifu kutoka kwenye *base*, tunaita *base course* kutoka kwenye msingi wa barabara ndiyo ambayo tunaijenga upya.

Mheshimiwa Spika, anapoona tunatia viraka, huu ni wajibu wetu sisi kwa barabara yeyote hata ambayo imepangiwa kujengwa lazima iwekewe viraka ili usafiri uendelee. Hatuwezi tu kuacha tukasema kwa sababu itajengwa basi hatuwezi kufanya *maintenance*. Kwa hiyo, tunafanya *maintenance* kwa sababu lazima iendelee kupitika mpaka pale ambapo tutakapokamilisha ujenzi wa kudumu.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Barabara ya Kitosua Mpembe na barabara ya Nkana Kala ni barabara zilizokwishaombewa kupandishwa hadhi kuwa za Mkoa na Wizara imeshatuma Kamati yake kwenda kuona na imekubali kwamba kwa kweli zinastahili na barabara hizi ni sumbufu sana na mwaka huu nikiwa kwenye ziara ya Kala, niliweza kushindwa kurudi kwa kulala mara mbili njiani na watu kunizomea kwamba Kiongozi wewe unalala njiani na una sababu ya kututetea na hujafanya hivyo.

Sasa na hadhi ya Serikali kupitia barabara hii imeshuka sana kwa Waziri Mkuu ana taarifa na mimi nimeuliza mara mbili, mara tatu kwenye Bunge hili Tukufu. Naomba mipango ya Wizara kuzipandisha hadhi barabara hizi kama tulivyoomba? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Mbunge kwa kulala njiani na mpaka anaanza kuzomewa. Mimi nimwombe tu kwa kifupi kama hali ni mbaya kiasi hicho kwa nini asinione baada ya muda wa maswali niweze kuangalia jinsi gani tutaweza kufanya katika maandalizi ya Bajeti ya sasa.

**MHE. MCH.PETER.S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na shughuli ya ujenzi wa barabara inayoendelea nchini, lakini barabara nyingi za Tanzania hazina hadhi kama barabara za Kusini mwa Afrika kwa sababu alama za barabarani haziko sawa sawa. Kwa mfano hatuna *speed limit.* Waziri anasemaje kuhusu kuweka *speed limit* ambazo ziko tu kwenye maeneo ya vijiji na haieleweki. Kwa mfano unapoendesha gari kwa speed 100 unakuta tu alama speed 50 hazina mpangilio mzuri kama Kusini mwa Afrika. Unaweza kusemaje Waziri?

**SPIKA:** Hilo swali lingine. Yaani mkitaja barabara basi anaweza kuuliza jambo lolote kuhusu barabara sivyo hivyo. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushauri wake nakiri kupokea na naona mapungufu tuliyo nayo katika barabara zetu tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

Na 127

**Ahadi ya Chuo cha Veta- Mbozi**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Mwaka 2008 Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Ufundi *VETA* Wilayani Mbozi.

Je, ni lini chuo hicho kitajengwa kutoa mafunzo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kujenga Chuo cha Ufundi Stadi kila Wilaya. Hata hivyo, kutokana na gharama za ujenzi kuwa kubwa, vyuo hivyo vitajengwa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbozi ipo katika orodha ya Wilaya 28 zitakazijengewa Vyuo vya Wilaya katika awamu ya kwanza, nachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Wilaya hiyo waendelee kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo ambapo Wilaya ya Mbozi inahusika.

Aidha, wananchi na vijana wa Wilaya ya Mbozi wanashauriwa kupata huduma hiyo ya vyuo katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mbeya.

**MHE. GODFEY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, haya ndio majibu ya Serikali ambayo kimsingi hayana tija.

(a) Serikali imetoa ahadi hii tangu mwaka 2008 tumepita Bajeti karibu nne za Serikali bado tuna dhamira, bado tuendelee kuvuta subira. Swali liko wazi ni lini Chuo cha Ufundi *VETA* kitaanza kujengwa Mbozi? Ni lini ndio swali. (*Makofi*)

(b)Kwa kuwa ahadi hii pia inavihusu vyuo 28 vya *VETA* nchini kote, Waziri pia atueleze hivi vyuo vingine vyote vilivyoahidiwa na Serikali nchini kote 28 mwaka 2008 na Mheshimiwa Margaret Sitta alipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, vitajengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ni kweli kabisa toka mwaka 2008 Serikali iliahidi kujenga vyuo hivi vya Wilaya kila Halmashauri. Lakini hata katika Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi (CCM) lipo ndani ya ilani yetu. Lakini nimwahidi tu Mheshimiwa Zambi kwamba hatujakaa kimya haya ni mambo ya Bajeti *constraints* kwamba tumeshaandika maandiko ya kuomba fedha mbalimbali kwa riba nafuu na labda hapa siwezi kusema lakini tuko na mazungumzo na Wachina, tumeshafikia muafaka fulani wa kupata mkopo wenye riba nafuu ili kuweza kujenga hivi vyuo vya *VETA* kwa hiyo, tuwe na subira.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Naomba na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya Mpya ya Kalambo ambayo haina chuo hata kimoja cha *VETA* na ili kijana aende kusoma inabidi aende kilomita 350 kwenda Mpanda. Je, Serikali inatuahidi nini kuhusu kutujengea chuo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli toka tumetoa ahadi hii ya kujenga vyuo vya Wilaya na ilikuwa ni mwaka 2008 lakini ni mwaka jana tu ambapo Serikali imetangaza Wilaya hizi mpya na bado hatujazifanyia ile *feasibility studies* kuweza kuangalia zile *study* zitakazotumika tunapojenga hivi

vyuo. Kwa hiyo, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa vile ameahidi na amesema kwamba Wilaya ya Kalambo haina chuo naomba basi awepo kwenye *list* ya zile Wilaya ambazo tutazifanyia *study* kuweza kujua ili iingie kwenye mfumo na wao wa kupata Chuo cha *VETA.*

Mheshimiwa Spika, lakini hii ni pamoja na ile Mikoa mipya ambayo imetangazwa mwaka huu Serikali imekuwa na dhamira ya kujenga vyuo lakini kwenye Mikoa tumemaliza na ilikuwa sasa tuanze kuingia kwenye Wilaya kama ambavyo nimesema. Lakini dhamira ya kwanza tutaanza kwenye hii Mikoa mipya iliyotangazwa hivi karibuni ambayo ni Geita, Simiyu, Katavi na Mkoa mwingine nadhani nimeusahau jina.

**SPIKA:** Mkoa wa Njombe wewe, unasahau Mkoa wa Spika? (*Kicheko*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uamuzi wa kujenga vyuo vya *VETA* kwenye Wilaya ni wa Kitaifa na kwa kuwa Wilaya nyingi hazina Vyuo. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa ratiba ya kitaifa kwa awamu hii ya kufikia mwaka 2015 kila mwaka ni vyuo vingapi vitajengwa ili tuachane na kazi ya kuuliza kila mtu hapa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba niwashukuru Wabunge inaonekana suala la Vyuo vya *VETA* ni *serious* na sisi Wizara ya Elimu kama nilivyosema kwamba tuko *serious* na tumeshaanza mazungumzo na Wachina ili waweze kutupatia fedha za riba nafuu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wawe na subira hiyo. Lakini kama alivyosema kwamba ni kweli ni mpango wa kitaifa na ni wazi kabisa kwamba kila Wilaya au kila Mheshimiwa Mbunge angeweza kujua yeye yuko katika awamu gani. Mheshimiwa Spika, unipe tu dakika moja niweze ku-list hapa kwamba katika ile orodha ya kwanza kwa Wilaya 28 na wananchi wote waliko wasikie ni kwamba ni katika Mkoa wa Tabora ni Wilaya ya Uyui...

**SPIKA:** Naomba ugawe katarasi tafadhali. Kanuni ndio zinakuruhusu hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, basi Waheshimiwa Wabunge wale wanaohitaji kujua kwamba Wilaya zao ziko katika awamu gani, basi nitagawa hizi karatasi.

**SPIKA:** Zigawe kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Na. 128

**Walimu Kuhama au Kutoripoti Katika Vituo vya Kazi**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Walimu wanaopangwa kufundisha katika Halmashauri za Vijijini baadhi yao hawaripoti kabisa au huomba kubadilisha vituo vya kazi na hivyo kusababisha upungufu wa walimu katika maeneo hayo.

Je, Serikali inazisaidieje Halmashauri zenye matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zipo shule zenye uhaba wa walimu katika baadhi ya maeneo kutokana na walimu wanaopangwa katika maeneo hayo kutoenda au kuhama katika vituo vya kazi kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hupanga walimu katika Halmashauri kulingana na upatikanaji wa walimu na upungufu uliopo. Halmashauri nazo hupanga walimu katika ngazi ya shule husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM II) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari( MMES II) imeweka vipaumbele vya kujenga nyumba za walimu katika maeneo ya Vijiji ili kuwavutia walimu kubaki katika maeneo hayo.

Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kushirikiana na Halmashauri zao kujenga mazingira vutivu ya kuwafanya walimu waweze kufika na kubaki katika vituo wanavyopangiwa. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina jumla ya wanafunzi 39,680, ina

shule 95 na ina walimu 760 tu na kwa kuwa mwaka 2010 Manispaa ya Songea ilipokuwa ikiongeza mipaka yake ilihama na walimu 200 na kata mbili na shule 6 ambazo mpaka sasa Serikali inahesabu walimu wale 200 wako bado katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na hivyo kutusababishia mgao mdogo na upungufu mkubwa wa walimu.

(a) Je, Serikali sasa iko tayari kwa kuzingatia uhamisho wa walimu hao 200 kuniongezea mgao wa walimu kutoka idadi ya walimu 10 tu tulioletewa kwa mwaka huu mpaka wale walimu 200 ambao wamehamia katika Manispaa ya Songea? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa suala la kuangalia mazingira ya walimu siyo kazi haswa ya Halmashauri zetu na siyo tatizo la makazi tu ni pamoja na mazingira magumu na maisha magumu yaliyoko vijijini. Je, ni lini Serikali itafanya maamuzi ya kutoa *allowance* ya mazingira magumu kwa walimu ili iwe motisha kwa walimu wetu, kuishi katika maeneo ya vijijini na kuwafanya wapende kukaa na kuwafundisha watoto wa taifa hili la Tanzania ikiwemo watoto wa Jimbo la Peramiho? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyoeleza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba walimu walihama kwenda Halmashauri ya Songea Mjini, lakini walipohama maana yake hata zile shule tulizihamisha vile vile kuzipeleka Halmashauri ya Songea Mjini.

Lakini *data* nilizonazo hapa ni kwamba mwaka 2009/2010 walimu waliokuwa wamepanga shule za msingi ni walimu 28, na walimu wasioripoti ni 2 tu kwa sababu mbalimbali. Mwaka 2010/2011 walimu waliokuwa wamepangwa shule za msingi za Halmashauri ya Songea Vijijini ni walimu 7 na ni mwalimu mmoja tu ambaye hakuripoti.

Lakini kwa mwaka huu wa fedha tulipokuwa tunaponga walimu Halmashauri ya Songea Vijijini hatukuwapa walimu kwa sababu tuliona *teaching proportional ratio* inatosheleza hatukupanga walimu na hivyo hakuna walimu ambao hawakuripoti. *(Makofi)*

Hata hivyo kutokana na Kata hizo za Lilambo na Tanga kumegwa na kuingizwa kwenye Manispaa ya Songea Kata hizi mbili zilikuwa na shule 12 zenye walimu 220. Kama ukichukua walimu wale 220 waliohamia Manispaa ya Songea na walimu waliopo sasa wanakuwa ni 760.

Kwa hiyo, utakuta hata ile *teaching ratio* bado inaweza ikawa inatosheleza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama aweze tu kujua kwamba tulichokifanya ni sahihi na ile *teaching ratio* sasa hivi kwa mfano shule za sekondari ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 24 kitu ambacho kwenye Halmashauri nyingine ni haba kabisa.

Kwa hiyo, bado aendelee kuona kwamba tunathamini hilo na Halmashauri ya Songea Vijijini walimu wanatosheleza.

Swali lake la pili kuhusu *allowance* kwa walimu kwenye mazingira magumu, mwaka jana Mheshimiwa Kawambwa Waziri wangu aliahidi hapa kwamba tumepata fedha za kuwapa walimu kitita cha bahasha cha 500,000 kwa ajili ya mazingira magumu.

Mpango huo ni kweli bado upo lakini hizi Wizara mbili TAMISEMI na Wizara ya Elimu tumekaa tumeona kwamba tuendelee kuangalia uwezekano vizuri kwa sababu tumeona kwamba labda tukigawa zile fedha kwa walimu watakaokuwa wameripoti mwaka huu tu tutaleta kweli vurugu kwenye mashule. Kwa hiyo, tunaangalia uwezekano wa kuangalia mazingira magumu kiujumla kwamba labda isiwe bahasha tu ya hela kuwe na mazingira mengine ambayo ni endelevu.

Ukimpa mwalimu shilingi 500,000 leo na mwalimu atakayekuja mwaka 2013 akakosa ile hela na Serikali zile hela ilipata kwa ajili ya mpango wa mwaka mmoja tu, tumeona kidogo itakuwa ni vurugu huko kwenye mazingira ya kazi.

Kwa hiyo, tunaangalia uwezekano mwingine wa kuweza kuzigawa zile fedha ili iwe mwalimu atakayekuja mwaka mwingine akute zile hela ili ziweze kumfaidisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika 10 zimetumika kujibu hilo swali. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Assumpter Mshama, atauliza swali hilo. *(Makofi)*

Na. 129

**Ugonjwa wa Mnyauko ya Migomba**

**MHE. ASSUMPTER NSHUNJU MSHAMA** aliuliza:-

Ugonjwa wa mnyauko unaoshambulia migomba asili ya ndizi zinazotumiwa kwa chakula na wananchi wa Bukoba kuharibika na

kuashiria kutoweka kabisa kama hatua za makusudi hazitachukuliwa kupambana na ugonjwa huo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti wa ugonjwa huo na hata kuutibu kabisa hasa ikizingatiwa kuwa nchi jirani wamefanikiwa kuutibu kabisa ugonjwa hou?

(b) Je, Serikali imefanya utafiti juu ya migomba mipya ya FHIA ambayo Wizara imeipeleka kwa wananchi lakini inaonekana tishio kwa kuangamiza migomba asili?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu ugonjwa huu uingie Tanzania, Wizara kupitia kituo cha utafiti wa mazao ya kilimo cha Maruku, imefanya utafiti na kugundua kuwa ugonjwa huu unasababishwa na *bacteria* aitwaye kwa kitaalam *(Xanthomonas compestris pv musacearum).* Ugonjwa huu unashambulia aina zote za migomba ile ya asili na ile ya kutoka nje au *(exotics)* pamoja na migomba chotara *(hybrids).* Utafiti uliofanywa katika kituo chetu cha Maruku na hata nje ya Tanzania haujafanikiwa kupata tiba ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu husambaa kupitia wadudu kama nyuki, vipando, au mbegu, vifaa vinavyotumika shambani na katika kuhamisha sehemu yeyote ya mgomba ulioathirika kwenda sehemu nyingine.

Ili kudhibiti ugonjwa huu, wakulima lazima watumie vipando safi kutoka kwenye vituo vya utafiti kama Maruku na vituo vingine ambavyo vimewekwa katika kila Wilaya ya Mkoa wa Kagera au kutoka kwenye mashina yasiyo na ugonjwa. Kuondoa maua ya kiume wiki moja baada ya ndizi kuchanua ili nyuki wasitembelee mikungu. Migomba yenye kuonyesha dalili za ugonjwa ing'olewe na kuteketezwa au kuifukia chini ya ardhi au kuchomwa moto na vifaa vilivyotumika kwenye shamba lenye ugonjwa visafishwe kwa kutumia dawa ya aina ya jiki au sehemu yake ile chuma kuchomwa moto mpaka iwe nyekundu. Wakulima wawe waangalifu katika kuazimana vifaa kama mapanga na majembe wanayotumia katika mashamba.

(b) Mheshimiwa Spika, utafiti umefanyika kuhusu migomba mipya ya FHIA ambayo ni migomba chotara yenye tija mpaka (tani 100 kwa hakta ikilinganishwa na tani 60 kwa hekta kwa migomba ya kienyeji iliyowekewa mbolea ya kutosha). Mizizi ya FHIA huenda zaidi ya futi tatu na husambaa hadi futi tano kutoka kwenye shina.

Hali hii huifanya migomba hii kuwa na uwezo mkubwa wa kushindania virutubisho ikilinganishwa na migomba ya asili. Wananchi wanashauriwa wapande migomba hiyo kwenye mashamba tofauti na yale mashamba yenye migomba ya kienyeji au wanapoipanda ipandwe kwenye mitaro ya kina cha futi mbili ili kuitenganisha migomba ya asili na migomba hiyo chotara.

**MHE. ASSUMPTER NSHUNJU MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nasikitika kwamba sikupata jibu la kunitia moyo ukizangatia kwamba maelekezo yote aliyoyatoa yanahitaji uwezesho ili watu waweze kununua hizo jiki wapate elimu hiyo hiyo ya namna gani ya kutunza hiyo migomba, kitendo ambacho naona lita moja jiki ni shilingi 6,000/=.

Mheshimiwa Waziri je, unaweza kutusaidia kuiweka katika ruzuku hiyo, hiyo dawa ili wananchi wote waweze kununua na kutibu migomba na kuweza kusaidia migomba yao? *(Makofi)*

Swali la pili. Mheshimiwa Spika, katika nchi ya Uganda jirani zetu wameweza kuthibiti ugonjwa huo na matokeo yao sasa hivi wanamenya ndizi na kuzi-*export* Marekani kama chakula kwa watu wengi.

Je, Serikali inaona vipi kunisaidia wananchi wangu wa Nkenge na Maafisa Ugani kwenda Uganda kujifunza hizo njia ambazo wenzetu wanatumia ili wakirudi wawafundishe wananchi na tupate ndizi zetu za asili kama kawaida? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, njia ambazo nimezitaja za kupambana na *bacteria* wa ugonjwa huu ziko ambazo ni ghali kama hiyo ya jiki. Lakini kama huwezi kununua jiki unaweza kuwasha moto ukachoma panga lako au vile vifaa unavyotumia mpaka likapata moto na kuwaua wadudu wale.

Aidha sehemu za mgomba ambazo zimepata athari unaweza kuzichimbia shimo na kuzizika chini au kuzichoma moto bila kutumia fedha zozote kutoka kwenye pesa za familia.

Mheshimiwa Spika, umuhimu ni kuhakikisha kwamba hatua hizi ambazo tumezipendekeza zinafuatwa na zinafuatwa kwa ukamilifu na kwa umakini sana. Ni muhimu sana mashamba yawekwe katika hali ya usafi. Hata ukitembelea mashamba yale ambayo nimeyatembelea mimi kule kwenye Wilaya ya Muleba wale ambao wameweka mashamba yao kwa hali ya usafi migomba yao bado iko salama.

Mheshimiwa Spika, Uganda wamefuata utaratibu huu vizuri na wameweza kuudhibiti ugonjwa huu. Hata hivyo bado utafiti unaendelea. Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya anayotoka Mheshimiwa Mbunge Assumpter Mshama ili kupeleka kikundi cha wakulima hao na Madiwani waweze kuona wenzao Uganda wanavyofuata hizi kanuni ili tuweze kuwapa uwezo nao wawasaidie wakulima wetu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Tatizo la magonjwa katika mazao ni kubwa sana hasa katika Wilaya ya Kilombero na Ulanga kuna ugonjwa mkubwa sana kule kwetu unaitwa kimyanga au ugonjwa wa manjano.

Je, Waziri ananiambiaje kuhusu ugonjwa wanaoupata wakulima wa mpunga katika Wilaya ya Kilombero na Ulanga kwa miaka mingi takriban sasa hivi tangu nilivyokuwa mdogo mpaka leo haujapatiwa ufumbuzi. Ananiambiaje kuhusu utafiti wa ugonjwa huo na hatima ya kuwaokoa wakulima wa Wilaya Ulanga na Kilombero?

**SPIKA:** Kwa hiyo umekuwa *chronic* Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutokea hapa kujibu swali la Mheshimiwa Kiwanga, Mbunge kutoka kule Kilombero.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya huu ugonjwa anaouita kwa jina hili alilolitaja nisingeweza kujua hasa, hasa kiini cha ugonjwa huo ni kitu gani. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge afike kwenye Ofisi zetu tuzungumze atuletee na taarifa za ugonjwa huu ili tuujue halafu tutampa majibu namna ya kufanya. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ni kweli lilikuwa swali jipya. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, atauliza swali l inalofuata.

No. 130

**Uhitaji wa Mawasiliano ya Simu**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Mawasiliano ya simu ni muhimu sana katika kuchangia maendeleo ya wananchi, lakini licha ya umuhimu huo, Kata za Mihambwe, Mkoreha Napula, Michenjele na Kitama zina tatizo kubwa sana la mawasiliano hasa ya simu za mkononi:-

Je, Serikali inawasaidiaje wananchi wa maeneo hayo kupata urahisi wa mawasiliano kwa kuwawekea minara ya simu za mkononi kwenye Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mawasiliano ya simu yana umuhimu katika kuchangia maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha, Serikali inaendelea kufanya juhudi za makusudi kwa kushirikiana na makampuni yote ya mawasiliano ya simu nchini ili kuhakikisha huduma hiyo inawafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, aidha, mnamo mwezi Julai mwaka 2011, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF)* uliorodhesha maeneo yote yanayohitaji mawasiliano kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuanza upembuzi na hatimaye kupeleka huduma husika. Napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mchakato huo umeanza kwa kutangaza zabuni mnamo mwezi Septemba mwaka 2011, ambapo Kampuni moja tu iliwasilisha maombi kwa ajili ya kufanyiwa tathmini. Kutokana na kampuni hiyo kutokidhi matakwa ya zabuni mfuko utatangaza upya zabuni hiyo hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa licha ya juhudi za pamoja zinazoendelea kati ya Serikali na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinafika maeneo yote nchini, Serikali itayahimiza makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini yaweze kuweka katika mipango yao ya kufikisha huduma za mawasiliano kwa wananchi wa Kata za Mihambwe, Mkoreha Naputa, Michenjele, Kitama

pamoja na maeneo mengine nchini yasiyokuwa na huduma za mawasiliano.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya jumla sana lakini naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kampuni iliyokuwa *Celtel* iliahidi kujenga minara mipya mitano Wilayani Tandahimba ikiwa ni pamoja na maeneo haya ya Kata nilizozitaja lakini iliweza kujenga tu minara mitatu ambayo ni Mkwiti, Luagala na Mchichira. Baadaye kampuni ya *Celtel* ikauzwa.

Tukatarajia kwamba kampuni ya *Zein* ingekamilisha kwenye maeneo haya yaliyobaki. Lakini hata hivyo hawakufanikiwa na baadaye ikauzwa tena kwa kampuni ya *Airtel.*

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwaahidi wananchi wale wenye tatizo la mawasiliano kiasi hiki kwamba sasa atawasukuma kampuni zilizopo ili kupata mawasiliano haraka iwezekanavyo?

Pili, kwa kuwa maeneo yenye mawasiliano sasa hivi kumejitokeza tatizo katikati ya mazungumzo simu inaweza ikakatika hivyo kulazimisha upige tena jambo ambalo linaongeza gharama. Lakini sambamba na hilo kumejitokeza tatizo la haya makampuni ya simu kutuma *message* tusizozihitaji wateja wao na hivyo kuleta usumbufu usio wa lazima. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliahidi Bunge hili na Taifa kwa ujumla kwamba marekebisho yatafanyika haraka ili kuondoa usumbufu huo tunaoupata na gharama zinazoongezeka kwa kulazimisha kupiga tena simu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, suala la kwanza kuhusu kuyasukuma haya makampuni kuhakikisha ya kwamba yanaweka minara katika maeneo yaliyokuwa yameahidiwa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge nitafuatilia na wenzetu wa *Airtel* tuone wamefikia wapi katika mchakato wa kuweza kuweka minara katika maeneo hayo.

Lakini la pili, amezungumzia suala la simu kukatika katikati wakati unaongea. Nipende tu kuliarifu Bunge lako Tukufu tena kwamba tumezungumza na hawa, *Chief Technical Officers* wa makampuni haya makubwa ya simu kuona tatizo hasa ni nini linalojitokeza katika hii hali ambayo inajitokeza. Lakini tumekuja kugundua kwamba hata kwa

kuangalia kitakwimu, mwaka 2008 watumiaji wa simu walikuwa milioni 13 mwezi Desemba.

Lakini mwaka 2011 Desemba, walifika milioni 25.8 karibu milioni 26. Utaona ongezeko ni kubwa sana. Karibu mara mbili ya pale na ukiangalia katika miaka hii ya 2008, 2009 mpaka 2011 kulikuwa na kushuka kwa gharama za kupiga. Walianza shilingi moja, wakaja nusu shilingi, wakaja robo shilingi. Katika hali ya kuyumbayumba kwa biashara namna hii makampuni mengi yalisita kuwekeza katika minara.

Kwa hivyo sasa hivi tumezungumza nao na wametuhakikishia kwamba watawekeza na kutakuwa na *improvement* kubwa sana kufikia *December*, kwa yale ambayo wametueleza sasa hivi.

Lakini kuhusu hili suala la *SMS,* ni kweli. Basi naomba nilichukue hili ili niweze kuzungumza nao tena hawa wenye makampuni tuone ni kwa namna gani wapunguze au waondoe kabisa hili suala la kuwatumia *SMS* watu bila kuzitaka. *(Makofi)*

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali imejipanga vipi kuangalia ubora wa simu zinazoingizwa nchini kwetu ili zisije zikaleta athari kwa watumiaji baadaye? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli simu zisizokuwa na ubora zinaweza zikachangia kuleta matatizo kwa wananchi. Sisi kama Wizara kwa kutumia *TCRA* kuna viwango ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kuingiza nchini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakapokuwa ameona aina ya simu tutaomba atusaidie kutuletea hiyo simu ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaipeleka *TCRA* kuthibitisha ubora wake, uchekiwe kwa kushirikiana na wenzetu wa *TBS* tuweze kuhakikisha kwamba simu kama hizo zinapigwa marufuku kuingia hapa nchini.

Na. 131

**Serikali Kutenga Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Uwekezaji kwenye mgodi wa *North Mara,* uliopo Nyamongo umesababisha adha kubwa kwa wananchi, ikiwemo ukosefu wa ajira kwa uchimbaji mdogo wa madini ambacho ndicho chanzo kikubwa cha mapato hayo na kwamba Serikali imeshaahidi kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini:-

(a) Je, ni lini maeneo hayo yatatengwa na kugawiwa kwa wachimbaji wadogo wadogo kuchimba madini?

(b) Je, maeneo yatakayogawiwa yamefanyiwa upembuzi yakinifu kubaini kama kuna madini ambayo yatafikika kirahisi na kuleta tija kwa uchimbaji mdogo mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uchimbaji madini nchini mwetu ni miongoni mwa mifumo ya nchi chache duniani ambayo inatambua mchango wa sekta ndogo ya uchimbaji madini kwa maana ya *(Artisanal Mining)* na kufanya jitihada za makusudi za kuirasimisha kwa misingi ya kisheria na Sera.

Huu ni mkakati ambao una misingi yake kwenye Ilani ya Uchaguzi na Wizara yangu imekuwa ikiupatia utekelezaji kwa mipango mbalimbali. Miongoni mwa mipango hiyo ni kutenga na kugawa maeneo, kulingana na tathmini za kitaalam na uhalisia wa maeneo hayo kuweza kukidhi vigezo vya kijiolojia, kiuchumi na kimazingira ya uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga maeneo yafuatayo kwa ajili ya uchimbaji mdogo mdogo wa madini hivyo basi kama ambavyo Wizara yangu imekuwa inafanya kwa maeneo mengine ya nchi yetu. Mpambaa na Maruga Wilayani ya Iramba, Mwau maeneo ya Singida Vijijini na Itandula, Mogabiri na Gibaso Wilayani Tarime. *(Makofi)*

Kwa sasa mchakato wa kutoa leseni kwa ajili ya eneo la Itandula unaendelea katika Ofisi ya Madini ya Kanda iliyopo Mwanza. Aidha,

kwa maeneo ya Mogabiri na Gibaso mazungumzo yanaendelea na kampuni ya Barrick ili iweze kuachia eneo hilo ambalo liko chini ya leseni lake. Kabla ya maeneo hayo kutengwa, maeneo hayo yalikuwa chini ya utafutaji madini ya dhahabu ambayo kutokana na takwimu zilizopo, yana rasilimali ya madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati yake ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo katika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini kwa kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwahamasisha wahimbaji kufanya kazi katika utaratibu utakaowawezesha kupata mikopo kwa jili ya mitaji ya riba nafuu na kutoa mafunzo ya namna bora ya kufanya uchimbaji kwa kutumia vifaa na taaluma zinazoongeza ufanisi na tija ili iweze kuinua kipato chao. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nasikitika sana na majibu ya Naibu Waziri. Swali langu la msingi nilimaanisha maeneo ya Nyamongo, mgodi wa *North Mara.* Maeneo yaliyoainishwa kwenye jibu lake la msingi ni maeneo ambayo yako mbali kabisa na ni maeneo ambayo ni *Local Mining* ambazo ni mfu kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba alijibu nje ya swali la msingi. Ningependa kujua mpaka leo ni wachimbaji wadogo wangapi ambao wameshapatiwa leseni au wapo kwenye huo mchakato wao wa kila siku wa kuwapatia leseni?

Swali la pili, mwaka jana mwezi wa tano kulitokea mauaji Tarime, watu waliuawa, Mawaziri wengi walienda na wakaahidi kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo maeneo ya kuchimba katika eneo la *North Mara.* Mpaka leo hii ninavyoongea takribani mwaka mmoja, hamna wachimbaji wadogo wadogo waliopatiwa eneo la kuchimba.

Natakakujua, je, Serikali ilienda Wilayani Tarime kuwahadaa wananchi wa Tarime?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anasema Serikali imeshatoa maeneo mangapi ya uchimbaji mdogo?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa maeneo kwenye Wilaya zisizopungua tisa za Mererani, Kilindi kwa Mheshimiwa Beatrice, Winza, Nyarugusu, Rwamgasa na Maganzo Kishapu kule. Kwa hiyo, maeneo

yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni mengi, lakini kabla hujatoa eneo la uchimbaji mdogo, hutoi eneo la uchimbaji mdogo kwa sababu umeomba, unatoa maeneo ya uchimbaji mdogo kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kuna vigezo vya kijiolojia, vya kiuchumi na vya kimazingira. Kwa sababu, hawa wachimbaji wadogo kama walivyokuwa wachimbaji wakubwa, wote wana wajibu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uchimbaji Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yapo maeneo ambayo kijiolojia hayafai kwa uchimbaji mkubwa na yapo ambayo hayafai kwa uchimbaji mdogo. Kwa hiyo, kazi hiyo tumeipa Wakala wa Jiolojia Tanzania, inayafanyia kazi na mara inapobaini maeneo hayo na tunapobaini kwamba leseni zilizokuwepo hapo ni za ubabaishaji, tumejikita kunyang'anya leseni hizo na kuwapa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, sasa ameuliza kama Mawaziri walipokwenda kule Tarime, walikwenda kwa ajili ya kuwahadaa wananchi. Mimi nadhani *that is not fair.* Wewe unafahamu kwamba, yapo maeneo ambayo awali yalikuwa yametengwa katika Wilaya ya Tarime na yale maeneo ya Nyamongo yana mgogoro, lakini yapo maeneo ndani ya Nyamongo ambayo yanasimamiwa na *African Barrick Gold,* ambayo tayari yameshabainishwa kwamba hayana misingi ya kuchimba uchimbaji mkubwa. Kwa hiyo, tupo kwenye mazungumzo ili pale ufanyike uchimbaji mdogo, maeneo wapewe na wapewe pia katika utaratibu ambao unawezesha uchimbaji endelevu, siyo uchimbaji wa holela.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kutoa maeneo kwa wachimbaji wadogowadogo; na kwa kuwa taratibu za *EIA* zinajulikana kwa hawa wachimbaji wakubwa *(investors):-*

Je, ni nani ndiye atakayekuwa na dhamana ya uharibifu wa mazingira na kufukia mashimo katika maeneo ya wachimbaji wadogowadogo ambayo inaonekana kuwa yanakuwa mengi na uharibifu wa mazingira unakuwa mkubwa; ni wachimbaji wadogowadogo ambao hawana uwezo au ni Serikali? Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mnyaa kwa kuuliza swali hili kwa sababu hata kwenye majibu yangu ya msingi nimesema kwamba, hata wachimbaji wadogo wana wajibu wa kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwenye uchimbaji mkubwa kuna kipande cha Mkataba kinachoelekeza kwamba, baadhi ya pesa yao itaelekea kwenye kutunza hiyo *Environmental Protection Fund,* ambayo ipo. Sasa tunasema kwenye uchimbaji mdogo, kama uchimbaji mdogo unafanywa katika mfumo endelevu, kutakuwa hakuna tatizo kwa sababu mapato yatakayopatikana pale yatakwenda pia kurekebisha uharibifu wa mazingira unaofanywa. Kama uchimbaji mdogo ule unafanywa kiholela, sasa hapo ndiyo tatizo linapokuja. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema kwamba, uchimbaji mkubwa kama ilivyokuwa kwa uchimbaji mdogo, yote tunataka ifuate misingi ya sheria, ili yote kwa pamoja iwe na manufaa kwa nchi yetu kama tunavyotarajia na tunavyokusudia.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo ya Nyamongo ni sawasawa na yale yanayonipata pale Buhemba, ambapo ni karibu sana na Nyamongo; wachimbaji wadogowadogo walioko pale Buhemba, wana matatizo makubwa kuliko hata yale ya Nyamongo. Je, Mheshimiwa Waziri, atakuja lini pale Buhemba atatue tatizo la Buhemba moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod Mkono, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema pana matatizo pale Buhemba, lakini kwa sasa hivi *STAMICO,* wamekabidhiwa eneo lile ili walipatie utaratibu wa kuliendeleza.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba, kuna utaratibu *STAMICO* wamekwenda kuliangalia eno hilo. Labda niseme tu kwamba, wiki iliyopita Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, akiambatana na Kaimu Kamishna, wamekwenda kufuatilia matatizo yote haya; hilo la Buhemba na lile la shule tuliyoahidi kule kwa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, tutakwenda kuangalia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya yote yanafuatiliwa katika *level* ya utendaji. Tukirudi Dar es Salaam kesho, watatupa taarifa za safari yao

na Mheshimiwa Waziri ama mimi, mmojawapo atajipanga kwenda Buhemba na Mheshimiwa Mkono, kufuatilia suala hili kwa karibu.

Na. 132

### ***NSSF* Kuzalisha Umeme - Kiwira**

**MHE. ALIKO N. KIBONA** aliuliza:-

(a) Je, ni sababu gani zinasababisha mchakato wa kuliruhusu Shirika la *NSSF* linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja lenye uwezo usio na shaka kuingia ubia na kampuni nyingine ili kuzalisha umeme katika Mgodi wa Kiwira usikamilike?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha za walipa kodi kimelipwa kama mishahara, matibabu na kodi kwa watumishi wa mgodi na gharama za kulinda Mgodi huo wa Kiwira tangu Mwekezaji *Tan Power Resources* ashindwe kuendeleza Mgodi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifikia makubaliano ya kuingia ubia na Kampuni ya *Tan Power Resources* mwaka 2005 ya kuiuzia hisa Kampuni hiyo asilimia 70 za Mradi huo na Serikali yenyewe kubaki na asilimia 30. Kampuni hiyo ilitarajiwa kuwekeza katika uzalishaji wa umeme unaotokana na makaa ya mawe na kuunganisha kwenye Gridi ya Umeme ya Taifa. Kulingana na mpango wa awali wa *Tan Power Resources,* Kampuni hiyo ingeunganisha kwenye Gridi ya Taifa, umeme wa kiasi cha *MW 200* ifikapo katikati ya mwaka 2009 na hadi mwisho wa mwaka 2010, walitarajia kufikia uzalishaji wa jumla ya *MW 400.* Aidha, madhumuni na sababu iliyosababisha Serikali kuridhia ubia huu ni kwamba, uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe, ungekuwa wa gharama nafuu kuliko vyanzo vya mafuta, hasa kwa kuwa rasilimali hiyo ni yetu wenyewe na tunayo ya kutosha na hivyo basi, Mradi huo ungekuwa wa manufaa kwa Taifa kwa kuwapatia wananchi huduma iliyo ya uhakika na yenye gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Tan Power Resources,* ilishindwa kuuendeleza Mradi huo kwa wakati na hivyo Serikali kwa kutambua

umuhimu wa Mradi huo kwa Taifa, chini ya *Consolidated Holding Company (CHC),* ilianzisha mchakato wa kurudisha hisa hizo asilimia 70 za *Tan Power Resources* Serikalini. Tathmnini ya thamani za hisa za *Tan Power Resources* imekamilika na Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kurudisha hisa hizo Serikalini. Pamoja na hatua hizi, Kampuni ya *Tan Power Resources* baada ya kukabidhiwa Mradi huu, ilifanya jitihada za kuongeza mtaji kwa kukopa fedha kwenye taasisi za fedha.

*Tan Power Resources* mbali ya kushindwa kuzalisha umeme, ilishindwa kufanyia kazi zilizokusudiwa mikopo hiyo na sasa Mradi wa Kiwira unadaiwa zaidi ya bilioni 33. Aidha, madeni mengine zikiwemo haki za wafanyakazi zinafikia bilioni 23. *NSSF, CRDB* na *PSPF* ni miongoni mwa Taasisi za fedha zinazoidai *Tan Power Resources,* ambayo sasa haina uwezo wa kuendelea na Mradi huo. Ni kweli *NSSF* iliwasilisha maombi ya kumilikishwa Mgodi huu ili uweze kuingia ubia na kampuni nyingine na kuzalisha umeme kwa lengo la kurejesha fedha zilizoikopesha *TPR.*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kama nilivyosema, ni kweli Serikali imepokea maombi ya *NSSF* ya kumilikishwa Mgodi huo. Hata hivyo, Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za kutengeneza utaratibu utakaowezesha ushiriki wa Wadau mbalimbali katika mazingira ya uwekezaji huria kama inavyoruhusiwa na Sheria za Madini na Sera ya Nishati. Mikakati inayokusudiwa kuukwamua Mradi huu ni ushirikiano wa pamoja wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP).* Baada ya taratibu za Serikali za kurudisha hisa za Mradi wa Kiwira Serikalini kukamilika, wawekezaji walio na nia ya kuwekeza katika Mradi huo ikiwemo *NSSF* watakaribishwa kuungana na *STAMICO,* ili kuendeleza Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Kiwira, kwa mikakati ya kuihami nchi yetu na matatizo yanayotokana na ukosefu wa nishati ya umeme, Serikali ilichukua jukumu la kuutunza na kuulinda Mradi huo kuanzia mwezi Agosti, 2008 baada ya kuthibitika kuwa, *TPR* walikuwa wameshindwa kufanya kazi hiyo. Serikali ilichukua dhamana ya kuwalipa Wafanyakazi wa Mradi wa Kiwira malipo yanayojumuisha mishahara, ulinzi wa Mgodi na uendeshaji wa Ofisi. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Januari, Serikali ilikuwa imekwishakulipa jumla ya Sh. 3,214,359,411.00 kulipia huduma za Mradi huo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, masharti kwa mwekezaji ambaye atachukua Mgodi wa *Kiwira Core Mine* itakuwa ni pamoja na kumkabidhi au akubali madeni ya bilioni 33 kama ulivyoziainisha? Kama *NSSF* wameonesha nia ya kuchukua madeni hayo kwa nini tusipunguze urasimu kwa kuwakabidhi *NSSF* waanze kazi mara moja kwa faida ya umma? *(Makofi)*

(ii) Ili kuzalisha umeme katika Mgodi wa *Kiwira Core Mine,* mwekezaji yeyote atahitaji Mlima wa Kabulo ambao tayari Wizara ya Nishati na Madini imeridhia kwa *Tan Power* kuuza kwa Kampuni nyingine. Kwa kuwa mchakato wa kumilikisha Mlima Kabulo kutoka *STAMICO,* Serikalini kwenda kwa *Tan Power* na *Tan Power* kwenda kwa Kampuni hii mpya haukuwa halali ulikuwa batili; je, Serikali ipo tayari kuurudisha Mlima Kabulo Serikalini ili huu mchakato uanze upya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Aliko Kibona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Mradi wa Kiwira, lina mambo mengi; sasa naomba nijielekeze kwenye suala hili la kwanza juu ya masharti ya kulipa deni. Haya ni madeni ambayo *Tan Power Resources,* baada ya kupata zile asilimia 70 alijielekeza akachukua milioni karibu 17 kutoka Taasisi za Fedha kama hizi nilizozisema, kwa lengo kwamba, ifikapo 2009 azalishe umeme *MW 200,* 2010 aongeze *MW* zingine zile 200; kashindwa kufanya hivyo. Kwa maana hiyo ni kwamba, *in any economic interpretation* pesa zile hazikufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo deni lipo kwa Taasisi hizi za fedha na kwa bahati mbaya, Taasisi mbili katika hizi ni za Hifadhi za Jamii; kwa hiyo, ni pesa za Wastaafu. Kwa hiyo, ni kwamba, hakuna namna, zile pesa ni lazima zitafutwe zirejeshwe. Katika uwekezaji wowote ambao unaendana na kufungua Kiwira kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, hilo lazima liwe ni sharti la kwanza. Kwamba, ni lazima zipatikane zile bilioni 33 ili kwa wale *NSSF* na *PSPF,* wao pesa zao zirudi na kwa maana hiyo na *CRDB* nao wamo wamejificha humu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni sharti na kama alivyouliza kwa nini *NSSF* wasipewe; kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi, utaratibu wa kufungua Mradi huu katika uwekezaji unafanyika. *NSSF* wameomba, wameleta pendekezo lao, kwa bahati nzuri wamekuja kutuona mimi na Mheshimiwa Waziri; nimewaambia kwamba, kusema kweli kama kuna uwekezaji utafanywa Kiwira ni lazima tuufanye tofauti na ule wa *Tan Power Resources* ili sasa uwekezaji uanze, tunahitaji sana hizi *MW* 400.

Mheshimiwa Spika, swali la pili hili la Mlima wa Kabulo; Mlima wa Kabulo, una leseni tofauti na Mgodi wa Kiwira. Pamoja na kwamba, una leseni tofauti, Mlima wa Kabulo ndiyo wenye hazina ya kama tani milioni 80 hivi za makaa ya mawe kwa ajili ya uzalishaji wa kiwango hiki cha *MW* 400 unaokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba hili jambo tulifanye kwa sababu inaonekana kwamba, huu mkakati wa kuuza au kununua Mlima Kabulo, ulifanywa kufuatia ushauri wa kitaalamu ambao ulifika katika ngazi ya Waziri wa Nishati na Madini. Pamoja na hayo, inabidi turejee nyuma tuangalie tathmini iliyofanywa hapa. Ninaomba tu nisistize kwamba, leseni ya Kabulo, ilikuwa ni tofauti na leseni ya Kiwira, lakini hiyo haiondoi kwamba Kiwira ilikuwa inategemea Mlima wa Kabulo, kwa ajili ya uzalishaji huu mkubwa wa *MW 400.*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuongezea majibu kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona. Ninapenda kuongezea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufasaha kabisa ni kwamba, Mgodi wa Kiwira na Mradi wenyewe kama ulivyo, umerudishwa Serikalini. Umekabidhiwa *STAMICO,* ambaye anaendelea sasa hivi na utaratibu wa kuwapata waendelezaji wabia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kufafanua kuhusu mahusiano ya Mgodi, eneo la Kabulo na Kiwira. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, maeneo haya yametolewa leseni tofauti na tathmini iliyofanywa sasa hivi ambayo taarifa zake zipo *STAMICO.* Mgodi wa Kiwira kama ulivyo, unaweza kuendelezwa kwa kiwango cha uzalishaji wa umeme ambao tumeukusudia bila kutegemea eneo la Kabulo; taarifa zipo Serikalini na zipo *STAMICO,* ni tathmini iliyofanywa kuanzia mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, eneo limekuwa na mkanganyiko sana; yapo mawazo kuwa kuna watu wanadhani kwamba, eneo la Kabulo lilitolewa kimakosa. Historia yake ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Kibona, eneo la Kabulo kabla ya Sera zote walizozibadilisha mwaka 1998, kabla hatujaitunga Sheria Mpya iliyotenguliwa na Serikali mwaka 1997, maeneo yote haya yalikuwa chini ya Serikali. Baada ya kubadilisha Sera, kila mwekezaji katika Sekta ya Madini, alipaswa sasa awe na leseni; hivyo, *STAMICO* walipaswa kuomba leseni kama waombaji wengine.

Mheshimiwa Spika, eneo la Kabulo, lilitolewa kwa *STAMICO,* lakini ilipofika wakati wa kuhuisha eneo hilo kwa sababu leseni ilikuwa inatolewa, ikishafika kipindi cha kwanza kuja kuomba ifanyiwe *renewal, STAMICO* bahati mbaya kipindi kile ilikuwa chini ya Taasisi iliyokuwa inasimamia ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. *STAMICO* ilishindwa kulipia ada inayopaswa ili kulihuisha eneo. Kwa hiyo, baada ya kushindwa eneo hilo likatoka mikononi mwa *STAMICO.* Baada ya kuwa wazi kuna Kampuni moja ya *Bandu Marbles,* ikaomba hilo eneo ikapewa, lakini nayo kwa sababu ambazo hazikueleweka ilishindwa kuliendeleza, ikapewa *Default Notice* kwa utaratibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, baada ya *Bandu Marbles* kushindwa ku-*rectify* hiyo *Default Notice* iliyokuwa imepewa, ikanyang'anywa eneo likabaki wazi, ndipo eneo hilo likaombwa na Kampuni ya *Tan Power Resources,* ikapewa hiyo leseni. Ilipopewa leseni hiyo ikafanya tathmini ya utafiti wa kijiolojia ikajiridhisha kwamba, eneo lile lina madini ya kutosha; ikaomba *Special Mining License,* ikapewa. Ndani ya kipindi hiki ambacho ina uhalali wa kulimiliki eneo hilo, ika-*transfer* eneo hilo kwa Kampuni ya *TANZACOL* kama ambavyo wamiliki wa leseni wamekuwa wakifanya nchini kote; haya maeneo, *assets* hizi ni *transferable,* unaweza kuzi-*assign* ama kuziuza. Kwa hivyo, hali ya sasa iliyopo, eneo hilo la Kabulo linamilikiwa na Kampuni ya *TANZAPOL* na utaratibu uliofuatwa ni wa Kisheria. Nakumbuka Mheshimiwa Zitto ni Mwenyekiti wa Kamati, wakati fulani alihoji jambo hili tukatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu na Watanzania waliopo kuwa, mchakato uliotumika kufikisha eneo hili katika Kampuni ya *TANZACOL* ni utaratibu unaotumika kuhalalisha leseni; zingine zikiwa zinamilikiwa na baadhi ya Wabunge kuzi-*transfer* kwa wamiliki wengine ndani ya utaratibu wa Kisheria kwa kadiri ambavyo wanapenda.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa.

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa.

**SPIKA:** Kwanza utaratibu. Waheshimiwa Mawaziri, mkikuta maswali ya nyongeza yanaulizwa yana uzito wa kutosha, mnaingia mara moja, kwa sababu tunatumia muda isivyotakiwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Aah, hatuna mjadala sasa hivi, sijafunga maswali. Kwanza, nitoe taarifa kwamba, maswali nimeshamaliza na yamekwisha.

Mheshimiwa Zitto, taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, suala la Mgodi wa Kiwira, Kamati yangu imelishughulikia kwa kina sana na ninasikitika kwamba, maelezo ambayo Naibu Waziri na Waziri wameyatoa, siyo ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Kabulo, ambao ulikuwa unamilikiwa na *STAMICO,* ulifanyiwa utafiti kwa fedha za mkopo, ambapo Serikali yetu ilichukua fedha kutoka Benki ya Dunia, zenye thamani ya Dola milioni sita. Siyo kweli kwamba, *STAMICO* walikosa Dola 200 za kulipia ku-*renew* leseni ile; isipokuwa *STAMICO* waliagizwa na Serikali na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, ambaye ndiye aliyekuwa mmiliki wa *Tan Power Resources* kwamba, wasi-*renew* leseni ile.

Wakati tunafanya utaratibu wa kuhamisha Mgodi wa Kiwira kwenda Serikalini, ilipaswa Serikali izingatie kwamba, Kabulo ilikuwa ni mali ya Umma na *Tan Power Resources* hawakuwa wamepaswa kupewa kwa utaratibu ambao umetajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupe taarifa na Serikali labda ituthibitishie hapa kwamba, licha ya kwamba Kampuni *Tan Power Resources* imeliingizia madeni kwa sabbabu madeni yote ambayo Naibu Waziri ameyataja yamedhaminiwa na Serikali kwa asilimia 85, kwa hiyo siku ya mwisho ni deni la Serikali. *(Makofi)*

Licha ya *Tan Power Resources* kuiingizia Serikali hasara ya madeni hayo, Serikali bado imeridhia kuilipa shilingi bilioni tisa kama *management fee* ku-*manage* mgodi ambao wameuharibu, wameshindwa kuuendeleza. Katika hili Serikali imeshindwa kuwajibika kulinda rasilimali za umma na ni lazima iwajibishwe kwa jambo hili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Eeh! Tunatulia, tunafanya kazi kwa utaratibu. Sasa ninachokisema ni kwamba, maelezo aliyosema Mheshimiwa Zitto ni

mazito, mnaweza kuleta kwa maandishi ili Serikali iweze kujibu. Kwa hiyo, naagiza kwamba, yaletwe kwa maandishi Serikali ijibu, kwa sababu nikisema Serikali ijibu tunaanza ubishi hapa sasa hivi na mimi nisingependa ubishi, lete hayo maneno vizuri tuyapate majibu yake inavyostahili. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, maelezo haya yapo kwa maandishi, Kamati iliwasilisha kwako.

**SPIKA:** Naomba uyalete kwa Spika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kwa hiyo nilete upya?

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, tutaleta upya.

**SPIKA:** Tafadhali, Waheshimiwa Wabunge, wageni nilionao hapa Bungeni; naomba mkae chini nifanye kazi yangu halafu mtafanya utaratibu unaostahili.

Wageni tulionao hapa Bungeni, kwanza kabisa ni Mheshimiwa Risasi Mwaulanga, ambaye ni Balozi wa Amani katika Maziwa Makuu. Ahsante, karibu. Siku nyingine tunafikiri ofisi yangu ihusike sana kwa sababu hatukuhusika hapa.

Tuna wanafunzi 67 kutoka Chuo cha *CBE* Dodoma; wasimame walipo wote wanafunzi, ahsante sana. Kama nilivyosema juzi, ninyi ni majirani, mnaweza kuja wakati tunapokutana. Someni kwa bidii.

Tuna wanafunzi sitini walimu wawili na madereva wawili kutoka Shule ya Msingi Eckernford ya Tanga. Walimu na wanafunzi, naomba wasimame kutoka Eckerneford Tanga; ahsante sana, tunafurahi kuwaona na tunatoa pongezi kwa Eckernford maana naona wanafanya mambo makubwa, someni kwa bidii watoto.

Tuna wanafunzi kutoka Chuo cha St. John's cha Dodoma; wasimame, ahsante sana na ninyi ndiyo majirani zetu pia wakati wa vikao mnakaribishwa na tunawaombea heri msome kwa bidii hapo chuo kwenu.

Tunao pia wanafunzi 24 wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo cha St. John's, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Machali. Wako wapi hao?

Tunawakaribisheni sana, someni kwa bidii kwa sababu Taifa linawategemeeni. Ahsante sana, naomba mkae.

Mwongozo; Mheshimiwa Matiko, naomba tusirudishwe nyuma kwa sababu inabidi kwenda mbele.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kanuni namba 43, naomba mwongozo wako....

**SPIKA:** Inahusu nini?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri wa Nishati na Madini anajibu swali langu la nyongeza la kwanza, nilikuwa nimeuliza kutaka kujua wananchi wangapi wachimbaji wadodo waliopatiwa leseni au ambao wapo kwenye mchakato wa kupatiwa leseni Tarime, lakini amenijibu kwa kutaja Wilaya zingine. Nilikuwa napenda ajibu swali langu kwa ufasaha. Ninaomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Kanuni gani, hebu soma kanuni uliyoniambia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 45(3), nimeomba mwongozo kwa kueleza swali langu ambayo inasema; iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi halijapata majibu, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge.

**SPIKA:** Basi Spika kama hajaridhika, kwa hiyo, mimi nimeridhika. Mheshimiwa Mchungaji Natse.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako, Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Hali kadhali, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kuhusu *Order Paper* ya leo na kuhusu ratiba ya Mkutano wa Bunge wa Saba. Katika *Order Paper,* Serikali ilipaswa kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ya Kamati Teule kuhusu Nishati na Madini. Leo tunafika mwisho na Bunge inaahirishwa na ikubumbukwe Serikali katika Mkutano wa Sita kwenye ratiba ilikuwepo siku ya kutoa taarifa haikutekelezwa, Bunge hatukuarifiwa. *(Makofi)*

Leo tunafika mwisho haitekelezwi na Bunge hatuarifiwi; Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA**: Umewahisha kazi ya Spika, tulikuwa tuweke katika Bunge hili utekelezaji wa Maazimio ya Kamati Teule niliyoiunda mwenyewe. Yale Maazimio walipoyaleta mimi Spika nimeyakataa, kwa sababu hayakukidhi hali inayostahili. Kwa hiyo, nimeyarudisha Serikalini wakayafanyie kazi tena halafu walete Bunge lijalo. Nimeyakataa mimi kwa sababu sikufikiri kwamba yamekidhi kile tulichokuwa tunategemea sisi, kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu na nilikuwa nasema hivyo.

Tunaendelea, Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusoma Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Haki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea wa Mwaka 2012 *(The Plant Breeder's Rights Bill, 2012).***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Moja ya taarifa ambayo nilitaka itolewe sasa hivi ni hii aliyouliza Mheshimiwa Natse juu ya majibu waliyotoa Serikali. Kwa hiyo, nimeagiza yafanyiwe kazi halafu na Kamati yangu ya Katiba pia itayafanyia kazi tutawasilisha Bunge lijalo. Nimeyakataa yale yaliyokuja.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo mengine niliyopenda kuyatoa ni kwamba, Kamati ya Uongozi ilikutana jana tarehe 22 Aprili, 2012 kupitia upya ratiba yetu inayoonesha kuwa tarehe 24 Aprili, 2012, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuwa shughuli hii ni kubwa na nzito hasa kwa kuzingatia changamoto zinazoikabili bajeti inayomalizika; ofisi yangu imeona ni vyema Kamati hii ya Mipango badala ya kutekeleza jukumu hilo la Kikatiba kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ndani ya Ukumbi huu wa Bunge, kazi hiyo ifanyike nje ya Ukumbi wa Bunge kwa msingi wa kutotawaliwa na masharti yaliyomo kwenye Kanuni za kudumu za Bunge. Kanuni hii ya 94 kwa miaka yote minne toka tuiandike kwenye Kanuni zetu imekuwa na ugumu wa utekelezaji. Kwanza, kanuni yenyewe inaelekeza kuwa tunajadili Mapendekezo ya Mpango na siyo Mpango wenyewe.

Pili, kutokana na maneno hayo ya Kanuni hii, kumekuwepo na mkanganyiko ni nini hasa kinachotakiwa Serikali iwasilishe Bunge na Bunge lizingatie nini. Hivyo, Kamati ya Uongozi imefikia uamuzi kuwa iangaliwe upya na suala la kuwa na Kamati ya Bunge ya Bajeti

liharakishwe na kwamba badala ya kukutana ndani ya Bunge kupitia Mapendekezo ya Mpango hayaleti manufaa yanayotarajiwa na hivyo tukutane katika Ukumbi wa Msekwa kama kamati ya Wabunge wote kujadili Mapendekezo ya Mpango wa 2012/2013.

Pia kwa kukutana katika Ukumbi wa Msekwa, tutatoa fursa kwa Maafisa Waandamizi wa Serikali, ambao ni Gavana wa Benki Kuu, Katibu wa Tume ya Mipango, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Wataalam wengine, kutoa maelezo ya kina juu ya Mapendekezo ya Mpango huu. Vilevile watasaidia kutoa ufafanuzi na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge; jambo ambalo ndani ya Ukumbi wa Bunge haliwezi kufanyika.

Hivyo basi, kabla Waziri hajaliahirisha Bunge, nitamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Uratibu na Bunge), aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili Kamati ya Wabunge ikae katika Ukumbi wa Msekwa kujadili Mapendekezo ya Mfumo wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2012/2013.

Waheshimiwa Wabunge, tulisema kwamba, tungekuwa na ile Kamati yetu ya Bajeti ndiyo ingekwenda kwa undani sana katika suala zima la huu Mpango, lakini tukikaa humu Wataalam hawawezi kuingia. Sisi wenyewe hatuwezi kufanya lolote, tunasema tu kama tunavyozungumza, ndiyo sababu Kamati ya Uongozi ilifikiria kwamba tuharakishe kuundwa ile Kamati yetu ya Bajeti, hata kama kuna masharti yake mengi lakini bado tuharakishe tuwe na changamoto ndani ya hiyo Kamati. Kwa hiyo, ingekuwa imeshatafuta wataalam, imefanya *research,* tukifika tunafanya kazi yetu kwa urahisi na kwa sababu hiyo namwomba Waziri wa Nchi, aweze kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

Kwa kuwa Kamati ya Uongozi iliyoketi tarehe 22 Aprili, 2012 chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Spika, iliamua kuwa shughuli zilizokuwa zimepangwa katika Mkutano huu wa Saba zimalizike leo tarehe 23 Aprili, 2012;

Na kwa kuwa katika Mkutano huu wa Saba, Bunge lilitakiwa kukaa kama Kamati ya Mipango kwa Mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilifikia uamuzi kuwa

endapo kazi hiyo itafanyika ndani ya Ukumbi wa Bunge itatawaliwa na masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

Na kwa kuwa tukitekeleza jukumu hilo kwa utaratibu wa kukutana ndani ya Ukumbi wa Msekwa, tutatoa fursa ya Maafisa Waandamizi ambao ni Gavana, Katibu wa Tume ya Mipango, Katibu wa Wizara ya Fedha na Wataalam wengine wote ambao Serikali itakuwa imewaleta kutoa maelezo ya kina juu ya Mapendekezo ya Mpango huo, jambo ambalo haliwezi kufanyika ndani ya Ukumbi wa Bunge;

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1), Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge, katika Mkutano huu wa Saba, Kanuni ya 84 itenguliwe ili Waheshimiwa Wabunge wajadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2012/2013 katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono sasa nitawahoji muiamue.

*(Hoja ilitolewa na iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni tajwa hapo juu iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda, vyombo vya habari pia vitakuwepo lakini uwezeshaji wa watu kuweza kuzungumza ndiyo hiyo tunayohitaji.

Nimeona ombi la matangazo kwa ajili ya vikao saa saba mchana. Ningependa kusema kuwa, saa saba mchana tuna shughuli fupi kabisa lakini ni muhimu kwetu, kutakuwa na Uzinduzi wa Mradi wa Kuwajengea Wabunge Uwezo, unaoitwa *Legislative Support Project.* Hii *Project* tulikuwa tumefanya utaratibu wa kukubaliana na *UNDP,* wakatoa ufadhili kwa ajili ya Bunge letu hili na Baraza la Wawakilishi. Hii ni *Project* ya miaka mitano ya kujenga uwezo kwa Wabunge. Leo tutafanya Uzinduzi ndani ya Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, ninawaalika Wabunge wote, saa saba mchana, wanaoweza kufika pale tuweze kuzindua huo Mradi. Huu ni Mradi wa miaka mitano lakini tunashirikiana Baraza la Wawakilishi na sisi chini ya utaratibu wa *UNDP*; kwa hiyo, naomba sana mfike pale.

Wenyeviti hao watajua wenyewe namna ya kufanya. Kwanza, Mheshimiwa Magaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, anaomba Wajumbe wa Kamati yake, wakutane saa saba katika Ukumbi wa Basement.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Zaynab Vullu, anaomba Wajumbe wa Kamati yake ya *PAC* wakutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa C. Sisi tutakuwa kwenye Ukumbi wa Msekwa, sasa mtaamua ninyi Viongozi namna gani iendelee. Katibu hatua inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

### Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira

**MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na kabla sijasoma Taarifa yangu, naomba marekebisho haya yaingizwe kwenye *Hansard.*

Ukurasa wa 45 na 84(A) badala ya Idara naomba isomeke Mkurugenzi wa Idara na ukurasa wa 49 na 88 kipengele 5(9) badala ya Dkt. Erasmus Tarimo naomba isomeke Dkt. Ladislaus Komba. Marekebisho haya yafanyike pia kwenye Taarifa kubwa ya Uchunguzi, ukurasa wa 89(7)(5)(a) na ukurasa wa 92(7)(9).

Mheshiwa Spika, aidha, utaona kwamba, katika Taarifa yetu viambatanisho havipo na hii ni kutokana na ukubwa wa viambatanisho hivyo; hivyo vitapatikana katika Maktaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kusoma Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Namba 114(15), Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kazi zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kipindi cha Aprili 2011 hadi Aprili 2012 ili iweze kujadiliwa na Bunge lako Tukufu na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ina sehemu mbili ambazo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Kawaida za Kamati na Taarifa ya Uchunguzi kuhusu Utaratibu Uliotumika katika Kukamata na Kusafirisha Twiga wawili nchi za

nje; na Utaratibu Uliotumika Kugawa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii kwa Msimu wa Mwaka 2013 - 2018.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, nitasoma vipengele muhimu tu na ninaomba Taarifa nzima iingizwe katika *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2011/2012. Mawazo na ushauri wao, umewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. James Daudi Lembeli, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Zakia Hamdan Meghji, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb | " |
| 5. Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb | " |
| 6. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb | " |
| 7. Mhe. Ali Khamis Seif, Mb | " |
| 8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | " |
| 9. Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb | " |
| 10. Mhe. Ali Abdallah Haji, Mb | " |
| 11. Mhe. Suzan Anselm Jerome Lyimo, Mb | " |
| 12. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb | " |
| 13. Mhe. Saleh Ahmed Pamba, Mb | " |
| 14. Mhe. Kaika Saning`o Telele, Mb | " |
| 15. Mhe. Amina Andrew Clement, Mb | " |
| 16. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | " |
| 17. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb | " |
| 18. Mhe. Bernadetha Kasabago Mshashu, Mb | " |
| 19. Mhe. Lediana Mafuru Mng`ong`o, Mb | " |
| 20. Mhe. Meshack Jeremiah Opulukwa, Mb | " |
| 21. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb | " |
| 22. Mhe. Kheri Khatib Ameir, Mb | " |
| 23. Mhe. AL-Shymaa John Kwegyir, Mb | " |
| 24. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb | " |
| 25. Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mb | " |
| 26. Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga, Mb | " |
| 27. Mhe. Mariam S. Mfaki, Mb | " |
| 28. Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mb | " |
| 29. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb | " |

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kifungu Na. 7 na 9(1), Toleo la 2007 kama ifuatavyo:-

- Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- Kushughulikia Taarifa za kila Mwaka za Utendaji za Wizara zilizo chini ya Kamati hii.

- Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 65(3)(b) ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa mwaka 2011/2012, ilipanga kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya mikutano mbalimbali ya Kamati na Watendaji wa Wizara husika ili kujadili na kutathmini shughuli za Kamati, shughuli za Wizara husika na kutoa mawazo, ushauri na maelekezo.

(ii) Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea Miradi ya Maendeleo na utekelezaji wa shughuli zilizo chini ya Wizara husika.

(iii) Kupitia na kujadili Taarifa za utendaji za Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(iv) Kuchambua Bajeti za Wizara husika.

(v) Kuchambua Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika**,** kazi za kawaida zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Aprili, 2011 – Aprili 2012:-

Kamati ilipata nafasi ya kufanya mikutano na semina mbalimbali katika nyakati tofauti kwa lengo la kuongeza upeo wa Wajumbe wa Kamati katika maeneo yanayohusu Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mnamo mwezi Aprili, 2012 Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa lengo la kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati kuhusu migogoro ya ardhi nchini.

Pamoja na changamoto nyingine zinazoikabili Wizara hii, bado baadhi ya Halmashauri zinazopewa fedha kwa ajili ya kupimia viwanja, yaani *revolving fund*, kutorudisha fedha hizo Wizarani kwa wakati; hivyo kukwamisha mpango wa Serikali wa kuendelea kutoa fedha hizo kwa Halmashauri za Wilaya nyingine nchini ili ziweze kupima ardhi na kuuza. Aidha, katika kipindi hiki, Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo:-

- Taarifa kuhusu ujangili wa tembo nchini, ambapo hali ya ujangili nchini imefikia kiwango cha juu. Hata hivyo, taarifa kuhusu ujangili ambayo ilitolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii haikukidhi haja na kuitaka Wizara kuandaa taarifa nyingine sahihi ili Bunge liweze kushauri hatua za kufanya;

- Taarifa kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya Wananchi wa Kijiji cha Shela (Urambo) na Hifadhi ya Msitu ya MPANDA LINE; na

- Taarifa kuhusu mgogoro wa Chuo cha Taifa cha Utalii.

Mheshimiwa Spika, lengo la semina kuhusu Mapitio ya Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 lilikuwa ni kutoa ufahamu kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu Sheria hii hususan kipengele kinachohusu uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu namna ya kukokotoa gharama za uhifadhi na tozo ya uchimbaji *(Concession Fee),* kwa kuchimba urani ndani ya Pori la Akiba la Sel*o*us, ililenga kutoa uelewa kuhusu mapato ambayo Serikali ya Tanzania inaweza kupata kwa kuruhusu uchimbaji wa Madini ya Urani ndani ya Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Spika, katika Semina hii, Kamati ilielezwa kuwa faida itakayopatikana kutokana na uchimbaji wa madini hayo ni pamoja na:-

- Kuiwezesha nchi kupata mapato ya moja kwa moja kutokana na kodi ya mapato, mrabaha, hisa za Serikali kwenye uwekezaji huo na tozo zingine;

- Kukuza ajira kwa Watanzania Wataalam na raia wa kawaida waliopo kwenye maeneo ya Wilaya ya Namtumbo na nchi nzima kwa ujumla;

- Kupata fedha za kuhifadhi Pori la Akiba la Selous. Fedha hizi zitatokana na fedha zitakazolipwa kwa ajili ya:-

(i) *Monitoring Cost* - gharama ambayo mwekezaji analipa siku kwa siku kutokana na uharibifu utakaotokea wakati shughuli za uchimbaji zikiendelea;

(ii) *Management Cost* - gharama za kiutawala ambazo mwekezaji anatakiwa kuzilipa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu hifadhini;

(iii) *Rehabilitation Cost* - pesa ambazo mwekezaji atatakiwa kuweka rehani *(deposit),* kiasi fulani cha fedha ambazo zitatumika kulifanyia ukarabati eneo la uchimbaji baada ya mkataba wa uchimbaji kumalizika; na

(iv) *Concession Fee* - fidia itakayotolewa na mwekezaji kwa kuikosesha fedha Wizara au Serikali, ilizokuwa inapata kabla ya kuanza kuchimbwa urani. Kwa mfano, eneo la Selous linalotegemea kuanza kuchimbwa urani ni eneo ambalo kwa sasa kuna vitalu vitatu vya uwindaji wa kitalii ambavyo vinaiingizia Serikali kiasi cha USD 90,000.00 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta mbalimbali nchini Tanzania ilitolewa na Wataalam mbalimbali kutoka Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa Kutokana na Ukataji Miti Ovyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) na Asasi mbalimbali zisizo za Kiserikali na ililenga kutoa uelewa kuhusu uhifadhi endelevu wa misitu unavyoweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi ndani na nje ya nchi. Athari hizo ni pamoja na kuongezeka kwa ukame, mvua zisizotarajiwa, kupungua kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro na kuongezeka kwa kina cha bahari. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kujifunza kuhusu Miradi ya Majaribio ya MKUHUMI, changamoto na mafanikio yake.

Mheshimiwa Spika, semina juu ya Hifadhi za Urithi wa Dunia ilitolewa na Tume ya Taifa ya *UNESCO* na ililenga kutoa uelewa kuhusu maeneo yenye vivutio vya kipekee yaliyohifadhiwa na Shirika la Uhifadhi la Dunia (*UNESCO*) nchini; taratibu zinazofuatwa ili eneo ama kivutio kiingizwe kwenye urithi wa dunia; hali ya maeneo yaliyohifadhiwa kama urithi wa

dunia; na utekelezaji wa Mikataba ya Urithi wa Dunia ambayo Serikali imeridhia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara mbalimbali ndani ya nchi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Mwanza na Tabora, kwa madhumuni ya kukagua utekelezaji wa maagizo au Miradi mbalimbali iliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Maeneo yaliyotembelewa yalijumuisha Migodi ya Dhahabu ya Barrick - Buzwagi na Bulyanhulu katika Wilaya ya Kahama na Mgodi wa Dhahabu wa Geita. Aidha, Kamati ilitembelea Kijiji cha Shela Wilayani Urambo, Chuo cha Wanyamapori Pasiansi, Shamba la Miti Buhindi - Sengerema, Hifadhi ya Taifa tarajiwa ya Kisiwa cha Saa Nane kilichopo Jijini Mwanza na Chuo cha Taifa cha Utalii - Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Migodi ya Dhahabu ya Bulyanhulu, Buzwagi na Geita ili kuona utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika Bunge la Tisa hususan uhifadhi wa mazingira. Katika ziara hizo mambo muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na:-

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kijiji cha Mwendakulima ambacho kinapakana na Mgodi wa Buzwagi na kukagua kisima kilichoko mita 50 kutoka Mgodini. Maji ya Kisima hicho yanatumika kwa shughuli za binadamu na mifugo. Maji hayo yanahofiwa kutokuwa salama kutokana na kemikali za shughuli za Mgodi. Aidha, Kamati ilipokea malalamiko kutoka kwa wanakijiji kuwa milipuko inayofanywa na Mgodi katika kupasua miamba inaathiri nyumba zao na nyingi zimebomoka.

Kamati pia ilitembelea Kijiji cha Mwime ambacho ni miongoni mwa vijiji vitatu vinavyozunguka Mgodi wa Buzwagi ambapo ilikutana na wananchi wa eneo hilo. Katika mkutano huo, kilio kikubwa cha wananchi kilikuwa ni Buzwagi kushindwa kukilipa kijiji hicho shilingi milioni 180 ambazo ni malimbikizo ya miaka mitatu, kwa ajili ya maendeleo ya Kijiji. Kijiji cha Mwime ndicho kilichokuwa kinamiliki leseni ya uchimbaji dhahabu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika**,** kufuatia malalamiko hayo, Kamati iliagiza Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya, ambao ndiyo msimamizi wa fedha hizo, kuhakikisha Barrick wanalipa fedha hizo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mgodi wa Bulyanhulu Kamati iliona aina ya uchimbaji unaofanyika ambao ni wa chini ya ardhi *(underground).* Kamati inapongeza uchimbaji huo ambao kwa kiasi kikubwa unasaidia kutunza mazingira tofauti na migodi mingine ya uchimbaji wa wazi *(open pit). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifurahishwa na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya Uongozi wa Mgodi na Wafanyakazi. Hata hivyo, hali ya uhusiano baina ya Vijiji na Mgodi bado hairidhishi kwani katika maeneo mengine migogoro kama vile ya fidia, bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa hapo awali, ziara ya Mgodi wa Geita pia ililenga kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati mwaka 2009, ikiwa ni pamoja na kuweka *liners* kwenye bwawa la kukusanya maji machafu, kufukia mashimo yanayoachwa wazi baada ya shughuli za uchimbaji wa udongo wenye madini, kupanda miti na kuboresha mahusiano kati ya jamii na Mgodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Bwawa la kutunzia maji machafu (*TFS*) kutokuwa na *liner* kwa madai kuwa mwamba uliopo chini hauwezi kupitisha maji hayo;

(ii) Utunzaji wa mazingira kwa ujumla katika eneo la Mgodi si wa kuridhisha; na

(iii) Mahusiano mabaya kati ya Mgodi na Jamii inayozunguka Mgodi.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Wilaya ya Urambo, Kijiji cha Shela, Kitongoji cha Luganjo Mtoni, ilifanyika ili kuthibitisha taarifa zilizotolewa Bungeni wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha Wananchi *(CUF)*, Mheshimiwa Magdalena Sakaya kuwa, kuna ukiukwaji mkubwa wa Haki za Binadamu uliofanywa na baadhi ya Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakishirikiana na Jeshi la Polisi na Mgambo, kuchoma moto nyumba za baadhi ya wakazi wa Kitongoji hicho, wanaosemekana wamevamia Hifadhi ya Msitu wa Mpanda Line. Kamati ilibaini kuwepo kwa baadhi ya nyumba za wananchi zilizochomwa moto na uelewa mdogo wa mipaka kwa wananchi, baadhi ya Watendaji wa Halmashauri na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliitaka Wizara kumaliza tatizo hilo haraka iwezekanavyo na wananchi wanaotuhumiwa kuvamia eneo la hifadhi

kuondoshwa mara moja. Aidha, Serikali iainishe mipaka halisi ya hifadhi, kuepusha wananchi kuvamia tena eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Shamba la Miti (Misitu) Buhindi Sengerema ilifanyika kufuatia malalamiko ya Wananchi wanaozunguka msitu kutonufaika na mapato yatokanayo na msitu ukizingatia uhifadhi mkubwa wa msitu huu unafanywa na vijiji vinavyozunguka msitu.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii changamoto zilizoibuliwa zilikuwa ni pamoja na mahitaji makubwa ya miti kuliko idadi inayoweza kupatikana na uwezo mdogo wa pesa na uhaba wa watendaji, hivyo kusababisha shughuli ya upandaji kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lengo la ziara ya Chuo cha Wanyamapori Pasiansi lilikuwa ni kukagua shughuli zinazoendeshwa na Chuo hususan kitengo kinachofundisha askari wa wanyamapori nchini na jinsi askari hao wanavyoandaliwa kutekeleza jukumu la kulinda rasilimali iliyomo katika maeneo yote yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na mbinu za kupambana na majangili.

Kamati ilisikitishwa na hali ya upungufu mkubwa wa askari wa wanyamapori na vitendea kazi. Pamoja na kuwepo kwa ujangili mkubwa katika eneo hilo, bado kituo kina gari moja tu la uhakika la kufanya doria.

Mheshimiwa Spika, ziara katika Hifadhi Tarajiwa ya Saanane ilifanyika hususan kwa ajili ya kujua mchakato wa kupandisha hadhi Kisiwa hicho kuwa Hifadhi ya Taifa. Waheshimiwa Wajumbe, walishauri mchakato huo uharakishwe ili Kisiwa hicho kiwe hifadhi kamili na hatimaye kiweze kuliingizia Taifa pato kubwa zaidi kwa njia ya utalii.

Mheshimiwa Spika, lengo la ziara ya Chuo cha Taifa cha Utalii lilikuwa kupata maelezo kuhusu Chuo kinavyotekeleza majukumu yake baada ya ujenzi wa Chuo kukamilika na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais tarehe 20 Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Kamati iligundua yafuatayo:-

- Kuwepo na tatizo la kiutawala kati ya Uongozi wa Chuo, Walimu na Wanafunzi;

- Ufunguzi rasmi wa Chuo ulifanywa na Mheshimiwa Rais huku baadhi ya mambo muhimu ya kukiwezesha Chuo kufanya kazi kwa ufanisi kutokamilika ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vitendea kazi;

- Uhaba wa walimu kutokana na wakufunzi wengi kuacha kazi ndani ya muda mfupi;

- Ada kubwa inayofanya Watanzania wengi kushindwa kujiunga na Chuo; na

- Chuo kutokuwa na *prospectus*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upungufu huo, Kamati iliitaka Serikali kurekebisha haraka dosari zilizopo chuoni hasa za kiutawala. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mara moja agizo hilo kwa kufanya mabadiliko ya Mkuu wa Chuo na inaendelea kurekebisha kasoro nyingi zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Shirika la Nyumba la Taifa na kupokea taarifa ya utendaji wa Shirika hilo. Kamati inalipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa kuwa na mipango mizuri ambayo Shirika imeanza kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika linatarajia kujenga nyumba 15,000 kati ya 2011 - 2015 na kazi ya ujenzi wa nyumba hizo imeanza katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za wazi za Shirika hilo, bado kumekuwa na madai ya baadhi ya wapangaji wa nyumba hizo kutaka kuuziwa baadhi ya nyumba za Shirika. Kamati haikubaliani na utaratibu huo, kwa kuwa nyumba hizo ni mali ya Watanzania wote.

**Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi ya Ardhi, Maliasili na Mazingira**

**MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Uchunguzi Kuhusu Utaratibu Uliotumika Katika Kuwakamata na Kuwasafirisha Twiga wawili kwa Kibali cha Wizara cha Tarehe 29 Aprili, 2011 na Kuchunguza Utaratibu Uliotumika Kugawa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii kwa Msimu wa Mwaka 2013 – 2018:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uchunguzi uliundwa na Wajumbe wanne wafuatao:-

Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Khamis Seif - Mjumbe, Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa - Mjumbe na Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Sekretaieti ya Kamati ya uchunguzi iliundwa na Maafisa wafuatao:-

Ndugu Mswige Dickson Bisile - Katibu wa Kamati, pamoja na Ndugu Hellen Stephen Mbeba, Ndugu Erick Sosthenes Maseke na Ndugu Rachel Nyambuli Nyega.

Kamati Ndogo ya Uchunguzi ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliundwa tarehe 14 Novemba, 2011 katika Mkutano wa Nne wa Bunge. Kamati hii iliundwa ili pamoja na mambo mengine, kuchunguza usahihi wa utaratibu uliotumika kuwakamata na kuwasafirisha twiga wawili ambao kibali chake kilitolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 29 Aprili, 2011 na kuchunguza utaratibu uliotumika katika zoezi la ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa msimu wa mwaka 2013 - 2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa Hadidu za Rejea tano zifuatazo, lakini nitasoma chache tu ambazo katika Taarifa hii zinapatikana:-

(a) Kupitia na kuchambua Sheria na Kanuni zinazosimamia biashara ya wanyamapori na nyara; na mfumo mzima wa biashara ya wanyampori hai na nyara ili kutoa maoni na mapendekezo ya kuboresha tasnia hii.

(b) Kuchunguza utaratibu uliotumika kukamata na kusafirisha Twiga wawili kwa kibali kilichotolewa tarehe 29 Aprili, 2011.

(c) Kuchunguza ushiriki wa Watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika biashara ya wanyamapori hai na nyara.

(d) Kuchunguza mchakato mzima wa utoaji na ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

(e) Kuchunguza jambo lingine lolote litakaloisaidia Kamati katika kutekeleza majukumu yake kuhusiana na biashara ya wanyamapori hai/nyara na ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi kwa kila hadidu ya rejea:-

Hadidu ya rejea ya kwanza iliitaka Kamati Ndogo kuchunguza Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia biashara ya wanyamapori hai na nyara, mfumo mzima wa biashara ya wanyamapori hai na nyara na

kutoa maoni juu ya Sheria, Kanuni, Mfumo na Taratibu zinazotumika katika biashara ya wanyamapori hai na nyara. Yaliyobainika ni kwamba:-

(a) Biashara ya wanyamapori na nyara inatekelezwa chini ya Sheria Na. 5 ya Wanyamapori na Nyara ya Mwaka 2009. Sheria hii ina sehemu 19 ambazo zimeainisha miongozo mbalimbali ya kuzingatiwa katika suala zima la biashara ya wanyamapori na nyara.

(b) Kifungu 51, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwa idhini ya Waziri wa Maliasili na Utalii, anaweza kutoa kibali cha kukamata mnyamapori ambacho kitatoa masharti ya namna ya kumkamata, tahadhari za kuchukua, utunzaji, ulishaji na kadhalika.

(c) Kifungu cha 58(1) kinamruhusu Mkurugenzi baada ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Waziri kutoa Kibali Maalum (*Special License*) kinachomruhusu mmiliki kuwinda, kukamata au kupiga picha wanyamapori.

(d) Kifungu cha 25(2) kinamtaka Waziri kuandaa Kanuni za jinsi Wanyama wa Taifa watakavyotumika kwenye masuala ya biashara. Kifungu hiki kinalenga kumpatia Waziri mamlaka ya kutengeneza Kanuni zitakazosimamia utumiaji wa Wanyama wa Taifa katika biashara mbalimbali ikiwemo kutumika kama nembo za biashara au nembo za bidhaa za biashara (*trademarks and product marks*).

(e) Kwa mujibu wa Kifungu cha 26(1), hakuna mtu yeyote atakayekamata, kuwinda, kujeruhi au kuua Mnyama wa Taifa bila idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.

(f) Kanuni ya tatu ya Kanuni za Ukamataji wa Wanyamapori *(GN 244/2010),* inaelekeza kwamba mmiliki wa leseni ya biashara ya nyara mwenye nia ya kukamata wanyamapori hai ataomba kibali cha kukamata wanyamapori hai. Kwa mujibu wa Kanuni za Biashara ya Nyara, mwombaji wa kibali cha kukamata wanyamapori hai anatakiwa kuwa na leseni za biashara ya nyara kuanzia daraja la 12, 13, 14, 15, 16 na 19. Hivyo, mwombaji anaweza kuomba leseni ya daraja moja au zaidi kati ya hizi.

(g) Pamoja na kwamba, Wizara ilitoa kibali kwa Kampuni ya *Jungle international* ili ikamate wanyama, hakuna ushahidi wowote wa kimaandishi kwamba *Jungle international* iliomba kwa mujibu wa Sheria, kukamata wanyama waliopo kwenye kibali cha Wizara cha tarehe 29 Aprili, 2011.

(h) Kinyume na matakwa ya Sheria kuhusu masharti ya ukamataji wa wanyamapori hai, wapo raia wa kigeni wanaomiliki kadi halali za ukamataji wa wanyama wakati sheria inakataza. Mfano mzuri ni Ndugu Kamran Ahmad, Raia wa Pakistani, ambaye ana Kadi Nambari 0016929 ya kukamata wanyama wakati sheria inakataza.

Maoni ya Kamati kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Mfumo Mzima wa Biashara ya Wanyamapori:-

(a) Adhabu zinazotolewa kwa mtu aliyefanya kosa kinyume na Sheria ya Wanyamapori haziendani na kosa lililofanyika kwa sababu hivi sasa adhabu zinazotolewa kwa ujumla siyo kali kiasi cha kumfanya mkosaji kujutia na kutorudia kosa (*lack of deterrence penalty*), yaani inatumika nguvu kubwa kumfikisha mhalifu kwenye mkondo wa sheria kuliko hatua au adhabu atakayopewa.

(b) Hakuna uelewa wa kutosha wa Sheria na Kanuni za Wanyamapori miongoni mwa Maafisa wanaosimamia utekelezaji wa Sheria hizo. Kwa mfano, Kamati iliwahoji baadhi ya Askari wa Kikosi cha Kuzuia Ujangili kwamba ni Sheria gani wanayoitumia katika utendaji wao; walijibu kuwa wanatumia Sheria ya Mwaka 1982 ambayo haipo. Kwa ujumla, Sheria na Kanuni kuhusiana na wanyamapori hazijaeleweka miongoni mwa watumiaji.

(c) Uelewa wa wadau wa tasnia ya wanyamapori juu ya sheria na kanuni za biashara ya wanyamapori na nyara si wa kuridhisha kwa wao kuweza kuendesha na kunufaika na biashara hiyo.

(d) Sheria haijaweka wazi vigezo (ukubwa na eneo) vitakavyozingatiwa na kutumika kuidhinisha zizi (*holding ground*) la kuhifadhi wanyama kabla ya kutoa kibali cha ukamataji.

(e) Kanuni nyingi zinazoelekeza namna ya kutekeleza Sheria ya Wanyamapori hazijatungwa, hivyo kasi ya utungaji wa Kanuni hizi iongezeke ili sheria itekelezwe kwa ujumla wake kama ilivyokusudiwa.

(f) Idadi ya watumishi haitoshi kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Wanyamapori. Mfano, usimamizi katika taratibu na viwango vya mazizi ya kuhifadhia wanyama, ukaguzi wa mazizi hayo, kusimamia zoezi la ukamataji na utoaji wa vibali.

(g) Upungufu wa kiutendaji uliobainika kwenye Idara ya Wanyamapori unatokana na kutokuwepo kwa chombo mahususi kinachosimamia tasnia ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya pili iliitaka Kamati kuchunguza utaratibu uliotumika kukamata na kuwasafirisha Twiga wawili kwa Kibali cha Wizara ya Maliasili na Utalii cha Tarehe 29 Aprili, 2011. Matokeo ya uchunguzi ni kwamba:-

(a)J ina la Kampuni lililoandikwa ndani ya barua ni *Jungle International* wakati jina halisi ambalo limeandikwa kwenye leseni ya biashara iliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Kampuni hiyo ni *Jungle International Limited*.

(b) Kibali cha maandishi kilichotolewa kwa Kampuni ya *Jungle Intenational* kuiruhusu kukamata wanyama wakiwemo twiga wawili (*National Game*), kilitolewa katika mfumo wa barua, lakini barua hiyo ilishindwa kuonesha rejea ya barua ya maombi ya kukamata wanyama hao, jambo linaloashiria kuwepo kwa aina fulani ya udanganyifu kama siyo uzembe katika uandishi wa barua husika. Hata hivyo, ili kujiridhisha na jambo hili, Kamati iliomba kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kupatiwa nakala halisi ya barua ya maombi kutoka kwa *Jungle International* ikiomba kibali cha kukamata wanyama hao, barua hiyo haikuwasilishwa mpaka hii leo. (*Makofi*)

(c) Kamati ilibaini kwamba, kibali kilichotolewa kilikuwa ni kwa ajili ya ukamataji wa wanyama kwa matumizi ya *zoo*, lakini hakikuonesha kuwa *zoo* hiyo iko mahali gani (ndani au nje ya nchi). Kwa kufanya hivyo, Kamati iliridhika kuwa jambo hilo lilifanywa kwa makusudi kuficha ukweli wa mahali ambapo wanyama hao wangetakiwa kupelekwa. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kibali husika kilielekeza ukamataji wa wanyama ufanyike katika Wilaya tatu ambazo ni Longido, Simanjiro na Monduli, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 3(4) na (5) ambayo inaelekeza kwamba kibali cha kukamata wanyama ni lazima kiainishe Wilaya moja tu na endapo kutakuwa na ulazima wa kukamata wanyama zaidi ya Wilaya moja basi vitatolewa vibali tofauti kwa kila Wilaya.

(d) Kamati ilibaini kwamba kutokana na kipengele (e) cha kibali alichopewa *Jungle International* ilionekana kwamba alitakiwa kuwasilisha *airway bills* na *custom stamp*, lakini kwa mujibu wa taratibu, nyaraka hizi ni uthibitisho kuwa wanyama hao wangesafirishwa nje ya nchi.

Mkanganyiko wa sehemu ambayo wanyama hao wangepelekwa unaendelea kuthibitishwa kutokana na ukweli kwamba barua ya *Jungle International* kwenda Wizarani ilikuwa wazi kuwa wanyama hao walikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya shamba la wanyama (*zoo), Savannah Plain International School* lililoko Shinyanga kinyume na barua ya idhini iliyotoka

Wizarani ikionesha kuwa wanyama hao walikuwa wanasafirishwa nje ya nchi.

(e) Kamati ilibaini kuwa idhini ya kuwakamata Wanyama wa Taifa (*National Game*) wakiwemo twiga, inatakiwa kutolewa kwa Kibali Maalum (*Special Permit*) na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, kinyume kabisa na ilivyoonekana katika kibali hiki ambacho kilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na kusainiwa na Ndugu M. Madehele, Afisa Wanyamapori Mkuu. Jambo hili ni kinyume na Kifungu cha 26(1) na 58(1).

(f) Kamati ilibaini kuwa Kampuni ya *Jungle International* siyo kampuni halali kuendesha biashara ya wanyamapori kwani taarifa za Msajili wa Makampuni (*BRELA*) zimethibitisha kuwa Kampuni ya *Jungle International* tangu tarehe 28 Desemba, 2001 ilibadili jina na shughuli zake, kwa sasa kampuni hiyo imesajiliwa kwa jina la *Jungle Auctioneers & Brokers Company* ambayo inafanya shughuli za udalali. Kwa msingi huu, Wizara kupitia barua Kumb. Na.GD/T.80/85/98 ya tarehe 29 Aprili, 2011 iliyosainiwa na Ndugu M. Madehele, Afisa Wanyamaporo Mkuu, kwa niaba ya Katibu Mkuu, ilitoa kibali kwa Kampuni ambayo haipo. (*Makofi*)

(g) Kamati haikuweza kupata ushahidi wa aina yoyote wa kuuzwa, kukamatwa na kusafirishwa kwa wanyama waliopo kwenye kibali cha Wizara kilichosainiwa na Ndugu M. Madehele. Pia Kamati imejiridhisha kwamba utaratibu uliotumika kutoa kibali cha kukamata wanyama haukuwa wa kawaida. Kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni za Ukamataji Wanyama za Mwaka 2010, inaelekezwa kuwa mwenye mamlaka ya kutoa kibali cha kukamata wanyama ni Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori pekee. (*Makofi*)

(h) Pamoja na kwamba Kamati haikubaini uuzwaji, ukamataji na usafirishaji wa wanyama waliokuwa wakichunguzwa, upo uwezekano kwamba wanyama hao walikamatwa na kusafirishwa nje ya nchi ikirejewa matukio mbalimbali ambapo wanyama wamekuwa wakikamatwa na kusafirishwa nje ya nchi kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, katika hatua zote tano za uchunguzi, Kamati haikuthibitisha kuwa twiga hao wawili waliuzwa, walikamatwa na kusafirishwa. Hata hivyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

(a) Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 na Kanuni zake zinampa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ambayo

yanakasimiwa kwake binafsi kama Mkurugenzi na yanalindwa kisheria, hivyo ni vyema yakazingatiwa.

(b) Kutokuwepo kwa Kanuni zinazoelekeza mambo mahususi katika tasnia ya wanyamapori kunaleta mianya ya uvunjifu wa Sheria. Kwa mfano, kutokuwepo kwa Kanuni za Kusimamia Matumizi ya Wanyama wa Taifa (*National Game*) kama vile twiga kunachangia mianya ya ujangiri na biashara zingine haramu dhidi ya wanyama hao.

(c) Katika taratibu zote zinazohusisha utoaji wa vibali na leseni hakuna uchunguzi wa kutosha unaokuwa umefanyika kubaini uhalali wa anayepewa leseni, aina ya leseni na matumizi ya leseni husika. Mfano ni Kampuni ya *Jungle International* kubadili jina tangu mwaka 2001, lakini hadi Desemba, 2011 imeendelea kushiriki shughuli mbalimbali za Wizara kwa jina lisilokuwepo.

(d) Utaratibu wa uandishi wa barua usiorejea maombi ya vibali vya kukamata wanyama unachangia ugumu katika utunzaji na ufuatiliaji wa kumbukumbu za maombi na vibali husika.

(e) Utoaji wa vibali bila mhusika kuomba kwa maandishi ni kinyume cha Sheria na inaashiria kuwa kulikuwa na mazungumzo kabla ya kutolewa kibali hicho.

(f) Kama siyo uzembe katika utekelezaji wa majukumu ya kiofisi, kibali kilichotolewa kwa *Jungle Internationa*l kukamata wanyama kiliandaliwa makusudi kwa lengo la kutoa mianya ambayo itasababisha rasilimali za Taifa kutumika kwa njia isiyofaa.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya tatu iliitaka Kamati ya Uchunguzi kuchunguza ushiriki wa Watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika biashara ya wanyamapori hai. Dhamira ya kuwepo kwa hadidu hii ya rejea ilikuwa ni kujiridhisha na namna mpangilio wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara unavyoathiri biashara ya wanyamapori hai. Pili, hadidu hii ilikusudia kuchunguza na kubaini kama kuna Watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii wanaomiliki Kampuni za Uwindaji wa Kitalii hivyo kusababisha mgongano wa kimaslahi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiutumishi.

Ushahidi wa nyaraka mbalimbali kutoka kwa Wakala wa Usajili wa Makampuni hauoneshi kuwepo kwa makampuni ya uwindaji wa kitalii ambayo wamiliki/wanahisa wake wana majina yanayofanana na majina ya Watumishi wa Wizara. Pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, alisita kutamka kwamba wapo watumishi wenye kumiliki makampuni ya

aina hii. Hivyo, zipo hisia ambazo ni vigumu kuzihakiki juu ya Watumishi wa Wizara kumiliki makampuni ya uwindaji wa kitalii.

Maoni ya Kamati kuhusu hadidu ya rejea ya tatu ni yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati haukuweza kuthibitisha kuwepo kwa Makampuni ya Biashara ya Wanyamapori hai yanayomilikiwa na Watumishi wa Wizara, hususan Watumishi wa Idara ya Wanyamapori. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa *quota* za baadhi ya wafanyabiashara zimekuwa zikibaki Wizarani katika Idara ya Wanyamapori kinyume na utaratibu, kama ilivyothibitishwa na Kampuni za *Ham Marketing* na *Jungle International Ltd.* Kitendo hiki kinatoa mwanya kwa Watumishi wa Idara kuwaruhusu wafanyabiashara wengine ambao hawakupewa *quota* hapo awali (kwa mujibu wa sheria), kutumia *quota* hizo kinyume na utaratibu, hali ambayo inaashiria kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa Watumishi wa Idara ya Wanyamapori kunufaika kimaslahi na utaratibu huo mbovu.

(b) Kitendo cha kuwapa wafanyabiashara vibali vya ukamataji wakati hawakuomba kinadhihirisha kwamba baadhi ya Watumishi wa Idara ya Wanyamapori wanajihusisha na biashara hii kinyume na sheria na misingi ya utawala bora. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati ya Uchunguzi kuwa, matokeo ya uchunguzi huu hayapaswi kuzuia uchunguzi wa vyombo vingine vya dola kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa watumishi wa namna hii katika Idara hii na zingine kwa sasa au baadaye.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya nne ilitaka Kamati kuchunguza utaratibu uliotumika kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa msimu wa uwindaji wa mwaka 2013 - 2018.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kwa ujumla utaratibu uliotumika ni wa kawaida kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori ya 2009 na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za 2010. Hata hivyo, palikuwepo na dosari kadhaa ambazo yawezekana ndizo zilizokuwa chanzo cha manung'uniko miongoni mwa wadau kuhusu uhalali wa zoezi zima. Kwa mfano:-

(i) Baadhi ya Makampuni kama vile Mwanauta, Saidi Kawawa na Malagarasi, yalipewa vitalu tena vya Daraja la Kwanza na la Pili wakati Kamati ya Kumshauri Waziri kuhusu ugawaji wa vitalu ilimshauri asizipatie Kampuni hizo vitalu kwa sababu hazina vigezo.

(ii) Tangazo la Wizara la Tarehe 7 Septemba, 2011 kuhusu mgao wa vitalu kwa Kampuni sitini zilizopata halikuonesha vitalu ambavyo

Kampuni hizo zilipatiwa. Kwa msingi huu, Kifungu cha 11 cha Sheria ya Wanyamapori, 2009 kwamba; *"The Minister shall ensure that any modality or system used in allocation of hunting blocks is transparent and is inline with the principles of good governance"* hakikuzingatiwa kwa sababu taarifa hiyo haikuweka wazi ni mwombaji gani amepata kitalu gani. Hivyo, kitendo hicho kiliwaweka gizani waombaji kujiandaa kwa ajili ya kuchukua hatua za malalamiko kwa Waziri mwenye dhamana. *(Makofi)*

(iii) Maombi yote ya wafanyabiashara walioomba kupewa vitalu vya uwindaji wa kitalii yalipokelewa na Idara ya Wanyamapori na kufunguliwa bila kuwahusisha waombaji kinyume na inavyotakiwa katika mfumo wa maombi ya shughuli mbalimbali zenye ushindani.

Yafuatayo ni maoni ya Kamati katika hadidu ya rejea ya nne:-

(a) Dhana ya utawala bora bado haijatekelezwa ipasavyo ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii hasa kwa kuendelea kuwa mgawaji wa maeneo ya vitalu vya uwindaji wa kitalii badala ya kuwa na mamlaka nyingine itakayokuwa inatekeleza jambo hilo kisheria ili Wizara ibaki kuwa msimamizi wa utekelezaji wa sera na hivyo kupunguza malalamiko ya wananchi katika jambo hili (*overseer function*).

(b) Katika jambo hili maoni ya Kamati kuwa vitalu vya uwindaji vitangazwe kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma kama ilivyorekebishwa Mwaka 2011 kwa kuhakikisha uwazi unakuwepo katika mchakato mzima wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

(c) Kamati ina maoni kuwa suala la uadilifu wa Watumishi ndani ya Wizara hii ni jambo la kuangaliwa upya ili kurudisha imani kwa wadau mbalimbali wa tasnia hii.

(d) Kuna viashiria kuwa, Idara ya Wanyamaori kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)*, haijafanya utafiti wa kutosha ili kuchagua, kuandaa na kutenga maeneo ya uwindaji wa kitalii (*hunting blocks*), kwa kuzingatia hali halisi ya maeneo husika ili kuhakikisha maeneo yanayopendekezwa kuwa vitalu vya uwindaji wa kitalii yanakidhi vigezo na yanapata wawekezaji sahihi ambao wataweza kulipa ada kwa wakati. Ndiyo maana baadhi ya maeneo yaliyo chini ya hatimiliki ya iliyokuwa Kampuni ya Taifa ya Uwindaji *(TAWICO)*, yakaingizwa kwenye mgao wa vitalu kinyume na matakwa ya kisheria.

(e) Eneo la Wilaya ya Simanjiro kwa maana ya maeneo tengefu na maeneo ya wazi yenye wanyamapori, sehemu kubwa ya maeneo hayo yamegawanywa kama vitalu vya uwindaji wa kitalii. Maoni ya

Kamati kuhusu maeneo haya yaliyogawanywa kwa Kampuni za Uwindaji wa Kitalii ni vizuri yaangaliwe upya.

Mpango wa matumizi wa eneo hilo (*General Management Plan - GMP*), uandaliwe upya kutoa matumizi yanayofaa na kwa usawa kwa wenyeji na vitalu vya uwindaji. Jambo hili likifanyika vyema litasaidia kupunguza mivutano ya mara kwa mara baina ya wawekezaji wa biashara ya vitalu na wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya tano iliitaka Kamati kuchunguza mambo mengine yaliyoisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kuhusiana na biashara ya wanyamapori hai/nyara na ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

Jambo lililobainika kuhusiana na masuala yaliyokuwa yakichunguzwa lilikuwa ni ukamataji na usafirishaji wa tembo wanne kwenda nchini Pakistani mwaka 2009. Matokeo ya uchunguzi wa Kamati katika suala hili ilikuwa ni kwamba, mchakato wa kuwasafirisha tembo hao wanne kwenda katika *Zoo* ya Karachi nchini Pakistani ulikuwa tata na tija yake kwa Taifa haijabainika.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusu hadidu ya rejea ya tano ni:-

Ni maoni ya Kamati kuwa, mchakato kwa ajili ya kutoa msaada kwa tembo hao wanne kwa Serikali ya Karachi ulianzishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii bila maombi ya Serikali ya Karachi. Maoni haya yanathibitishwa na kukosekana kwa vielelezo vya kimaandishi vinavyoonesha maombi ya Serikali ya Jiji la Karachi kupatiwa msaada huo. Hapa Bibi Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii alisema:-

"…lazima kuwe na mawasiliano, kwamba lazima wale waliomba. Wanaomba kwetu kwa maana hiyo *District* ya Karachi lazima waliomba kwenye Wizara na Wizara lazima iliwaandikia, kwanza, kuwakubalia na kama walihitaji idadi gani, wakaambiwa tunaweza kuwapa tu idadi hii…"

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuweza kupatiwa uthibitisho kuwa Serikali ya Karachi iliomba kwa Serikali ya Tanzania wanyama hao. Aidha, hapakuoneshwa pia ushahidi wa Serikali ya Jiji la Karachi kukiri kuwapokea tembo hao wanne.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa uthibitisho wa maandishi wa Ndugu Kamran Ahmed kuwa Mwakilishi wa Serikali ya Jiji la Karachi hapa

nchini ni maoni ya Kamati kwamba makubaliano yaliyoingiwa kati ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na aliyeonekana kuwa ni Mwakilishi wa Serikali ya Jiji la Karachi bila uthibitisho wowote wa kimaandishi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala kutumika kwa mihuri ya mamlaka za pande zote mbili ni ya kiulaghai. Ilikuwa ni vigumu kwa Kamati kujiridhisha kwamba Ndugu Kamran Ahmed aliteuliwa na Serikali ya Jiji la Karachi kuwa mwakilishi wake.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati ulikwenda mbali zaidi kwa kubaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii mnamo tarehe 19 Julai, 2010 ilitoa kibali kilichosainiwa na Ndugu B. M. C. M. Midala kwa niaba ya Katibu Mkuu kwa Serikali ya Jiji la Karachi kuruhusu usafirishwaji wa twiga wawili, viboko wawili, greater kudu wawili na errands wanne kwa Kibali cha Ukamataji Namba GD/R.20/2/87 cha tarehe 27 Januari, 2010.

Mheshimiwa Spika, kilichoishtua Kamati katika jambo hili ni kwamba, Idara iliendelea kuwa na ujasiri wa kupeleka wanyama zaidi huko Karachi wakati haijapata uthibitisho (*acknowledgement*) kwamba wale wanyama wa awali (tembo majike wanne) walishapokelewa na Serikali ya Jiji hilo. Kitendo hicho kinatoa mwanya wa fikra kwamba yawezekana Idara ya Wanyamapori ilihusika katika biashara isiyokuwa na maslahi kwa Taifa. Ni vyema basi Serikali ikalihakikishia Bunge lako Tukufu namna mchakato huo ulivyofanyika ikiwa ni pamoja na tija yake kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo (Hoja) ya Kamati; baada ya kueleza masuala yaliyojitokeza na maoni ya Kamati katika kila Hadidu ya Rejea, ninaomba kuwasilisha mapendekezo kumi na moja ya Kamati lakini nitasoma machache katika utaratibu wa Hoja iliyokamili ili kila pendekezo lijadiliwe/liafikiwe na kupata uamuzi wa Bunge kwa ajili ya utekelezaji bora wa Serikali. (*Makofi*)

Kwa kuwa uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa ni matakwa ya kisheria kwa Waziri kutunga Kanuni kumi na sita zinazohusiana na utekelezaji wa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009; na mpaka sasa zimetungwa Kanuni tano tu kati ya hizo 16;

Na kwa kuwa kutokamilisha Kanuni hizo kunafanywa kwa makusudi hivyo kuathiri utendaji wa Serikali na kutengeneza mianya ya rushwa na kuikosesha Serikali mapato;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liiagize Serikali kutunga Kanuni hizo ndani ya miezi sita kuanzia sasa.

Kwa kuwa kibali kilichoandikwa na Ndugu M. Madehele kwa niaba ya Katibu Mkuu kilikuwa na makosa ya kudhamiria;

Na kwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hana mamlaka ya kutoa vibali hivyo vya namna hiyo kisheria (Kifungu Na. 26(1) cha Sheria Na. 5 ya Mwaka 2009);

Na kwa kuwa dhamira hiyo iliruhusu wanyama kusafirishwa nje ya nchi kwa kuitaka Kampuni iliyopewa kibali hicho (*Jungle International*) kuwasilisha *airway bills* na *custom stamps* baada ya kusafirisha wanyama hao;

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liiagize Serikali kuwachukulia hatua kali za kinidhamu aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara kwa kipindi hicho (Ndugu Ladislaus Komba), Ndugu M. Madehele na wale wote waliohusika na utoaji wa kibali hicho. *(Makofi)*

Kwa kuwa uchunguzi wa Kamati ulibaini kuwa kibali alichopewa *Jungle International* kilielekeza ukamataji wa wanyama kufanyika katika Wilaya tatu ambazo ni Longido, Simanjiro na Monduli, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni kwani kibali cha kukamata wanyama ni lazima kiainishe Wilaya moja tu na endapo kutakuwa na ulazima wa kukamata katika zaidi ya Wilaya moja basi vitolewe vibali tofauti kwa kila Wilaya;

Na kwa kuwa vibali vya namna hii vinachochea udanganyifu kwa mfanyabiashara kuweza kuwinda wanyama hao hao katika sehemu zote na kujipatia wanyama wengi zaidi ya aliopewa; na kwamba vibali vingi vilivyotolewa na Idara ya Wanyamapori vimeandikwa kwa mtindo huo;

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kukomesha udanganyifu wa aina hiyo na wote wanaohusika kutoa vibali vya namna hiyo wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Kwa kuwa, Wizara ilitoa kibali cha kukamata wanyama kwa Kampuni ya *Jungle International* wakati kwa mujibu wa taarifa za Msajili wa Makampuni *(BRELA),* Kampuni hiyo haipo kihalali na wala haikupeleka maombi ya kupewa wanyama hao;

Na kwa kuwa hali hiyo inadhihirisha udanganyifu wa kutisha, harufu ya rushwa na uhujumu uchumi wa nchi;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kutoa maelezo ya kina ni kwa nini kibali kilitolewa kwa Kampuni isiyo halali

na kuipatia wanyama ambao haikuomba na wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Kwa kuwa uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa Ndugu Kamran Ahmed ni Raia wa Pakistani, ambaye mnamo mwaka 2009 alijitambulisha kwenye Idara ya Wanyamapori kama Mwakilishi wa Serikali ya Jiji la Karachi na akaingia Mkataba (Memorandum of Understanding) na aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Ndugu Erasmus Tarimo, kwa niaba ya Serikali na kuwezesha tembo wanne kusafirishwa nje ya nchi kinyume cha Sheria;

Na kwa kuwa Ndugu Kamran kwa ushahidi uliopo katika Kikosi dhidi ya Ujangili, Arusha aliwahi kuwa na kesi nyingi za kujihusisha na ukamataji na usafirishaji wa wanyamapori hai kinyume na Sheria;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori (2009) hairuhusiwi kutoa ama kumiliki kadi ya ukamataji wanyamapori (*trappers card*) kwa raia wa kigeni lakini yeye anayo Kadi Namba 0016929;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Wanyamapori Ndugu Erasmus Tarimo na Ndugu Kamran Ahmed anayemiliki kibali hicho na watumishi wengine waliohusika katika sakata hilo.

Kwa kuwa uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba katika mchakato wa ugawaji wa vitalu kulikuwa na dosari nyingi kama vile:-

(a) Kamati ya Ushauri ilipelekewa maombi yaliyofunguliwa na kuchambuliwa na Sekretarieti badala ya kufunguliwa na kuchambuliwa na Kamati yenyewe.

(b) Waziri kutangaza majina ya waliopata vitalu bila kuonesha ni vitalu vipi wamepewa.

(c) Baadhi ya Makampuni kugawiwa vitalu kinyume na ushauri wa Kamati ya Kumshauri Waziri kulingana na sifa na vigezo kama ifuatavyo:-

(i) Makampuni matatu *(Mwanauta and Company Ltd, Said Kawawa Hunting Safaris Ltd* na *Malagarasi Hunting Safaris Ltd),* kugawiwa vitalu kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Ushauri iliyoshauri kuwa Makampuni hayo hayakuwa na sifa.

(ii) Makampuni kumi na sita (*Mkwawa Hunting Safaris (T) Limited, Fereck Safaris Limited, EBN Hunting Safaris Limited, Wild Foot Prints Limited, Malagarasi Hunting Safari Limited, Auto Africa Safaris Limited, HSK Safari Company Limited, Green Leef Limited, African Trophy Hunting Limited, African Buffalos Safari Truckers Limited, FOA Adventure Safaris Limited, Mbogo Hunting Safaris Ltd, Robin Hurt Safaris Ltd, Michaelle Maenthiakis Safaris Ltd, Melami Hunting Safaris Ltd* na *Safari Club Ltd* kugawiwa vitalu ambavyo hayakuomba tena vingi vikiwa vya daraja la kwanza na la pili wakati kulikuwa na kampuni za kizalendo zilizokuwa na vigezo na zilipendekezwa na Kamati ya Kumshauri Waziri kwamba zipate vitalu.

Na kwa kuwa dosari hizo ziliathiri dhana ya uwazi na misingi ya utawala bora na kuashiria kuwepo kwa rushwa katika zoezi hilo na hivyo kusababisha malalamiko makubwa kutoka kwa waombaji;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kumwajibisha Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), kwa kutengeneza mazingira ya rushwa ikiwa ni pamoja na kuyanyang'anya makampuni kumi na tisa vitalu yalivyogawiwa.

Kwa kuwa yawezekana upo udhaifu katika Sheria ya Wanyamapori unaotumiwa na wafanyabiashara wakubwa kumiliki makampuni zaidi ya moja hivyo kujipatia vitalu vingi zaidi ya matakwa ya kisheria;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liishauri Serikali kuchunguza na kuziba mianya hii kisheria ili kuwadhibiti wafanyabiashara wenye mitaji mikubwa kufanya ujanja wa kuanzisha makampuni mbalimbali na kujitokeza kama wanahisa tu.

Kwa kuwa Kamati ilibaini kuwa mnamo tarehe 23 Machi, 2009 Idara ya Wanyamapori ilimwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Karachi barua yenye Kumb. Na. GD./R.40/20/Vol.II/8 kumwarifu kuwa maombi yake ya kukamata tembo majike wanne yamekubaliwa, lakini katika uchunguzi wa Kamati hapakuwa na uthibitisho wa kimaandishi kuwa Serikali ya Jiji la Karachi iliomba tembo hao. Aidha**,** hakuna ushahidi kuwa Serikali ya Jiji la Karachi ilipokea tembo hao;

Na kwa kuwa hali hii inaashiria kwamba kulikuwa na udanganyifu katika zoezi zima;

Kwa hiyo basi Bunge linaombwa liridhie wale wote walioshiriki katika suala hilo wachukuliwe hatua za kinidhamu na fedha za Serikali zilizotumika katika mchakato huo zirejeshwe.

Kwa kuwa udanganyifu wa kupeleka wanyama kwa Serikali ya Jiji la Karachi uliendelea ambapo Ndugu B.M.C.M. Midala kwa niaba ya Katibu Mkuu alitoa kibali cha kuruhusu ukamataji na usafirishaji wa twiga wawili, viboko wawili, *greater kudu* wawili na elands wanne kwenda Serikali ya Jiji la Karachi;

Na kwa kuwa hali hiyo ni ishara tosha kwamba Idara ya Wanyamapori inajishughulisha na utoaji wa vibali vya ukamataji na usafirishaji wa wanyamapori hai kinyume na utaratibu kwani hapaoneshi kwamba Jiji la Karachi liliomba kupelekewa wanyama hao;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Ladislaus Komba, Ndugu B. M. C. M. Midala, Ndugu M. Madehele na wale wote walioshiriki katika suala hilo.

Kwa kuwa uchunguzi wa Kamati ulibaini kuwepo kwa upungufu mkubwa wa watumishi katika Idara ya Wanyamapori hususan Askari wa Kikosi cha Kuzuia Ujangili;

Na kwa kuwa upungufu huo siyo tu kwamba unaathiri udhibiti wa ujangili, lakini pia unachochea vitendo vya rushwa kwa maaskari wachache waliopo;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liishauri Serikali mambo yafuatayo:  Katika hali ya dharura vyombo vingine vya dola kama vile jeshi vitumike kufanya doria za kuzuia ujangili; na iajiri watumishi na vitendea kazi zaidi wenye sifa kwa ajili ya kupunguza ujangili na kudhibiti vitendo vya rushwa.

Kwa kuwa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii yanaonekana kuwa mengi na yenye kuhitaji ufanisi kuliko ilivyo sasa;

Na kwa kuwa kukosekana kwa ufanisi huo kunachangia kuibuka kwa malalamiko mbalimbali ya wadau hasa katika tasnia ya wanyamapori na uwindaji wa kitalii;

Kwa hiyo basi Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuunda Mamlaka Maalumu (ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuanzia sasa), kwa ajili kushughulikia masuala ya biashara ya wanyamapori na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, taarifa nzima ya uchunguzi imeambatishwa katika taarifa hii (Kiambatisho A) na naomba iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizofanywa na Kamati katika kipindi cha Mwaka 2011/2012; kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba niwasilishe mambo ambayo Kamati ingependa kuona utekelezaji wake unafanyika kikamilifu hasa kwa kipindi hiki cha mwaka 2012/2013, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na uchimbaji wa urani nchini, Kamati inapendekeza kufanyika kwa tathmini ya kina kuhusu athari za kimazingira na kiuhifadhi zinazoweza kutokea kutokana na uchimbaji wa madini hayo katika Hifadhi za Pori la Akiba la Selous. Aidha, uchimbaji ukianza basi ufanyike kwa uangalifu ili kutunza hazina ya maliasili iliyopo kwenye Pori hilo, wakati huo huo nchi ikivuna madini ya urani yaliyopo; na vilevile Serikali ihakikishe Mkataba wa kuchimba urani katika eneo hilo unafanyika kwa uwazi na uzingatie maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kuwa Sera ya Misitu haijaweka wazi kiasi cha asilimia ya mapato kinachotakiwa kutolewa kwa wanavijiji wanaozunguka maeneo ya misitu ili kuhamasisha wanavijiji kuendelea na uhifadhi endelevu ni vyema sera ikafanyiwa marekebisho ili kuaainisha wazi kiasi cha asilimia inayotakiwa kutolewa kwa shughuli za ujirani mwema kama ilivyo kwa wanyamapori. Aidha, suala hili la wananchi kufaidika na uwepo wa misitu katika maeneo yao, liwekewe misingi ya kisheria ili manufaa hayo yajulikane na utaratibu wa kuyapata uwe wa moja kwa moja ili iwe chachu ya maendeleo ya wananchi wanaoishi kuzunguka mashamba ya misitu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa ugawaji wa vibali vya kuvuna msitu vinatolewa kwa wenye viwanda tu, Kamati inashauri Kamati za ugawaji zitumie vigezo vilivyo ndani ya uwezo wa wananchi wanaoishi kuzunguka Mashamba ya Miti ya Serikali ili manufaa ya uwepo wa misitu hii yawafikie wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chuo cha Taifa cha Utalii kimejengwa kwa gharama kubwa na chenye vifaa vya kisasa na kinategemewa kuwa Chuo Kikubwa Afrika Mashariki, sasa ni wakati mwafaka kwa Wizara kuajiri watendaji wenye sifa ambao watapelekea kutoa wataalam bora wa masuala ya hoteli na utalii na hivyo kufanya Watanzania kuwa vinara kwenye soko la ajira katika Afrika Mashariki.

Aidha, ili kukabiliana na tatizo la ada kubwa ni vyema Wizara ikawasiliana na Bodi ya Mikopo ili kuona uwezekano wa Bodi hiyo kutoa mikopo pia kwa wanafunzi wa chuo hiki. Hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira na kuajiri watumishi wengi kwenye sekta ya hoteli kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, suala la uhifadhi wa maliasili ni la muhimu sana katika nchi yetu na dunia kwa ujumla. Kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka na hata katika baadhi ya maeneo ya hifadhi kuvamiwa na shughuli za binadamu, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi. Aidha, kwa kuwa tatizo la uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya hifadhi ni la muda mrefu, ni vyema Wizara ikaendesha zoezi la kuhakiki upya mipaka ya hifadhi kwa kushirikisha wananchi wanaozunguka maeneo hayo na ikiwa kuna fidia inayotakiwa kutolewa kwa wananchi, fidia hiyo iendane na hali halisi ya maisha na ikiwa wananchi wataombwa kupisha eneo la hifadhi, ni jukumu la Serikali kutafuta eneo watakalohamia wananchi hao.

Hata hivyo, Kamati inaiagiza Serikali izijengee uwezo Halmashauri za Wilaya na Taasisi zake ili ziweze kuhakikisha kwamba wananchi hawavamii maeneo ya hifadhi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ni wakati sasa kwa Serikali kuiagiza Kampuni ya *Africa Barrick Gold* na *Anglo Gold Ashanti* kutekeleza maagizo yote yanayohusu athari za mazingira katika Migodi ya North Mara, Buzwagi na Geita. Aidha, migodi itekeleze ahadi zote ilizotoa kuhusu miradi ya maendeleo kwa jamii inayozunguka migodi na pia ijenge mazingira mazuri ya ujirani mwema na vijiji husika ili kuondoa migogoro ambayo imekuwa kikwazo cha maendeleo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Tume ya Taifa ya *UNESCO* kwa kuonesha juhudi katika kuingiza Njia ya Kati ya Biashara ya Watumwa na Vipusa katika Urithi wa Dunia kutokana na historia ya kipekee siyo tu katika nchi yetu bali katika Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla. Kamati inaendelea kuishauri Tume ifanye haraka na kwa wakati uliopangwa, marekebisho yanayohitajika ya Kabrasha *(Dosier)* ambayo iliwasilishwa awali *UNESCO* kuomba njia hiyo kuwekwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia ili iwasilishwe kabla ya tarehe 1 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upungufu wa magari na vitendea kazi katika Chuo cha Wanyamapori Pasiansi, Kamati inashauri Idara ya Wanyamapori ipunguze mrundikano wa magari Wizarani kwa kuyapeleka vituoni kusaidia doria ili kuokoa wanyama wanaouwawa kila

siku na hivyo kupoteza rasilimali ya Taifa. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya suala zima la kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa askari wa wanyamapori ili kuweza kukabiliana na ujangili unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia Sekta ya Wanyamapori kikamilifu, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Mamlaka ya Wanyamapori inaanzishwa mara moja kwani imechelewa sana baada ya Sheria kupitishwa Mwaka 2009 *(Wildlife Conservation Act, 2009).*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua utaratibu mzuri wa Serikali wa kutoa fedha kwa ajili ya kupimia viwanja katika Halmashauri zetu nchini. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa sana na baadhi ya Halmashauri kutoonesha juhudi katika kurejesha fedha hizo katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kufanya Kamati iamini kuwa fedha hizi hazitumiki kwa ajili ya kupima viwanja. Kamati inaagiza Wizara iwe makini na ijiwekee utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa kwa Halmashauri zinatumika kwa matumizi yaliyopangwa na Wizara izipangie Halmashauri muda wa kurudisha fedha hizo, yaani *timeframe* na Halmashauri zitozwe riba endapo zitachelewa kurudisha malipo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada zinazoonekana za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia Miradi ya Majaribio ya MKUHUMI. Hata hivyo, Kamati inashauri Miradi hii ilenge tatizo halisi linalosababisha mabadiliko ya tabianchi kama vile jinsi gani ya kupunguza ongezeko la watu; kupunguza uhamaji wa mara kwa mara wa watu hasa makundi ya jamii za wafugaji; na kuweka mipango madhubuti ya kukabiliana na tatizo kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa ieleweke kwamba uchunguzi huo hauhusiani kabisa na masuala ya wanyamapori hai waliotoroshwa ambao kesi yao ipo mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake katika mwaka 2011/2012, yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Wadau wetu wote; napenda kuwashukuru wote kwa ujumla. (*Makofi*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani nyingi kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwenye Ofisi yako Mheshimiwa Spika. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah na

Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Grace Bidya, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2011/ 2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba nitoe Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia mwezi Mei, 2011 hadi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, mawasilisho yangu yatakuwa katika sehemu mbili; sehemu moja ni shughuli za kawaida kama tunavyoelekezwa na Kanuni zetu za kudumu za Bunge; na mawasilisho ya pili ilikuwa ni Kamati Ndogo tuliyoiteua ili kuzamia katika mgogoro wa ardhi uliopo katika Mkoa wa Kagera unaohusiana na ubinafsishaji wa ranchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kazi zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha kuanzia Mei, 2011 hadi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ina majukumu ya kushughulikia masuala ya utendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane iliyo chini ya Kanuni ya 115, Kifungu 9 (1), Majukumu ya Kamati ni:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

(iii) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za utendaji kazi wa Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mei, 2011 hadi Aprili, 2012 Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kuchambua Bajeti; Kamati ilijadili utekelezaji wa Mipango ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 kwa Wizara inazozisimamia. Katika kujadili utekelezaji wa mipango ya bajeti hiyo, ilibainika kuwa Wizara zinakabiliwa na changamoto zinazofanana ambazo ni kupata kiasi kidogo cha fedha za Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na Wizara hizo kuchelewa kupata fedha hizo. Aidha, Kamati ilichambua Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kutoa maoni ya kuzingatiwa hasa kuhusiana na ufinyu wa bajeti kwa Wizara zote tatu. Maoni hayo yaliwasilishwa kupitia Taarifa za Kamati zilizowasilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara mbalimbali ili kujionea jinsi Wizara zinavyotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, Kamati ilitembelea maeneo yafuatayo:-

Kituo cha Utafiti wa Kilimo – Maruku, Kagera. Kituo hiki kinajihusisha na utafiti wa magonjwa ya mimea, wadudu waharibifu, teknolojia bora ya uzalishaji wa mazao na matumizi bora ya udongo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maruku ni sehemu pekee duniani yenye hifadhi ya aina zaidi ya mia moja na hamsini za migomba iliyo hai. Kituo pia kinaendesha Chuo cha Kilimo (Chuo cha Kilimo Maruku), ambacho kinafundisha Wataalamu wa Kilimo na Wakulima. Kamati ilitembelea Mashamba Darasa yanayosimamiwa na Kituo hiki ili kuona namna wananchi wanavyonufaika.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii Kamati ilibaini kuwa Kituo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: Uhaba wa Wataalam wa Utafiti; ufinyu wa bajeti na pia fedha zinazotolewa na Wizara kuchelewa kukifikia

Kituo; uhaba wa vyumba vya madarasa kwa upande wa Chuo baada ya vilivyokuwepo kuchukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kutumika kama shule ya sekondari; na uhaba wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na yaliyojiri wakati wa ziara katika Kituo hiki, Kamati inashauri kwamba, Serikali iongeze bajeti ya kituo hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Serikali inashauriwa kukirejeshea Kituo majengo iliyoyachukua ili yaweze kuondoa uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Spika, katika ziara kwenye Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji – Nyida, Kamati ilibaini kuwa kilimo cha umwagiliaji hufanyika wakati wa masika tu kutokana na skimu kutokuwa na bwawa la kuhifadhi maji ambayo yangetumika wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufanisi usioridhisha wa skimu hii, Kamati inashauri juhudi zaidi zielekezwe kwenye ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji ambayo yatawezesha kilimo cha umwagiliaji kifanyike kwa mwaka mzima. Vilevile Serikali itoe ruzuku kwenye umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kupunguza kodi kwenye vifaa vya umwagiliaji ili kuwawezesha wakulima kumudu bei ya vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mradi wa Kilimo cha Miwa ambao unatumia teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*Drip Irrigation*). Mradi unaendeshwa na Kampuni ya *EcoEnergy* na unazalisha mbegu bora za miwa kutoka nchi za Afrika Kusini na Brazil. Mbegu hizo zinaelezwa kuwa na tija katika uzalishaji wa miwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba, Mradi huu unakabiliwa na tatizo la ardhi hasa baada ya sehemu ya eneo lake kuvamiwa na wananchi. Mgogoro huu umeathiri mipango ya uwekezaji kutokana na kufunguliwa kwa shauri mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali iiwezeshe mahakama ili iweze kushughulikia kwa haraka kesi zilizopo mahakamani. Kumalizika kwa mgogoro huu kutatoa fursa, kwa Mwekezaji kuendelea na shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara sehemu mbalimbali zinazohusu Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Sehemu hizo ni pamoja na Maabara Kuu ya Taifa ya Magonjwa ya Mifugo – Temeke.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii Kamati iliona namna ambavyo Maabara inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi wa chombo hiki muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini, Kamati inashauri Serikali kuifanya Maabara hii kuwa taasisi inayojitegemea ili iweze kupata bajeti ya kutosha kufanya tafiti za magonjwa mbalimbali ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Ranchi za Taifa Kagoma, Mabale, Kitengule, Kikulula na Misenyi zilizopo Mkoani Kagera ni kati ya Ranchi kumi zinazomilikiwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO).* Kama ilivyo katika sekta nyingine, Serikali iliamua kubinafsisha baadhi ya maeneo ya Ranchi za Taifa zikiwemo za Mkoani Kagera kwa lengo la kuziwezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa na wa kibiashara tofauti na ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, licha ya azma hiyo nzuri iliyokusudiwa na Serikali, Ranchi hizo zimekumbwa na migogoro baina ya *NARCO,* wawekezaji na wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka Ranchi. Kamati ilibaini kuwa miongoni mwa mambo mengine, migogoro hiyo inasababishwa na mambo yafuatayo:-

- Kuzorota kwa uhusiano baina ya wawekezaji na wananchi kunakosababishwa na kila upande kukiuka kanuni na taratibu ikiwemo kutoheshimu mipaka ya ranchi;

- Miundombinu hafifu katika ranchi ambayo inasababisha kutofikiwa kwa kiwango cha uwekezaji kilichotarajiwa;

- Uwekezaji kutowanufaisha wananchi kwa mujibu wa makubaliano yaliyo katika mikataba ya ubinafsishaji wa Ranchi hizo;

- Uwepo wa wahamiaji haramu kutoka nchi jirani ambao wanaishi katika maeneo ya Ranchi; na

- Tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na wawekezaji kwa baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa migogoro mingi baina ya wawekezaji na wananchi wa maeneo yaliyo jirani na Ranchi imepelekwa Mahakamani, Kamati inashauri Serikali iiwezeshe mahakama ili itekeleze majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kukamilisha kesi za muda mrefu. Aidha, Serikali iimarishe ulinzi wa mipakani na mikakati endelevu ya kudhibiti wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya muda mrefu yaliyokuwa yakitolewa na Wananchi na Wabunge wa maeneo husika,

Kamati iliamua kuunda Kamati Ndogo kwa lengo la kupata ukweli kuhusiana na migogoro iliyopo. Taarifa ya Kamati Ndogo imeambatishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kitengo cha Kudhibiti Usalama na Ubora wa Samaki na Mazao yake katika Chuo cha Uvuvi – Nyegezi Mwanza. Kitengo hiki kinahusisha maabara ya uchunguzi wa vimelea na kemikali.

Mheshimiwa Spika, katika ziara kwenye Chuo hiki Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: Ufinyu wa bajeti; upungufu wa wakufunzi na watumishi wengine; na uhaba wa majengo kwa ajili ya ofisi, madarasa, mabweni, maktaba, maabara, chumba cha kompyuta, karakana na nyumba za Watumishi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri kwamba, Chuo kiongezewe bajeti ili kiweze kuondokana na changamoto hizo na hivyo kutimiza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kuchakata minofu ya samaki vya Tanzania Fish Processors Ltd - Mwanza na Vick Fish – Bukoba, licha ya kuanzishwa kwa lengo la kusaidia uwepo wa soko la samaki la uhakika na pia kutoa ajira kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka viwanda, bado malengo hayo yameshindwa kufikiwa kutokana na changamoto zifuatazo:-

- Viwanda kuzalisha chini ya kiwango kutokana na uhaba wa samaki unaosababishwa na uvuvi haramu na utoroshwaji wa samaki unaofanywa na wavuvi wanaotoka nchi jirani za Kenya na Uganda.

- Viwanda kushindwa kuvisaidia vijiji vya maeneo yayozunguka viwanda kutokana na maeneo hayo kutopimwa na kupewa mpango wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

- Uongozi wa viwanda hivyo uendelee kusaidia wakazi wa maeneo yanayozunguka viwanda (*corporate social responsibility*) ili kuboresha ustawi wa jamii baina ya pande hizo.

- Wananchi wa maeneo yanayozunguka viwanda wahamasishwe kufuga Samaki ili kufidia upungufu wa samaki wa maji baridi unaojitokeza.

- Serikali ihakikishe sheria zilizopo zinatekelezwa ili kudhibiti uvuvi haramu ambao ni tishio kwa samaki na viumbe wengine wanaoishi majini. Aidha, vijiji vyenye shughuli za uvuvi vitunge Sheria Ndogo kwa lengo la kudhibiti vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika Soko la Kimataifa la Samaki – Kirumba, Mwanza na ilikutana na Uongozi wa Wafanyabiashara wa Soko la Mwaloni - Kirumba na kuona mazao mbalimbali yatokanayo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto ambazo zinalikabili Soko hili ni pamoja na ununuzi wa samaki wazima badala ya minofu ambao hufanywa na wageni kutoka nchi jirani, jambo ambalo ni kinyume cha sheria zinazosimamia biashara ya samaki kwa lengo la kusafirishwa kwenda nje ya nchi; upungufu wa samaki ambao kwa sehemu kubwa unachangiwa na uvuvi haramu na matumizi ya nyavu zenye matundu madogo; msongamano wa wafanyabiashara; na uchakavu wa gati pamoja na uhaba wa maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali iweke mikakati ya kudhibiti uvuvi haramu unaofanywa na wageni kutoka nchi jirani na kudhibiti uuzaji wa samaki wazima kwa wageni badala ya minofu ya samaki.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa ziara katika Wilaya za Bukoba na Muleba, Kamati ilibaini kuwa Wananchi wana hamasa kubwa kuhusiana na ufugaji wa samaki. Kutokana na hamasa hiyo, wananchi hao wamepata mafanikio makubwa katika sekta hii ikiwa ni pamoja na kufikia hatua ya kuzalisha vifaranga vya samaki kwa lengo la kuwauzia wafugaji wengine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, wananchi wanaoendesha ufugaji wa samaki katika maeneo haya wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinaathiri ufugaji wanaoufanya. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa elimu ya ufugaji, uhaba wa wataalamu wa uvuvi na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ili kukabili changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali iongeze Wataalamu (Wagani) wa Uvuvi kwenye Wilaya zinazojishughulisha na Uvuvi pamoja na ufugaji wa samaki ili waweze kutoa elimu ya uvuvi na ufugaji wa samaki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Chuo cha Uvuvi cha Mbegani Bagamoyo kilichopo katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoani Pwani, ambacho baadhi ya Miradi yake inafadhiliwa na *MACEMP*. Chuo cha Mbegani kilianzishwa mnamo mwaka 1966 kwa lengo la kutoa elimu na taaluma inayohusiana na teknolojia ya uvuvi. Aidha, Chuo kinafanya tafiti zinazohitajika katika kuongeza tija kwenye shughuli za uvuvi na kutoa mafunzo na ushauri kwa wadau wa Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki ni hazina kubwa kwa Taifa kwani kina ithibati kamili *(full accreditation*) kutoka *NACTE* na kinapokea wanafunzi kutoka nje ya nchi. Mbegani ni chuo pekee kinachotoa mafunzo ya *Fisheries Enforcement (MCS)* kwa Nchi za *SADC* na mafunzo ya udhibiti wa usalama na ubora (*Quality Assurance)* kwa Nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Chuo hiki ni hazina kubwa kutokana na kuzalisha wataalam hapa nchini na nje ya nchi, bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa Watumishi wenye sifa zinazotakiwa; maslahi duni ya Watumishi; uhaba na uchakavu wa vitendea kazi muhimu; na ufinyu wa bajeti ambao unazuia Chuo kupanua udahili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali iongeze bajeti na kuona uwezekano wa kuboresha miundombinu na rasilimali watu ili Chuo kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea *TAFIRI* ambayo ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya terehe 2 Februari, 1980 kwa lengo la kufanya utafiti wa rasilimali za majini ili kuleta maendeleo kwa Sekta ya Uvuvi nchini. Jukumu kuu la *TAFIRI* ni kuainisha, kuendeleza na kuratibu utafiti wa uvuvi na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake, *TAFIRI* imepata mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kukamilisha Mpango Mkakati wa Taasisi unaolenga utekelezaji wa kazi za miaka mitano, kuanza mchakato wa kutengeneza ajenda za utafiti zinazolenga maendeleo katika Sekta ya Uvuvi na kuendelea kutoa takwimu sahihi kuhusu uvuvi wa sangara katika Ziwa Victoria. Aidha, *TAFIRI* kwa kushirikiana na Taasisi za Japani na Afrika ya Kusini, imefanya uchunguzi wa upatikanaji wa samaki aina ya *Silikanti* ambaye anasadikiwa kutoweka duniani miaka 65 milioni iliyopita na kuonekana kwa wingi ghafla nchini na kuwa kivutio kikubwa kwa wanasayansi ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaniko hayo, *TAFIRI* inakabiliwa na changamoto zifuatazo: Ufinyu wa bajeti ikiwa ni pamoja na kuchanganywa kwa vifungu vya mishahara *(PE)* na kile cha matumizi mengine *(OC);* ukosefu wa Ofisi na Maabara kwa Kituo cha Dar es Salaam; ukosefu wa vitendea kazi kwa ujumla ikiwemo meli ya kufanyia utafiti; ukosefu wa sehemu ya kuhifadhi sampuli za utafiti; na uchakavu wa meli za kufanyia utafiti na nyumba za taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti inayotengwa kwa ajili ya Taasisi hii na pia iangalie uwezekano wa kuipa Taasisi fungu dogo (*sub vote*), ambalo litatenganisha mishahara *(PE)* na matumizi mengine *(OC).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea baadhi ya Miradi ya Maji iliyo chini ya Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati walitembelea maeneo yafuatayo ya Mradi wa Majisafi na Majitaka Mwanza Mjini:-

Chanzo cha uzalishaji maji, mashine za kusukumia maji na kituo cha tiba ya maji safi Capri-point, Kituo cha maji safi Kona ya Bwiru ambacho kinasaidia usambazaji wa maji kwenda sehemu zenye miinuko ili kupunguza uhaba wa maji katika Jiji la Mwanza, Kituo kikuu cha maji taka Makongoro kilichopo kando ya Mto Mirongo ambacho hukusanya majitaka na kuyasukuma kwenda kwenye mabwawa kumi na tatu ya kuchujia maji, Kituo cha majitaka Kirumba (Mradi mpya) kinachochangia asilimia 15 ya miundombinu ya mfumo wa majitaka katika Jiji la Mwanza na Mabwawa kumi na tatu ya tiba ya majitaka yaliyopo Butuja-Ilemela, ambayo huchuja na kusafisha majitaka hadi kufikia viwango vilivyowekwa.

Mheshimwa Spika, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka ya Majitaka na Majisafi Jijini Mwanza ambazo ni pamoja na:-

Upotevu wa maji kwa zaidi ya asilimia 35, madeni ya Taasisi za Serikali kutolipwa kwa wakati na hivyo kuilazimu Mamlaka kusitisha huduma ya maji kwa taasisi husika. Mfano wa taasisi hizo ni Jeshi la Polisi. Mwamko mdogo wa wananchi kuhitaji huduma ya majitaka, ukosefu wa Ofisi kwa *MWAWASA,* uhaba wa fedha kwa ajili ya kuboresha na kusambaza maji katika maeneo mapya na gharama kubwa za uendeshaji zinazotokana na Mji wa Mwanza kuwa na maeneo mengi yenye miinuko na miamba. Mfano, mamlaka hutumia zaidi ya shilingi

milioni 180 kwa mwezi kugharimia umeme wa kuendesha mitambo ya kuzalisha na kusukuma maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Hazina ihakikishe madeni ambayo zinadaiwa Taasisi za Serikali yanalipwa hatua kwa hatua ikiwezekana kwa kukata fedha kutoka katika vifungu vya *OC* ambavyo vinatengwa kwa ajili ya taasisi husika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mkoani Mwanza iangalie namna ya kupunguza upotevu wa maji ambao umevuka kiwango cha kati ya asilimia 25 na asilimia 27 kinachokubalika kwa nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama – Shinyanga na kuona maeneo mbalimbali ya Mradi ikiwa ni pamoja na choteo la maji lililopo kwenye ukingo wa Ziwa Victoria. Choteo hilo lipo kwenye Kijiji cha Ihelele kilicho umbali wa Km.3.3 kutoka ulipo mtambo wa kuchuja na kutibu maji.

Maeneo mengine ya Mradi ambayo Kamati ilitembelea ni pamoja na matangi ya kuhamishia tope (*sedimentation tanks*), chujio la maji kuelekea kwenye matangi makubwa, mashine kubwa za kusukumia maji kuelekea tangi kubwa la kuhifadhia maji na mabomba ya kusafirishia maji kwenda kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo kuhusiana na Mradi huu:-

Ukosefu wa vitendea kazi na vipuli kwa ajili ya mitambo, mabadiliko ya mara kwa mara ya kiwango cha umeme unaoingia kwenye kituo cha uzalishaji wa maji ambayo husababisha uharibifu wa vifaa vya umeme, upungufu wa vyombo vya usafiri na nyumba za Watumishi katika eneo la Ihelele, uhaba wa vifaa vya umeme na kutobolewa kwa mabomba katika maeneo ambayo vijiji havijapatiwa maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri yafuatayo kuhusiana na changamoto zilizopo:-

Serikali iharakishe upatikanaji wa maji katika vijiji ambavyo vipo kwenye maeneo ambayo Mradi huu unapita ili kupunguza uharibifu wa miundombinu ya maji unaofanywa na Wananchi wa maeneo hayo. Aidha, *TANESCO* ihakikishe umeme wa uhakika unapatikana kwa ajili ya kusukuma maji katika Mradi huu.

Vilevile Serikali ikamilishe utandazaji wa miundombinu ya mali ili pampu za kusukuma maji ambazo hazijaanza kufanya kazi ziweze kusukuma maji kwa lengo la kuyafikisha katika Miji ya Nzega, Igunga na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Taasisi na Bodi zifuatazo: Bodi ya Korosho Tanzania. Katika kikao hiki, Kamati ilibaini kuwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umeonesha mafanikio makubwa kwa kusaidia kuongeza uzalishaji wa Zao la Korosho nchini. Mfumo huo umewasaidia wakulima kuondokana na tatizo la upatikanaji wa pembejeo za kilimo na pia bei nzuri ya korosho ikilinganishwa na kipindi kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, licha ya mafanikio hayo bado zipo changamoto ambazo zinakabili uzalishaji wa Zao la Korosho nchini ambazo ni pamoja na kufa kwa viwanda vingi vilivyokuwa vinabangua Korosho na hivyo kufanya kiwango kikubwa cha Korosho (asilimia 95) kuuzwa nje kikiwa ghafi na pia utegemezi wa nchi ya India kama soko pekee la Korosho.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi ili kuongeza thamani ya korosho zitakazouzwa nje. Pia, Bodi ya Korosho ihakikishe inapata masoko mengine ya korosho badala ya kutegemea sehemu moja tu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Maziwa Tanzania na Chama cha Wasindika Maziwe *(TAMPA):* Licha ya Tanzania kuwa na idadi kubwa ya Ng'ombe (milioni 21. 3), mchango wake katika Pato la Taifa ni mdogo asilimia 3.8. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka 15 iliyopita usindikaji wa maziwa umeshuka kwa asilimia 85 hii ikichangiwa kwa sehemu kubwa na kufungwa kwa viwanda 13 kati ya 35 vya kusindika maziwa. Kwa sasa kiwango cha maziwa kinachozalishwa nchini kwa siku ni lita milioni 4.5 lakini kiasi kinachosindikwa ni asilimia 2.3 tu.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Sekta hii ni pamoja na uingizaji wa maziwa na bidhaa zake kwa wingi kutoka nje na ukosefu wa umeme wa kuaminika, kodi nyingi zinazotozwa kwa wazalishaji, kukosekana kwa vituo vya ukusanyaji wa maziwa na wananchi kukosa hamasa ya kunywa maziwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha sekta hii kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo:-

Serikali iondoe kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT), (zero rating),* kwenye maziwa yaliyosindikwa na mazao yake. Serikali iangalie namna ya kulinda wazalishaji wa ndani wa maziwa na viwanda vya kusindika maziwa ili kuviwezesha kushindana na bidhaa za maziwa zinazotoka nje, Jamii ihamasishwe kunywa maziwa hasa katika shule, vituo vya ukusanyaji wa maziwa (*milk collection centres*) vijengwe kwa wingi ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa sambamba na kupunguza urasimu kwa wawekezaji wa viwanda vya kusindika maziwa. Taasisi nyingi (16) ambazo zina wajibu wa kutoa maamuzi kabla mwekezaji hajakubaliwa kuanza uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kikao na Bodi ya Pamba, Kamati ilielezwa kuhusiana na kuyumba kwa soko la pamba, jambo ambalo limesababisha kuanzishwa kwa kilimo cha mkataba baina ya mkulima na mnunuzi.

Changamoto nyingine ambazo zinakabili uzalishaji wa Zao la Pamba ni pamoja na upungufu wa wagani, ukosefu wa mfumo mzuri wa usambazji wa pembejeo, uchanganyaji wa kilimo cha pamba na mazao mengine, jambo ambalo linasababisha wadudu na magonjwa ya mazao mengine kuhamia kwenye Zao la Pamba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Bodi kuhakikisha inajikita katika kuhakikisha wakulima wa pamba wanapata pembejeo za kutosha kwa wakati na kwa gharama nafuu, sambamba na upatikanaji wa soko la uhakika kwa Zao la Pamba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ihakikishe inaongeza Wataalamu wa Kilimo (Maafisa Ugani) ili kusaidia wakulima waweze kuendesha kilimo cha kisasa chenye tija.

Wizara ya Kilimo, Kamati ilikutana na Wizara ya Chakula na Ushirika ili kupata maelezo kuhusiana na Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA na hususan upatikanaji wa pembejeo za kilimo za kutosha, kwa gharama nafuu na kwa wakati. Pia Kamati ilitaka maelezo kutoka kwa Serikali kuhusiana na hali ya usalama wa chakula nchini na hasa ahadi ya Serikali kwa wakulima wa mikoa inayozalisha kwa wingi nafaka kwamba itanunua chakula watakachozalisha.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake Serikali ilikiri kutotekeleza ahadi zake kutokana na changamoto zilizo nje ya uwezo wake. Hali hiyo ilisababisha pembejeo za kilimo kuwa chache, kupatikana kwa gharama kubwa na pia kuchelewa kuwafikia wakulima. Sambamba na hilo mazao ya wakulima hayakununuliwa yote na Serikali kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo Kamati inashauri Serikali ihakikishe pembejeo za kilimo zinawafikia wakulima kwa wingi, kwa bei nafuu na kwa wakati. Aidha, ili kuhakikisha usalama wa chakula nchini, Serikali itenge bajeti ya kutosha ambayo itaiwezesha kununua chakula cha wakulima kwa kiwango kikubwa na kukarabati na kuongeza maghala ya hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka kuwavunja moyo wakulima kwa kushindwa kununua mazao yao, Serikali ifanye tathmini mapema kuhusu hali ya usalama wa chakula nchini ili kama kutakuwa na ziada basi wakulima waruhusiwe kuuza chakula nje ya nchi. Sambamba na hilo, Serikali ijikite katika utafiti wa aina za mazao ambayo yatazalishwa kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokea ili kuepusha wakulima kuzalisha bila tija.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2011 – 2012, Kamati ilifikiria na kujadili Muswada wa Sheria ufuatao: Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (*The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011)*. Muswada huu ulipita hatua zake zote katika Bunge na kinachosubiriwa ni ridhaa ya Rais.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati:-

Kamati ilitafakari taarifa zilizowasilishwa mbele yake pamoja na kutembelea maeneo mbalimbali ili kuona shughuli zinazofanyika na inatoa Maoni na Ushauri kama ifuatavyo:-

Serikali ihakikishe viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa vinafanya kazi ili ubanguaji wa korosho ufanyikie nchini badala ya kuuza korosho ghafi nje ya nchi. Hatua hii itasaidia kuongeza thamani ya korosho na hivyo kuongeza kipato cha mkulima na Taifa. Hatua hii pia itaongeza ajira nchini. Aidha, Bodi ya Korosho ifanye jitihada ya kupata soko la uhakika la korosho nje na ndani ya nchi. Kupatikana kwa soko la uhakika hasa la ndani kutasaidia kuondokana na utegemezi wa soko la India pekee. Serikali kupitia Bodi ya Pamba ihakikishe inapata soko la uhakika la pamba ili kuwasaidia wakulima wa zao hili na kuwapa motisha ya kulima kwa bidii zaidi. Serikali itazame utaratibu mpya wa namna ya kusambaza pembejeo kwa wakulima ili ziwafikie kwa muda mwafaka na kwa bei iliyopangwa badala ya hivi ambavyo inafanyika sasa bila tija.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupungua kwa samaki katika maji baridi ni vyema ufugaji wa samaki ukapewa kipaumbele na kuhamasishwa ili kufidia upungufu huo. Kutokana na hali ngumu waliyonayo wavuvi, Kamati inaona ni vyema itungwe sera ya kuwezesha

wavuvi kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kuendeleza Sekta ya Uvuvi.

Uhaba wa Wataalam ni moja ya tatizo katika Sekta hii. Kamati inashauri Wataalamu wa Uvuvi waongezwe ili kufikia idadi itakayokidhi mahitaji. Aidha, motisha mbalimbali zitolewe kwa Watumishi zikiwemo mafunzo na kuboresha maslahi yao na kutokana na umuhimu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(TAFIRI),* Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuhakikisha utafiti unaendelea kufanyika. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania ambayo inaanzishwa ije na mpango ambao utabadilisha hali ya mifugo nchini.

Kutokana na umuhimu wa maji kwa jamii, Serikali haina budi kuhakikisha inatenga bajeti ya kutosha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, fedha hizo zitolewe kwa muda sahihi ili utekelezaji ufanyike kama ulivyopangwa.

Tatizo la maji kwa Jiji la Dar es Salaam bado ni kubwa sana. Serikali iweke mipango madhubuti ili kuhakikisha Mradi wa Kimbiji – Mpera unafanikiwa na ikibidi Serikali itumie fedha zake za ndani badala ya kutegemea fedha za wafadhili kama ilivyofanya kwa Mradi wa Kahama – Shinyanga.

Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi kwa kila Wilaya ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia *(WB)*, hautekelezwi kwa kasi ya kuridhisha; hivyo, Serikali ichangie fedha ili kufanikisha utekelezaji wa Mradi huu. Kwa kuwa maji ni uhai, Serikali iangalie uwezekano wa kuchangia gharama za maji kwa kuondoa kodi kwenye dawa za kusafishia maji ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za umeme kwa mamlaka za maji ili ziweze kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi zaidi. Elimu ya mazingira itolewe kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji.

Serikali iangalie kwa makini biashara ya vyuma chakavu kwani imeonekana tangu biashara hiyo ishamiri ndiyo hujuma za miundombinu ya maji imekuwa ikiongezeka siku hadi siku. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa elimu kwa jamii juu ya athari zitokanazo na hujuma za miundombinu ya maji na ikiwezekana kuwepo na ulinzi shirikishi ili kuweza kuwabaini wale wote wanaojihusisha na hujuma.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara zote tatu ambazo zipo kwenye Sekta ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati inatekeleza majukumu yake. Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri hao ni Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe (Mb) - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza (Mb) - Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, (Mb) - Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro (Mb) - Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya (Mb) - Waziri wa Maji na Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge (Mb) - Naibu Waziri wa Maji. Aidha, natoa shukrani kwa Watendaji wa Wizara zote tatu wakiongozwa na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa ushirikiano wao mzuri waliouonesha kwa kipindi kilichopita. Kamati inatumaini ushirikiano huo utaendelea katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Grace Bidya, kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa kipindi chote na kuratibu kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa uvumilivu, busara na ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa – Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Sylevester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Amer, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Sharif Hiran, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni.

**Taarifa ya Kamati Ndogo ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Mgogoro wa Ardhi ya Narco Kati ya Wawekezaji Kwenye Ranchi za Kagoma, Mabale, Kitengule, Kikulula, Missenyi na Wananchi Waishio Jirani na Ranchi Hizo Katika Mkoa wa Kagera**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali ili Kamati hii kupitia Kamati yake Ndogo, kufanya kazi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba ya Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake kwa niaba ya Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 115, Nyongeza ya Nane, kifungu cha 9 (1) (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyofuatilia na kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya wawekezaji kwenye Ranchi za Kagoma, Mabale na Kitengule, Kikulula na Missenyi na wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la ziara ya Kamati hii kutembelea Ranchi za Kagoma, Mabale na Kitengule limetokana na malalamiko ya muda mrefu yaliyokuwa yakitolewa na wananchi na Wabunge wa maeneo husika kuhusu migogoro ya ardhi iliyosababishwa na ubinafsishaji wa Ranchi za Taifa za Kagoma, Mabale, Kikulula, Kitengule na Missenyi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 28 Oktoba hadi tarehe 3 Novemba, 2011 baadhi ya Wajumbe wa Kamati walitembelea Ranchi ya Kagoma na Vijiji vya Lubare na Lutoro. Pia kati ya tarehe 13 - 18 Februari, 2012 baadhi ya Wajumbe wa Kamati hii walitembelea Ranchi za Missenyi, Mabale, Kikulula na Kitengule.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wafuatao walishiriki katika ziara ya kutembelea Ranchi ya Kagoma na Vijiji vya Lubare na Lutoro:-

Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Suleiman Kakoso, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Ndugu Ramadhan Abdallah - Katibu wa Kamati na Ndugu Sophia Vumbi - Msaidizi wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wafuatao walishiriki katika ziara ya kutembelea Ranchi ya Missenyi, Mabale, Kikulula na Kitengule:-

Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Suleimani Saidi Jafo, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Ndugu Michael Kadebe - Katibu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufasaha, Kamati ilitekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Kupata maelezo ya awali kutoka kwa Wataalam wa Serikali kuhusu Ranchi za Taifa, ubinafsishaji na uwekezaji wa Mashamba ya Ranchi za Taifa, masuala ya uhamiaji na wahamiaji haramu na hali ya usalama wa maeneo husika.

(b) Kupata maelezo kutoka kwa baadhi ya Wabunge wa maeneo hayo.

(c) Kutembelea Mashamba ya Ranchi ya Taifa ya Kagoma, Missenyi, Kikulula, Mabale na Kitengule na kukutana na wananchi wanaoishi ndani ya Ranchi na maeneo yanayozunguka Ranchi hizo na kusikiliza malalamiko yao.

(d) Kupata taarifa kutoka kwa wawekezaji wa Mashamba ya Ranchi za Taifa.

(e) Kufanya majumuisho ya ziara ikihusisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, historia ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (*National Agricultural Company*) ilianza mwaka 1947 na tarehe 14 Oktoba 1975 Kampuni hii ilibadili jina na kuwa *National Ranching Company Limited (NARCO),* ikiwa na majukumu ya kushughulikia ufugaji wa kisasa wa ng'ombe hasa wa nyama kwenye mashamba makubwa ya biashara.

*NARCO* ilikuwa na jumla ya Ranchi 15 katika Mikoa tisa ya Tanzania ambazo kwa pamoja zilikuwa na ukubwa wa hekta 630,000 na uwezo wa kuweka ngombe 180,000.

Mheshmiwa Spika, hadi Februari, 2012 *NARCO* inamiliki Ranchi kumi tu zenye ukubwa wa eneo la hekta 230,384, baada ya uamuzi wa Serikali wa mwaka 2002 kumilikisha kwa wawekezaji binafsi na mengine kugawiwa kwa Wilaya. Aidha, Shirika hili katika kipindi cha mwaka 1992 na 2002 halikufanya shughuli yoyote za uwekezaji kwa kuwa lilikuwa linategemea kuuzwa. Hivyo, kutokana na uamuzi wa Serikali baadhi ya

Ranchi za *NARCO* zilibinafsishwa kwa wananchi ili kuwawezesha kuingia kwenye ufugaji wa kisasa unaoendeshwa kibiashara kama ilivyoelezwa kwenye Waraka Na. 2 wa Baraza la Mawaziri wa Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika Kampuni ya *NARCO* ya sasa, idadi kubwa ya ng'ombe wanaofugwa ni aina ya Boran ambao wana umbile kubwa ukilinganisha na ng'ombe wa kienyeji *(Short Horn Zebu)* na wana sifa ya kukua haraka. Takwimu za uzalishaji katika Ranchi za *NARCO* kwa ujumla ni nzuri, ambapo wastani wa uzalishaji wa ndama ni asilimia 75, wastani wa vifo vyote ni asilimia 1.63 na ndama asilimia 2.58.

*NARCO* ni chanzo muhimu cha mitamba na madume bora kwa wafugaji wadogo Tanzania na wale walioko kwenye Vitalu vya *NARCO* vilivyomilikishwa kwa wawekezaji wadogo kwa kuwauzia mitamba na madume bora ya boran kwa nia ya kubadilisha mifugo yao iwe bora hasa katika kutoa nyama nyingi zenye ubora wa hali ya juu na kwa muda mfupi kuliko kutegemea ng'ombe aina ya zebu peke yake. Bila *NARCO* kuwezeshwa ni rahisi kabisa mbegu bora ya boran kutoweka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii haipati ruzuku yoyote katika kuendesha shughuli zake, bali mapato yake yanatokana na mauzo ya mifugo hasa ng'ombe wanaozalishwa katika Ranchi zake kumi. Kwa vile uwekezaji haujakuwepo kwa miaka mingi, idadi ya ng'ombe ambao wanaweza kuuzwa imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka na idadi ya wanaoweza kuuzwa kwa sasa haitoshi tena kugharimia shughuli za kampuni. Kuna Miradi mitatu ya unenepeshaji wa ng'ombe katika ranchi tatu ambayo imeanzishwa mwaka 2010/11 kwa mikopo ya CRDB na TIB. Mikopo hii itaanza kuonesha matunda katika miaka miwili kuanzia 2012. Kampuni hii haina budi kupata ruzuku kutoka kwa mmiliki ambaye ni Serikali ili kuweza kusimamia uuzaji wa majike na madume ya boran kwa wingi.

Mheshimiwa spika, Mkoa wa Kagera una Ranchi za Taifa za Mifugo tano kati ya tisa zinazomilikiwa na *NARCO* ambazo ni Missenyi, Kitengule, Kikulula, Mabale na Kagoma. Ranchi hizi zina kiasi cha eneo kama ifuatavyo: Mabale hekta 14,026.91; Kikulula 12,700; Kagoma 50,689; Kitengule 14062.094 na Missenyi 20,771.563. *NARCO* imebakiwa na hekta 45,026 tu.

Mheshimiwa Spika, katika kila Ranchi vimetengwa vitalu kwa ajili ya uwekezaji kama ifuatavyo: Kitengule 9, Mabale 6, Kagoma 17 na Missenyi 20. Jumla ya maeneo ya uwekezaji ni vitalu 52. Ziara ya Kamati katika maeneo yanayozunguka Ranchi Wilaya ya Muleba kutembelea Ranchi ya Kagoma na Vijiji vya Lubare na Lutoro na Wilaya ya Missenyi na

Karagwe kutembelea Ranchi za Taifa za Missenyi, Kitengule, Kikulula na Mabale.

Mheshimiwa spika, Kamati ilitembelea maeneo haya tarehe 1 Novemba 2011 na kujionea hali ya umaskini mkubwa na ya kusikitisha kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka ranchi. Hali kadhalika, Kamati haikuridhika na viwango vya uwekezaji uliofanyika kwenye mashamba yaliyobinafsishwa pamoja na mahusiano yaliyopo yenye uhasama kati ya wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa spika, Ranchi ya Kagoma ina ukubwa wa hekta 50,689 ikiwa na ngombe 2,263 na imepakana na vijiji mbalimbali vikiwemo vya Rubale na Lutoro. Vitalu vipatavyo 17 (hekta 34,377) vimegawiwa kwa wawekezaji na inapata kiasi cha shilingi 1,700,000 kwa mwaka kwa vitalu vyote hivi kwa mujibu wa mkataba ambapo malipo ya ukodishwaji wa vitalu kwa eka moja ni shilingi mia mbili na ishirini tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Ranchi za Taifa za Missenyi na Kitengule zilizopo Wilaya ya Missenyi na Ranchi za Taifa za Kikulula na Mabale zilizopo Wilaya ya Karagwe na kujionea hali halisi ya uwekezaji katika ranchi hizi zilizobinafsishwa pamoja na hali halisi ya maisha ya wananchi wanaoishi ndani na nje ya ranchi.

Mheshimiwa Spika, katika nyakati tofauti Kamati ilikutana na Wananchi wa Vijiji vya Kakunyu, Bugango, Bubale na Byeju, ambavyo vina migogoro na wawekezaji. Kamati ilipata malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi pamoja na wawekezaji wa maeneo husika ambayo kimsingi yanatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka kwa kuwa pande zote mbili zinaathirika na mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya ya Wilaya za Muleba na Missenyi Kamati ilibaini yafuatayo:-

Uhusiano mbaya kati ya wawekezaji na wananchi wa maeneo husika, kiasi kwamba amani na usalama vimetoweka katika maeneo haya, hakuna mipaka rasmi inayotambuliwa na wahusika wa pande zote mbili, yaani wanakijiji na wawekezaji, kiasi kwamba imesababisha migogoro mikubwa, kuwapo kwa madai ya unyanyasaji, kupigwa, kubakwa, kuchomewa makazi, matumizi ya risasi za moto, kubambikiwa kesi, kunyang'anywa mifugo, kutozwa faini nje ya utaratibu unaojulikana na wizi wa mifugo na wawekezaji kuingiza kwa nguvu mifugo yao kwenye mashamba ya wanavijiji.

Kamati pia imebaini kuwa wanakijiji wanazuiwa kulima katika makazi yao kwenye maeneo yaliyopo ndani ya ranchi, kuwepo kwa raia wengi wa kigeni wanaofanya kazi ya uchungaji katika vitalu vilivyobinafsishwa, raia hawa pia wanahusika katika uvunjifu wa amani kwenye maeneo ya wanavijiji, kiwango cha uwekezaji kilichofanyika katika vitalu vilivyobinafsishwa hakikidhi viwango vya kitaalamu vya ufugaji mfano; *paddocks, fencing,* majosho, mabwawa ya maji na uendelezaji wa malisho.

Vilevile Kamati imebaini kwamba, hakuna faida ya moja kwa moja inayoonekana kupatikana kwa wananchi wanaokaa maeneo yanayozunguka Ranchi za Taifa zilizobinafsishwa, kuonekana kwa dalili za chini chini kwa baadhi ya Viongozi wa Wilaya na Mkoa waliofuatana na Kamati kutokuwa tayari kuwapeleka Wajumbe wa Kamati kutembelea vijiji vinavyozunguka mashamba ya mifugo, baadhi ya wawekezaji kudharau wazi wazi wawakilishi wa wananchi yaani wabunge kwa kusema Mbunge ni nini bwana, wananchi wa maeneo haya wamekata tamaa kabisa dhidi ya watendaji wa Serikali na kupoteza imani na Serikali yao katika kushughulikia masuala yao ya msingi.

Hali ya afya kwa watoto kwenye vijiji hivi siyo ya kuridhisha, wageni wanaingia na kutoka ndani ya Tanzania bila kikwazo, hali hii inapelekea kushamiri kwa vitendo viovu na visivyochukuliwa hatua zinazostahili na baadhi ya wananchi wanalima na kuchungia mifugo ndani ya vitalu vya wawekezaji. Kulikuwa na tuhuma kuwa baadhi ya wanasiasa wanachangia kutokuwepo kwa ushirikiano baina ya wananchi na wawekezaji, wananchi wanatozwa gharama kubwa ya fidia ya kukomboa mifugo yao inapoingia katika maeneo ya wawekezaji. Gharama hiyo ni kiasi kisichopungua shilingi elfu thelathini kwa ng'ombe ambacho ni kiasi kikubwa kwa mfugaji na inasemekana kuwa wawekezaji waliomilikishwa vitalu siyo hasa wenye vitalu hivyo ila wametumiwa tu kuwa kama wamiliki. Wenye vitalu hivyo inasemekana wapo ndani na nje ya nchi na wana uwezo mkubwa kifedha au ni Viongozi wa ngazi za juu Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa za awali na Uongozi wa Mkoa wa Kagera namna Serikali ilivyochukua hatua mbalimbali za kutatua mgogoro huu. Uongozi ulisema kuwa, katika kila ranchi kumetengwa vitalu kwa ajili ya uwekezaji; Kitengule 9, Mabale 6, Kagoma 17 na Missenyi 20. Jumla ya maeneo ya uwekezaji ni vitalu 52.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliambiwa kuwa, Serikali ya Mkoa chini ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, ikishirikiana na Serikali za Wilaya ya Missenyi na Karagwe na zile za vijiji vilivyopo ndani ya hifadhi, ilifanya

tathmini kubwa na kutoa maoni kwa wananchi wanaoishi kwenye migogoro baada ya kukamilisha zoezi la kutembelea na kuona hali halisi ya makazi katika vitalu vyote vyenye migogoro.

Baada ya tathmini hiyo, Serikali ilikwenda kwa wananchi na kuwapa maoni yaliyotokana na hali halisi iliyoona katika maeneo husika na hivyo ilikaribisha maoni ya wananchi kutokana na mtazamo wao na agizo la Rais alilolitoa alipotembelea Wilaya ya Missenyi tarehe 14 Januari, 2007 kwamba; katika kushughulikia mgogoro uliopo kati ya wanavijiji walio katika maeneo yaliyo ndani ya Ranchi ya Taifa Missenyi na wawekezaji waliopewa vitalu vya kufugia katika eneo hilo ihakikishwe kwamba pande zote wanatendewa haki, yaani wanavijiji wasiondolewe na wawekezaji wasipoteze haki yao, bali wawezeshwe kuendelea na azma yao ya kuwekeza katika ufugaji ndani ya Ranchi ya Taifa ya Missenyi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hili, Uongozi wa Mkoa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ilitembelea vitalu vyote vilivyo na migogoro kwa lengo la kupata picha kamili ya ukubwa wa mashamba yanayolimwa, maeneo ya mashamba ya mifugo, idadi ya kaya zilizopo na watu, huduma za jamii zilizopo na kadhalika. Aidha, Uongozi wa Mkoa ulifanya vikao na viongozi wa vijiji na kujadili kwa pamoja taarifa iliyotokana na tathmini hiyo ya kutembelea vitalu vyote vilivyo na migogoro. Kazi hii ilifanyika kati ya tarehe 14 Mei – 12 Juni 2007.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini hii iligundulika kuwa baadhi ya vitalu vilivyotolewa kwa wawekezaji vimekuwa ni makazi ya watu kwa muda mrefu hivyo idadi ya kaya na watu kwa kila Kitongoji au *Block* imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika Wilaya ya Missenyi, Shamba la Mifugo Namba 287 limegawanywa katika jumla ya vitalu 22 vyenye jumla ya hekta 21,032.711, ambapo kuna Vijiji vinne vya Kakuyu, Bugango, Bubale na Byeju.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Kakunyu, mapendekezo ya Serikali yanaonesha kuwa vitalu namba 2 na 5 vina kaya nyingi za watu na hivyo viachwe kwa Serikali ya Kijiji na vitalu namba 1, 3 na 6 vibaki kwa wawekezaji. Aidha, ilipendekezwa kwamba, kwa kuwa Wakazi wa Kikunyu na vitongoji vyake wanategemea maji ya Mto Kagera, ilipendekezwa kwamba yatengwe mapitio ya mifugo kati ya kitalu Na. 1 na Na. 3 kwa ajili ya kupitisha mifugo yao kwenda Mto Kagera.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Bugango, Kitalu Namba 7 na 8 vilikutwa na idadi kubwa ya watu; hivyo, Serikali ilipendekeza kuwa vitalu

hivyo vibaki kwa wananchi pamoja na Kitalu Namba 4 kinachopakana na Kijiji cha Kakunyu. Pia njia ilitakiwa kutengwa kwa ajili ya wananchi kupeleka mifugo yao Mto Kagera pasipo kizuizi.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Bubale sehemu kubwa ya kijiji hicho ipo nje ya Ranchi na katika Kitalu Namba 14 na 15 kuna kaya chache; hivyo, Serikali ilipendekeza kuwa katika Kitalu Namba 14 na 15 kijiji kiongezewe hekta 350 kwa ajili ya matumizi ya wananchi na katika Kitalu Namba 16 kibaki kwa wawekezaji. Baada ya mapendekezo haya, Serikali ilifanya tathmini mpya baada ya kusikiliza mawazo ya wananchi wa eneo husika na ili kufikia mwafaka wa amani ya kudumu kati ya wananchi na mwekezaji, ilipendekeza tena kuwa Kitalu Namba 15 kirudishwe kwa wananchi na mwekezaji apewe kitalu kingine. Aidha, sehemu ya Vitalu Namba 14 na 16 ambazo zipo ndani ya Mto Kiboronga upande wa kijiji wapewe wananchi na zile zinazobaki upande wa pili ziunganishwe kiwe kitalu kimoja na apewe mwekezaji. Kwa mgawanyo huu, Mto Kiboronga kutoka Kitalu Namba 17 mpaka kwenye tingatinga (*swamp)* la Kakinga utakuwa mpaka wa Kijiji na Ranchi na hivyo wafugaji wa pande zote wataweza kutumia maji ya mto.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Byeju, Serikali ilipendekeza kuwa Kitalu Namba 19 na 21 wapewe wawekezaji na Kitalu Namba 20 na 22 vibaki kwa matumizi ya wananchi. Hata hivyo, baada ya maoni ya wananchi na kufanya tathmini upya, ilipendekezwa kuwa Kitalu Namba 21 na 19 wapewe wananchi kwa kuwa sehemu kubwa zina kaya nyingi na sehemu za mabondeni zimejaa maji. Katika eneo hili kuna mfugaji anamiliki zaidi ya hekta 1,200 za kitalu na amewekewa mipaka ya shamba lake. Aidha, kwa upande wa Kitalu Namba 19 sehemu kubwa ipo mpakani mwa Uganda ambayo haina makazi hivyo ilipendekezwa ipimwe upya ili iunganishwe na Kitalu Namba 17 kwa matumizi ya mwekezaji ili kusaidia kudhibiti uingizaji wa mifugo holela kutoka nchini Uganda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ziara katika maeneo ya Ranchi za Kagoma, Mabale, Kitengule, Kikulula na Missenyi na maeneo ya wananchi yanayozunguka Ranchi hizo, Kamati ilishuhudia na kujionea mambo ya ujumla yafuatayo:-

Kuna uhusiano mbaya kati ya wawekezaji, *NARCO* na wananchi wa maeneo husika ambapo amani na usalama imetoweka katika maeneo haya, kuna migogoro mikubwa ya mara kwa mara kati ya wawekezaji ya unyanyasaji, kupigwa, kubakwa, kuchomewa makazi, matumizi ya risasi za moto, kubambikiwa kesi, kunyang'anywa mifugo, kutozwa faini nje ya utaratibu unaojulikana na wizi wa mifugo. Baadhi ya

Ranchi hazina mipaka maalum inayotambuliwa na wahusika wa pande zote mbili, yaani wanakijiji na wawekezaji.

Kuna madai kutoka kwa Watendaji wa Mkoa, Wilaya na Vijiji kuwa baadhi ya wanasiasa wanachangia hali ya kutokuwepo kwa uelewano na ushirikiano baina ya wananchi, wawekezaji na watendaji wa Mkoa katika ngazi mbalimbali. Kuna wahamiaji haramu kutoka nchi za jirani ambao wanajihusisha na shughuli za ufugaji nje ya taratibu zinazokubalika na baadhi ya Viongozi wa Vijiji wamekuwa wakiwahifadhi wahusika na kuwatetea. Wawekezaji kuingiza kwa nguvu mifugo yao kwenye mashamba ya wanavijiji lakini wanavijiji kuzuiwa kulima katika mashamba yaliyomo ndani ya ranchi za wawekezaji. Baadhi ya Ranchi za wawekezaji hazijaendelezwa ipasavyo kama mikataba inavyowataka. Aidha, kiwango cha uwekezaji kilichofanyika katika vitalu vilivyobinafsishwa hakikidhi viwango vya kitaalamu vya ufugaji mfano; *paddocks, fencing,* majosho, mabwawa ya maji na uendelezaji wa malisho. Baadhi ya kaya zinaishi ndani ya vitalu vya mashamba ya mifugo hivyo kuna mwingiliano mkubwa wa shughuli za wanavijiji na shughuli za mwekezaji, mipaka ya Tanzania na nchi jirani haijafyekwa na hailindwi ipasavyo. Wageni wanaingia na kutoka ndani ya Tanzania bila kikwazo, hali ambayo inapelekea kushamiri kwa vitendo viovu.

Kuna madai kuwa baadhi ya wawekezaji siyo wamiliki sahihi wa vitalu, wapo kwa niaba ya watu fulani wa ndani na nje ya nchi. Baadhi ya wananchi wa maeneo husika wamekata tamaa na utendaji wa Serikali ya Mkoa, Wilaya na Kijiji katika kutatua migogro yao. Pia kuna malalamiko kutoka kwa Wananchi kutozwa fidia kubwa ya kukomboa mifugo yao inapokutwa kwenye mashamba ya mifugo ya wawekezaji na Kusitishwa kwa zoezi la kutambua na kuwarudisha nyumbani wahamiaji haramu kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara ya Wilaya za Muleba, Karagwe na Missenyi wakati wa kutembelea Ranchi za Taifa zilizopo ndani ya Wilaya hizi na kuzungumza na wawekezaji, Uongozi wa *NARCO,* wananchi wa maeneo husika na Uongozi wa Mkoa kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo:-

Serikali kupitia vyombo vyake husika viweke mipaka ya Ranchi za Taifa ili itambuliwe na kuheshimiwa na pande zote mbili. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali kufungua Kambi ya JKT katika maeneo ya mipaka ili kuongeza ulinzi na usalama katika maeneo haya na kuwa jicho la Taifa kwenye mipaka yetu. Aidha, iimarishe Kambi ya JWTZ Kaboya ili kuimarisha hali ya ulinzi.

Serikali ichukue hatua madhubuti ya kudhibiti vitendo viovu vinavyofanyika katika maeneo ya vijiji na ya wawekezaji ili kurudisha amani katika maeneo husika. Aidha, Watendaji wa Vijiji wafanyiwe tathmini ya uraia wao kwa kuwa kuna madai ya kuwa wengi wao siyo Raia wa Tanzania na wanawasaidia wahamiaji haramu. Serikali iendelee na zoezi lake la kuwatambua na kuwarudisha wahamiaji haramu waliopo katika wilaya hizi. Aidha, adhabu kali zichukuliwe kwa wale watakaobainika kuishi ndani ya nchi bila kibali ikiwa ni pamoja na wale wanaowahifadhi kinyume na taratibu. Serikali iwachunguze baadhi ya Watumishi wa Serikali katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vijiji vya Mkoa wa Kagera ili kubaini ushiriki wao katika mgogoro huu. Serikali ifanye mapitio ya mikataba ya wawekezaji kwenye Ranchi hizi hasa katika suala la malipo ya ukodishwaji wa vitalu. Kiasi kinacholipwa sasa kwa eka cha shilingi 220 kwa mwaka hakina tija na wala hakisaidii mapato ya Serikali kama njia mojawapo ya kuendeleza uchumi wa nchi kupitia ufugaji.

Serikali kupitia Wizara yake ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iweke Mpango Bora wa Matumizi ya Ardhi katika maeneo haya ili kupunguza mwingiliano wa shughuli kati ya wafugaji na wakulima. Serikali iwachukulie hatua Viongozi wa Vijiji ambao wamekuwa wakiuza ardhi kubwa kwa wahamiaji haramu, wawekezaji na wananchi bila kufuata taratibu na sheria za ardhi pamoja na mpangilio bora wa watumizi ya ardhi. Kwa mujibu wa kifungu Na. 20 (i) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na ile ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999, mtu ambaye si raia wa nchi hii haruhusiwi kumiliki ardhi isipokuwa kwa madhumuni ya uwekezaji tu na atamilikishwa ardhi hiyo chini ya Sheria ya Uwekezaji Nchini ya Mwaka 1997. Serikali iwanyang'anye mashamba wawekezaji ambao hawajatimiza masharti ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione uwezekano wa kuisaidia mahakama ili kesi zilizopo mahakamani zinazohusiana na matatizo ya ranchi zisikilizwe ili kutoa fursa na haki kwa pande zote mbili, yaani wawekezaji, wananchi na Uongozi wa Ranchi. Wanasiasa washirikiane na watumishi katika kutatua migogoro kwenye maeneo yao kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo bila kuathiri utendaji kazi wa Watumishi wa Serikali, uwepo wa wawekezaji na shughuli za wananchi. Upanuzi wa mashamba ya miwa uangaliwe upya ili kuruhusu baadhi ya maeneo kuwa wazi kwa ajili ya malisho ya mifugo na kwenda mtoni kwa ajili ya maji. Serikali itoe fedha kwa *NARCO* ili iweze kutekeleza Mpango wake wa Miaka Mitano uliobuniwa mwaka 2005 ambao utekelezaji wake unahitaji shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kurekebisha miundombinu na ununuzi wa ng'ombe hasa boran. Utekelezaji wa *NARCO* katika kusimamia na kuendeleza ufugaji bora hasa ng'ombe bora wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje umekuwa wa pole pole sana kwa

sababu ya ukosefu wa fedha. Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2006/2007 *NARCO* ilikuwa na idadi ya ng'ombe 36,813, mpaka Desemba 2011 idadi ya ng'ombe waliopo ni 23,798.

Mheshimiwa Spika, Serikali iisaidie *NARCO* katika jitihada za kutafuta wawekezaji kwa kuingia ubia nao, wenye uwezo wa fedha, utaalamu wa mifugo na pale inapowezekana masoko. Wawekezaji watakaopatikana wanatarajiwa kuongeza tija katika kuboresha mazingira ya Ranchi, utendaji na uzalishaji pamoja na ajira ili kuinua Sekta na Uchumi wa Taifa kupitia shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu, kwa kukubali ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuunda Kamati yake Ndogo kufuatilia malalamiko ya wananchi kuhusu mgogoro wa ardhi kati ya wawekezaji wa kwenye Ranchi za Kagoma, Mabale na Kitengule, Kikulula na Missenyi na wananchi wa maeneo hayo.

Shukrani za dhati ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kujitoa kwao na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wajumbe wa Kamati Ndogo ambao walijitoa kwa hali na mali na kufanya kazi bila kuchoka. Kwa hakika wamefanya kazi kubwa sana na wanastahili pongezi. Vilevile shukrani zetu ziende kwa Watendaji wote wa Serikali ya Mkoa, Wilaya na Vijiji, kwa ushirikiano wao na kutuwezesha kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuisaidia Kamati hii kufanya kazi vizuri. Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano walioipa Kamati katika kutekeleza jukumu hili kubwa. Mwisho kabisa lakini kwa umuhimu wa pekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Chacha Nyakega, kwa kuisaidia Kamati na kufanikisha kumaliza kazi hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante, nashukuru sana kwa taarifa yenu. Sasa Waheshimiwa Wabunge, mpaka saa 7.00 naweza kupata wachangiaji sita tu na nitaanza na wale ambao hawajachangia kabisa, halafu kama

nafasi inatosha waliochangia mara moja watapata nafasi. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Charles Tizeba na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili na mimi niweze kuchangia katika taarifa hizi mbili zilizotolewa siku hii ya leo. Awali kabisa, naomba niwapongeze Wenyeviti wote wawili kwa kutoa maelezo mazuri sana katika taarifa zao. Lakini vilevile kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kuzungumza tangu kuzungumzia taarifa hizi, naomba niwapongeze vilevile Wenyeviti wengine wote ambao walifanya kazi kwa makini sana na wamefanya tathmini nzuri sana ambazo zimekuwa ni kwa ajili ya afya na kwa ajili ya kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Awali kabisa, naomba niipongeze Serikali kwa kuweza kuisaidia Kamati hii pamoja na Kamati nyingine kuweza kufanya Semina kwa Wabunge ambao hasa katika eneo hili walipata nafasi ya kujifunza athari zinazotokana na tabia nchi. Suala hili ni muhimu sana na tumejionea wazi kwamba mara nyingi hatuko makini sana kuzungumzia suala la tabia nchi na athari zake. Tumejionea majanga mengi sana yakijitokeza hivi karibuni na katika historia ya nchi hii kwa kweli imekuwa ni tatizo. Tumejionea wenyewe mwaka huu na mwaka jana jinsi nchi yetu ambavyo imeweza kupata mafuriko makubwa sana pale Dar es Salaam, wananchi wamehangaika sana na mpaka kusababisha uhamisho kwenda maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tumejionea jua kali sana, tumejionea mafuriko maeneo mbalimbali katika nchi yetu na katika dunia ya leo. Kwa hiyo, naomba sana Kamati hii sasa ijielekeze tena katika kutembelea maeneo ambayo yanahusu hifadhi ya milima, ambayo ni chanzo kikubwa sana cha maji; milima mingi sana, hasa safu ya milima ya *Livingstone*, Kilimanjaro, Rungwe na Uluguru imeharibiwa sana. Ukitoka Dodoma unaelekea Dar es Salaam unapofika maeneo ya Morogoro unajionea jinsi gani ambavyo nchi sasa inakwenda pabaya.

Milima ya Uluguru ilikuwa ni milima inayotiririsha maji mengi, maji mazuri ambayo baadaye yalianzisha hata bwawa la Mindu. Sasa milima ile ni vipara kabisa na haivutii kabisa. Ni kwa sababu misitu ambayo iko kule juu, imefyekwa yote, watu wanalima hovyo bila kuzingatia Kanuni za Kilimo. Kwa hiyo, milima ile haifai tena.

Mheshimiwa Spika, naomba Kamati hii iombe Serikali iwapeleke kwenye maeneo yale wakajionee wenyewe. Mimi nakumbuka Serikali ilishatoa maelekezo kwamba wananchi wanaoishi katika milima ya Uluguru wateremshwe chini ili kuweka nafasi ya kurudisha tena uoto wa asili katika milima ile. Utekelezaji mpaka leo hakuna na badala yake bado wananchi wanazidi kukwatua milima ile na kuifanya kama sesa, jambo ambalo mimi sitashangaa kama katika kipindi kifupi kijacho milima ile ikiporomoka na kufunika wananchi wanaokaa chini. Hali ni mbaya! Naomba Kamati hii itusaidie na Serikali kwa ujumla. Ukienda kwenye safu ya milima ya Livingstone, mambo ni hivyo hivyo. Utaona na kushuhudia milima ikichomwa moto hovyo hivyo. Utaona wananchi wanalima huko hovyo hovyo, hakuna mtu anayejali, hakuna mtu anayezungumzia! Tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukasema kiuchumi tunakwenda mbele ndiyo, lakini kama hatutahifadhi milima hii ambayo ndiyo uchumi wa nchi, ndiyo uhai wa Tanzania. Kwa kweli tutashitukia tunakwenda katika kujiua wenyewe. Naomba suala hili lizingatie. Lakini tuna milima mingine Mlima Kilimanjaro ambayo nilizoea kuiona kule nako hivyo hivyo, watu wanaingia mpaka misituni na misumeno na kukata miti hovyo na misitu inatoweka kabisa na leo tunalia kwamba *ice* ile inayeyuka. Ni kwa sababu kuna haya maeneo ambayo sisi wenyewe tunaweza tukayafanya. Yapo maeneo ambayo hatuwezi tukayafanya. Lakini kukata miti, kuhifadhi mazingira tunaweza. Tunaweza kabisa. Kwa hiyo, nilidhani hili nilizungumzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama ziara zinafanyika, basi ziara hizo zilenge kwenda kuona maeneo hayo kwa macho. Nashukuru kwamba Kamati imeweza kutembelea maeneo ya migodi, wamejionea wenyewe jinsi gani migodi hiyo na yenyewe inachangia katika kuharibu mazingira ya nchi hii bila kurudishia hali ile ya asili. Naiomba Kamati, kama mlivyoanza, Mwenyekiti kama ulivyoanza naomba uhimize Serikali mwende mkajionee maeneo yote ambayo madini yanachimbwa. Naomba suala hili la hifadhi ya mazingira lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba nilizungumzie suala la kilimo. Ni kweli suala la Kilimo Kwanza limekuwa ni dhana nzuri, dhana ambayo wananchi wamejengewa imani kwamba wataondokana na umaskini. Lakini bado kuna mambo mengi ambayo Kamati imeyaangalia hapa, lakini yanatakiwa yaangaliwe kwa undani zaidi. Suala la usambazi wa pembejeo kama lisipoangalia vizuri, tunaua kilimo moja kwa moja. Hakutakuwa na uhai wowote wa kilimo iwapo mipango ya usambazaji wa pembejeo hautakuwa thabiti. Ninaomba utaratibu wa mwaka jana

uliotumika katika kuchelewesha kusambaza pembejeo usirudiwe tena kwa sababu wanachi walikata tamaa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi wapelekewe pembejeo wakati ule au kabla msimu haujaanza, sio wakati msimu umeshapita. Hilo lisirudiwe, wala haiingii akilini, kama mkulima anataka tu asaidiwe hayo, lazima tuyaangalie. Vilevile mwaka jana, 2011 wananchi walipelekewa pembejeo wakati ambapo wanapalilia wakati wamepanda bila pembejeo. Haisaidii kitu chochote! Wizara iwe na ratiba mezani inayoonyesha ratiba za kilimo nchi nzima. Kwa hiyo, lazima kuwe na madawati hayo ndani ya Wizara ambayo yanaonyesha kwamba leo, au msimu huu, au mwezi huu, Wilaya fulani, Mkoa wa Njombe ndiyo ambao unatakiwa upelekewe pembejeo. Wafanye hivyo na kuhangaika kufa na kupona wananchi wa Mbeya wapate pembejeo kabla ya kilimo. Hivyo hivyo inapofika msimu wa pembejeo za kupandia, hapo ndipo tutakuwa tumejibu hoja ya Kilimo Kwanza. Lakini hoja ya Kilimo Kwanza vilevile lazima ijibu hoja ya uvuvi. Hoja ya uvuvi lazima ijibiwe vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi na mimi niweze kuchangia katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwa makini hiyo taarifa. Mambo mawili yamejitokeza ambayo ni ya fedha na mambo ya aibu kwa Serikali yetu. Jambo la kwanza katika uchunguzi, imedhihirika kwamba kuna wizi mkubwa, hujuma kubwa, ujambazi mkubwa unaofanyiwa rasilimali za nchi hii. Kwa mtaji huo, hatufiki. Nataka kuiambia Serikali, sasa wameamua kuiba hata vitu visivyoibika, vinavyoonekana waziwazi. Mwaka 2009 tumeambiwa tembo wanne, mmefikia mahali hata tembo mnawapeleka Pakistan. Mwaka 2010, twiga wawili, viboko wawili, kudu wawili, *elands* wanne kwenda Japan. Wananchi wa Tanzania nataka kuwaambia kitu kinachotisha, ndiyo sababu tunasema Mawaziri mjiuzulu mnaona tunawasukuma, tunawaonea. Hatuwaonei! Vitu hivi mnavyofanya vya aibu na vya fedheha.

Mheshimiwa Spika, tena leo nilikuwa nasema ufunge milango yote tushikane mashati huku ndani, hakuna kutoka mpaka tujue kwanini nchi hii inaendeshwa hivi? Tatizo ni nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unaambiwa hawa wanyama wamepelekwa hakuna nyaraka, hakuna barua, hakuna vielelezo. Ndivyo Kamati inavyosema, wala hakuna barua ya maombi kutoka Pakistan kwamba tunataka hao wanyama, tunataka hao tembo wala hakuna *dispatch* ya kuonyesha kwamba hao wanyama walikwenda Karachi Pakistan. Tunaendesha nchi hii namna gani jamani? Mnasema tunaonea Serikali, tunawasukuma na mnasema hamjiuzulu ng'o! Katika mazingira kama haya ni sababu zipi mtakazowaambia Watanzania kwanini msijiuzulu. Hakuna *dispatch*, hakuna nyaraka yoyote. Hii nchi inaendeshwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kuna huyu Kamran Ahmed, huyu anaambiwa ni Mwakilishi wa Pakistan huku. Hakuna barua, hakuna nyaraka, hakuna jambo lolote linalomwonyesha kwamba ni Mwakilishi halali wa Serikali ya Pakistan na hiyo mikataba amefanya mtu asiyejulikana, mtu asiyefahamika, mtu anachukuliwa *from no where,* wanafanya mikataba ya kuchukua wanyama kwenda Pakistan. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, huu ni wizi. Hauwezi kuvumiliwa! Watanzania hawatakubali. Mnaiangusha Serikali yenu nyie wenyewe viongozi wa Chama cha Mapinduzi. *Why*? Kwanini tunatia aibu? Kwanini tunatia fedheha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vibali vya kusafirisha wanyama, vile vibali vilitolewa kwa udanganyifu, kwa hila. Sheria inasema Mkurugenzi wa Wanyamapori ndio anatakiwa atoe lakini badala yake wanatoa watu wengine wasiohusika. Wanatoa vibali vya udanganyifu, vibali vya uongo na vibali *fake!* Mambo haya yamefichuliwa na hii Kamati. Naipongeza sana. Kwa hiyo, la kwanza nililoliona ni wizi mtupu! Mtu anaiba kuku anapigwa mawe anakufa, watu wanaiba twiga, wanaiba tembo, bado wako Dar es Salaam wanatembea na ni watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kuhusu rushwa, naambiwa hii *Jungle International* ni kampuni hewa. Kampuni haipo, taarifa zake hazipo *BRELA* wala hawakupeleka maombi. Jamani hebu fikiria mtu hajaomba kitu, lakini anapewa twiga, anapewa tembo. Sisi tueleweje jamani? Mnatuona sisi Wapinzani kama nyanya mbichi. Sasa tufanyeje? Sisi tutaendelea kusema tu, mpaka mtusikie, sio kwamba tunawaonea. Mambo yenyewe mnafanya waziwazi haya. Rushwa nyingine Kamran Ahmed huyu anamiliki kibali cha ukamataji wa wanyama na ni mgeni. Raia wa Pakistan kampa nani hicho kibali cha kudumu cha kukamata wanyama kila anavyoona inafaa? Haya, kugawa vitalu kwa makampuni ambayo hayakuomba.

Mheshimiwa Spika, fikiria makampuni 16 hayajaomba, mtu hajaomba kitalu anapewa. Jamani hii nchi ina huruma kiasi gani? Kuna Kamati za kumshauri Waziri, hakuzingatia ushauri wa zile Kamati. Sasa kinachojitokeza, tunaambiwa wale watu wasiokuwa na vigezo, wasiokuwa na uwezo wa ku-*qualify* wanatoa hela Dola 150,000 mpaka Dola 250,000 wanapewa kitalu, kukiendeleza hawezi. Yeye anakwenda kukiuza Dola 600,000. Ni nini hii? Ni kitu gani tunafanya kwenye nchi hii? Yaani mnafanya Watanzania wote ni wajinga, hatuna macho, hatuoni? Tukisema, mnatuona sisi watu wabaya, mnatunyooshea vidole. Mnajidai nini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrema, hii taarifa ni ya Kamati, sio taarifa ya Upinzani. Ni Kamati ya Bunge.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante. Sasa kinachonifanya niwe na hasira, na watu wangu wa Vunjo wawe na hasira, na watu wa Kilimanjaro, asilimia 60 ya fedha zote za utalii zinatoka Kilimanjaro, *60 percent* ni fedha nyingi katika fedha zote zinazoingizwa. Ni fedha nyingi katika fedha zote zinazoingizwa. Sasa kama mmeanza kuwashugulikia wanyama, mnaanza kuhujumu hayo mapato yatakujaje kule? Tumeomba fedha hizo za utalii ili tuendelee kuimarisha kule, tupewe asilimia 15 ya mapato ya *TANAPA.* Hatujapewa mpaka leo! Tangu nimeingia Bungeni, tunaendelea kuomba, Mheshimiwa Mbowe ameomba hizo fedha zihudumie ule Mlima, mnasema tumeendelea hatujaendelea. Mimi naomba, kama mnataka kujua, nendeni barabara ya Uchira kwenda Kisomach ndiyo mtajua kwamba siyo kweli Moshi kuna maendeleo. Kuna zile barabara za mkoloni zimejengwa, lakini ukienda barabara za vijijini, hazipitiki. Barabara ya Kilimatofu kwenda Kilema Hospitali, haipitiki. Hata ile inayokwenda Kilaracha kutoka kwa Mrema kwenda kwa Msuya haipitiki. Sasa hayo maendeleo tunayosema ni ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, tulitegemea kwamba kama tungehifadhi hawa wanyamapori wetu hivi vitalu vyetu nina hakika nchi hii ingetajirika. Tunasema nchi hii ni maskini. Siyo maskini! Kuna vyanzo vingi vya mapato. Kuna rasilimali nyingi, kama zingesimamiwa na kudhibitiwa. Nataka niseme tu ndugu zangu, hebu tuionee huruma nchi hii, tuwaonee huruma Watanzania, tukienda kwenye shule hakuna madawati, watoto wanakaa chini, lakini twiga anakwenda Pakistan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda sasa hivi wanalalamika kule, mbolea haijafika jamani, na kama imefika ni kwa ajili ya watu wachache tu, walio wengi hawajapata mbolea.

Mheshimiwa Spika, maji ya kunywa kule Mwika, Mheshimiwa Rais atakwenda kule wiki hii. Mwika hakuna maji kwa wananchi wangu. Kwa nini tusimsaidie Rais wetu jamani nchi hii ikatawalika vizuri? *Why?* Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachotaka kusema hapa ni kwamba, hizi Kamati za Kudumu za Hesabu za Serikali, za Mashirika ya Umma *(PAC, POAC, LAAC)* pamoja na Kamati nyingine zilizokuja hapa, tumesema maneno mengi sana kwa uchungu hapa kwa sababu tunaona nchi hii haiendi vizuri, madhambi ni mengi, fedheha ni kubwa. Mwenye macho haambiwi tazama, na sisi tunaona! Sasa tukiwashauri, ninyi mnakuwa jeuri, mnakuwa wababe, mnasema hajiuzulu mtu hapa! Sasa tufanyeje?

Mheshimiwa Spika, sasa makosa kama haya ya kupeleka Twiga Pakistan, hawana kibali, hawana barua, hakuna *dispatch*, tunyamaze? Huu si ujambazi? Huu ni wizi? Sisi tutaendelea kusema tu, tutaendelea kupiga kelele tu, watu watatusikia. Lakini ninachotaka kuwashauri jamani, hapo mlipokwishafikisha nchi hii sasa semeni basi inatosha, tusiendelee hivyo. Kama mtu anashindwa eneo lake la kazi, si anawajibika? Mbona mimi niliwajibika? Mimi nilikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri Mkuu, nilivyoona Chavda amechukua fedha za wahisani, akajidai kuendeleza yale mashamba ya Mkonge Tanga, hakuyaendeleza, niliondoka. Mpaka leo nina heshima yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja na mapendekezo yote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tena unataka kusahau, ulikuwa Naibu Waziri Mkuu, siyo Waziri tu. Kwa hiyo, ulitoka. Haya basi, haya. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii fupi niseme mawili matatu kwa yale ambayo ninataka kuyazungumza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii na mimi kuwapongeza wawasilishaji wa leo wa taarifa za Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfumo huu ambao tunakwenda nao wa kuwa pamoja katika kujadili taarifa hizi bila kujali itikadi za kisiasa, uendelee na tuudumishe ili kweli tufike mahali tulijenge Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna nia njema, tuna nia njema kabisa. Hatuna cha kuwa na mtu rohoni, hatuna nia ya kuharibu maisha ya mtu, tuna nia ya kujenga Taifa hili ambalo kwa kweli tumetoka nalo mbali, kama akina mama Hewa hivi, tumetoka mbali sana. Tunatakiwa kuona tulikotoka, tulipo sasa na mbele ya safari. Taifa hili tunalipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kuzungumzia suala zima la chakula, kuhusiana na mgao wa chakula hapa nchini. Naanza kuzungumzia taarifa ya kilimo.

Mhesimiwa Spika, tunalima. Tanzania ni nchi ya wakulima. Asilimia kubwa ni ya wakulima, wanalima. Lakini bahati mbaya tu wanadhalilika na hali ya hewa, wanadhalilika na mabadiliko haya tunayosema ya tabianchi, wanalima lakini wanaambulia sifuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna maeneo mengine wanalima na wanapata chakula cha kutosha. Kwa mfano, kama Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, labda na Kigoma na wenyewe wanapata chakula. Sasa, Taifa ni moja, tunapaswa kugawa chakula au kusafirisha vyakula kwa maeneo ambayo yanakosa chakula cha kutosha katika Mikoa mbalimbali, kwa mfano, Mwanza, Mikoa kama hapa Dodoma ambapo kabisa ukame ndiyo umekithiri kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, unakuta maeneo sasa huko waliko wenzetu, Mungu kawabariki wamepata chakula, wanabaki nacho, kinawaozea huko, kinawaotea huko, kinanyeshewa mvua, wanalalamika tena kwa kuzungumza kabisa, "jamani njooni mchukue chakula, sisi chakula kimetuzidi!" Ni kitu gani? Serikali ni kwa nini inashindwa kusema ndiyo tunakuja? Badala yake ni kimya. Panakuwa na ukimya kabisa huku watu wanakosa chakula, badala yake wanapata mlo wa mara moja wakati kumbe huko kwingine chakula kinawaozea mpaka wanageuza wanafanya mbolea kwa msimu unaofuata. Ni haki? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aibu!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Jamani, naogopa kusema aibu kwa sababu ni Serikali yangu!

**MBUNGE FULANI:** Sema tu!

**MHE. MARIA I. HEWA:** *Message sent! (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika kuishi kwa kawaida, naona magari ya Jeshi, wenyewe nadhani wanaamrishwa tu, "toa gari", zinatoka, ndiyo

wanaosafirisha chakula. Lakini siri iliyopo, nadhani ni pesa. Ukimwuliza Waziri wa Kilimo, anakwambia Mama Hewa, (mimi labda niseme, niko katika Kamati hiyo, nimetajwa mmenisikia) hakuna pesa. Hivi kweli hakuna pesa? Hivi kweli!

Mheshimiwa Spika, najua tatizo letu Watanzania tunapenda kufanyia kazi matukio. Tungelisikia kwamba kuna watu wameanza kufa njaa Mwanza, Kagera, wameanza kufa njaa mahali fedha zingepatikana. Huu ukimya nadhani ndiyo unatuponza. Lakini fedha sidhani kama kweli tunakomba mpaka tunamaliza tusipate ya kusafirisha chakula. Watu wanakula mlo mmoja, kumbe mahali pengine vyakula vinanyeshewa mvua mpaka vinaota, wanatupa; mahindi mpaka yanasubiri kwenda kuwekwa mbolea msimu unaokuja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba katika hili, hebu Serikali ishituke. Tusifanye kazi kwa kusubiri matukio. Hatutaki kutangaza vifo ndiyo tufanye kazi. Mimi ninaamini kama kweli hili tunalibebea bango, tunaweza tukalifikisha tu mahali pazuri, chakula kikasafirishwa.

Hata juzi Mbunge mmoja wa Sumve alisema, mimi nina eneo la kuwekea, lipo ghala pale Kwimba, Nkalalo. Hata kama mnapoleta hivyo vyakula kwenye Mikoa, vyakula vyenyewe vinakuja kidogo, havitutoshi. Naomba hili tulibebee bango. Nilitaka niliseme hili kwa kirefu ili tusije tukafika mahali tukaanza kupata maafa, kumbe vyakula vinaoza kwenye Mikoa wanayozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili na la mwisho ni suala zima tunalowagonganisha wawekezaji. Tunapogombana na wawekezaji kuhusu masuala ya kilimo, masuala ya mifuko na masuala ya makazi ya wananchi, naomba Serikali ifike mahali waweze kuwaelimisha viongozi katika ngazi za Vijiji. Serikali inaposema wawekezaji nendeni mahali fulani, mmejiandaa kuwapeleka mahali fulani, kumbukeni kule watu wanalima, wana mifugo, wanahitaji pia makazi. Siyo kuwapeleka tu wawekezaji, basi masuala ya kilimo, ufugaji na makazi yanavurugika.

Mheshimiwa Spika, tunawataka wawekezaji, sawa. Lakini tusiathiri kilimo, tusiathiri makazi, na tusiathiri mifugo. Kutufukuza, kufukuza wafugaji sisi hatutaki kwa sababu wawekezaji hawa wanakuja kubeba maeneo yetu ambayo tunafugia mifugo, tunalima na tunataka kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwisho, ni taarifa tu kwamba pembejeo sasa hivi zinazokuja, pamoja na kwamba zinachelewa, hata kupelekwa kwenye maeneo, lakini nazo zinachakachuliwa. Pembejeo sasa hivi wanaweka huko, wanachanganya na chumvi ya kawaida tunayolia

kwenye vyakula. Mfuko mmoja unagawanywa nusu, nusu chumvi hiyo ya mbolea na nusu chumvi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza. Lakini naomba Serikali izingatie tunayoyasema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, naomba niseme kwamba mimi ni mjumbe katika Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kwa hiyo, naunga mkono hoja iliyowasilishwa. *(Makofi)*

Naomba kwanza nianze mchango wangu na kazi za Kamati. Katika ziara yetu tumepitia maeneo mbalimbali ikiwemo migodi na mashamba ya miti. Ninao ushauri kwa Serikali. Ushauri huu haukujitokeza vizuri kwenye ripoti yetu, naomba nitumie muda huu kuuwasilisha. Mashamba ya Miti, Vijiji vinavyoyazunguka havinufaiki kama inavyopaswa. Tumesikia malalamiko ya Mufindi na maeneo mengine. Natolea mfano tu wa shamba la Buhindi lililoko katika Jimbo langu. Shamba hili linazungukwa na Vijiji 16. Lakini tangu liwepo, Vijiji vitatu tu ndiyo vinanufaika na shamba lile. Hii naamini iko kinyume kabisa na sera ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu ni kwamba kama zilivyo maliasili nyingine, basi ile 25% inayotolewa kwenye maeneo yenye vitalu vya uwindaji, vyenye mbuga za wanyama na nini, basi na maeneo haya yenye mashamba ya miti na wao wapate 25% inayotokana na maduhuli yanayopatikana kutoka kwenye mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni pale Bulyankhulu. Ni mgodi ambao upo mpakani mwa Wilaya mbili, Wilaya ya Kahama na Wilaya mpya ya Nyagh'wale. Lakini utakuta mgodi unajihusisha zaidi na masuala ya kijamii ya upande mmoja wa Kusini wa Kahama. Eneo la Nyagh'wale, Vijiji kama zaidi ya nane havionekani kabisa kupata msaada wa aina yoyote kutoka kwenye mgodi huu wakati vinapakana *fence* ya mgodi inapakana na Vijiji hivyo. Tofauti tu ni kwamba eneo la uchimbaji liko kwenye eneo la utawala la Wilaya ya Kahama. Kwa hiyo, tuombe tu kwamba na hawa athari zinazowapata wenzao wa Kusini, zinawapata pia na wenzao wa Kaskazini. Kwa hiyo, ni vyema wanapogawanya ile *corporate social responsibility* yao, waangalie sehemu zote zainazozunguka mgodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, nitoe pongezi kwa Kamati Ndogo ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kazi nzuri waliyofanya. Mzee Mrema amegusa gusa, mimi sipendi kuingia kwenye *details*. Lakini, tuite kijiko, kijiko; koleo, koleo na siyo kijiko ni koleo ndogo. Hapa upo uozo wa kutosha tu na mtu asijaribu kutafuta namna yoyote ya kujihalalisha katika

jambo hili. Watu wamekiuka sheria, watu wamekiuka taratibu, hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaposema hatua zichukuliwe, isiwe jumla jumla. Uchunguzi ufanyike na katika hizo hatua asionewe mtu. Upo uwezekano wa watu kuzolewa zolewa wakaingizwa waliokuwamo na wasiokuwamo. Kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali, itakapokuwa inafanya uchunguzi wa hili jambo, kwa hatua za kuchukua dhidi ya Watendaji waliojihusisha, basi uonevu usije ukatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatatizwa sana na huyu mtu anayeitwa Kamran. Kwa kesi iliyo Mahakamani sitamzungumzia, lakini kwa haya matendo aliyoyafanya, muda haukutosha kumsema vizuri katika Kamati hii bwana huyu. Ni mkaidi! Anaogopewa! Maafisa wa Serikali wanaogopa hata kufika nyumbani kwake. Lakini nakumbuka maneno ya Mwalimu kuhusu mtu mmoja sijui visiwa gani vya *Cyprus* aliyedai kaiweka Serikali yake mfukoni, Mwalimu aliwahi kuuliza: Hivi ana mfuko mkubwa kiasi gani wa kuiweka Serikali nzima ndani yake? Sasa huyu Kamran ana nini? Anaishije hapa nchini kwa uvunjaji wote wa sheria hizi na hajaondolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, mtafute huyu Kamran umwulize. *Status* yake ya ukaaji hapa nchini ikoje? Haiwezekani bwana mmoja tu *"a fake"*, kwa sababu *documents* anazo-*exist* nazo hapa, hazina *authenticity* ya aina yoyote. Yupo anaendelea kutuvunjia sheria zetu. *Why?* Kama kuna mengine, aulizwe, basi watuambie, yaani yeye ni nani katika nchi hii kwamba aweze kufanya yote haya na asichukuliwe hatua stahiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakumbuka tangu Bunge la Tisa vitalu vilipigiwa kelele hapa Bungeni? Hatukuwemo sisi, lakini tulikuwa tunashuhudia. Ikaenda, ikarudi, zoezi likaahirishwa, baadaye likaendeshwa tena kiujanjaujanja, lakini matokeo yake ndiyo tunayaona haya. Nianze kwanza kwa kuomba, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, kanuni 11 ambazo hujaziandika, ziandike haraka.

Kamati imeomba miezi sita, lakini naamini ukidhamiria, miezi mitatu itatosha kwa sababu kupitia ukosefu wa hizi kanuni ndiyo mianya ya ujanja ujanja inaendelea kuwapo. Hata zoezi lenyewe limekuwa *tinted* sana ni kwa sababu tu kanuni hizi hazijawa kamili. Umetengeneza tano, malizia na hizo 11 tuone kama *structure* ya kushughulikia hili jambo inaweza ikawa nzuri zaidi. Wale 16 mliowapa hawakuomba, tuombe tu hili suala la kuvirudisha tena hivi vitalu lifanyike mara moja. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji umekaribia kwisha)*

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, juzi niliomba muda kuongezwa kwa sababu hii hii, kwamba hujaanza kusema kengele tayari.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kilimo, huku kuna tatizo kubwa sana la ugawanyaji wa pembejeo. Pembejeo zinagawiwa nchini kwenye maeneo yanayostahili kwa kipindi kimoja nchi nzima. Huu ni uvivu tu wa kufikiri au wa utendaji miongoni mwa watumishi wa Wizara ya Kilimo. Kwa sababu nchi hii inayo misimu miwili ya kilimo. Wako wenye Vuli, wako wenye Masika. Ukikuta wenye Vuli na Masika, mbolea, pembejeo na mambo mengine vinapelekwa mwezi Novemba, Desemba wakati watu wanakaribia kuvuna mahindi. Buchosa ni *classic case*. Mbolea inapelekwa mwezi wa Novemba, mwezi Desemba ya nini wakati kule Kome Kisiwani watu tayari mahindi wanavuna? Matokeo yake ni wizi. Wananchi wanasainishwa zile vocha, wanapewa mbegu kwamba mtatumia msimu ujao, anasaini kwa ajili ya mbolea na dawa. Kwa hiyo, watu wanakwenda benki, wanachukua fedha ya Serikali wakati wananchi hawakunufaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilifikia mwaka jana, 2011 tukashauri, kama Serikali haiwezi kujipanga vizuri kugawanya hii mbolea kwa kipindi muafaka, basi waache kuliko kupeleka mbolea inakwenda kuporwa tu na watu wajanja huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu pamba. Pamba kwetu sisi wa Kanda ya Ziwa ni siasa. Ni siasa kabisa! Leo marobota 98,000 yako kwenye ma-*go-down* ya wanunuzi. Wanunuzi wote wa pamba *as we speak* hakuna hata mmoja aliyekwishapata *facility* ya benki kumwezesha kununua. Msimu uko miezi miwili ijayo au mwezi mmoja na nusu ujao. Tunafanyaje wakati huo njaa inatunyemelea kule, mvua haikuwa nzuri. Wakulima wangeuza pamba, wangenunua chakula. Sasa pamba hawatanunua, chakula hawana. Kama siyo *crisis*, maana yake nini? Halafu Serikali yetu itaanza kutukanwa kumbe kuna watu wanafanya uvivu uvivu.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotolewa, *stimulus package* imegawiwa kiujanja ujanja Benki Kuu, tumeomba jana kupitia mkutano wa wadau na Wabunge, iundwe Tume.

Mheshimiwa Spika, naomba iundwe Tume ikachunguze fedha hizo ziligawanywaje pale Benki Kuu. Kwa sababu jana tulikuwa hapo ndani Ukumbi wa Msekwa na wanunuzi wote wa pamba nchini.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kuiunga mkono hoja na vile vile niweke wazi kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na vile vile nilikuwa Mjumbe wa Kamati ndogo ambayo ilikuwa inafanya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, mengi tumeyazungumza katika taarifa yetu, lakini nilitaka nianze kwanza kwa kutoa nukuu ya mwanamahesabu mmoja anaitwa Albert Einstein anasema: *"Problems can not be solved by the same level of thinking that created them."* Wabunge wenzangu, kwa tafsiri isiyo rasmi sana, matatizo makubwa tuliyonayo leo hayawezi kutatuliwa kwa mtazamo wa fikra zile zile tulizokuwanazo wakati tunatengeneza au kuyasababisha hayo matatizo.

Mheshimiwa Spika, leo tunapokuwa wawakilishi wa wananchi, tunajadili na kuzungumza shida kubwa inayoikumba tasnia hii au Wizara hii, Wizara imewekwa kwa ajili ya kutatua tuliyonayo, lakini kwa bahati mbaya wale wanaokuwa wamepewa dhamana wanashindwa kuelewa wajibu wao ni nini.

Mheshimiwa Spika, nisingependa niende sana kwenye taarifa ambayo tumeitoa, lakini kwa sisi ambao tulipata nafasi ya kuzunguka karibu sehemu mbalimbali kwa ajili ya kufanya uchunguzi huu, tumeona kuna madudu mengi makubwa sana ambayo ikiwezekana Wabunge wengi tuweze kusoma katika taarifa kubwa ambayo tumeipata. Ningeomba kama Bunge, ningemsihi tushirikiane kwa pamoja tulinde rasilimali ambazo Taifa hili Mungu alitujalia.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tumeshindwa kabisa kutunza rasilimali ambazo Mungu alitupa, tumeshindwa kukusanya mapato ambayo tungeweza kuyapata kutokana na hizi rasilimali. Swali langu ambalo ningeweza nikauliza, nasikitika kwamba hata Waziri; Mimi ni Waziri Kivuli katika Wizara hii, lakini Waziri Mhusika simwoni tunapojadili mambo yanayohusu Wizara yake. Kwangu mimi naona kwamba hatilii maanani uzito mkubwa ambao upo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nasikitika tunapofanya mzaha na masuala muhimu kama haya katika Taifa letu. Wanyama tulionao ambao wanapotezwa hatuwatunzi, tutakuja kulaumiwa na vizazi vijavyo. Mfano mzuri, hata matatizo mengine ambayo hatujayaeleza hapa, kuna Mwekezaji mwingine ni Mwarabu, anapopita katika Uwanja wa Ndege

*(KIA)* hata taratibu hazifuatwi, anakuja na watu wake ndani ya ndege, anawalazimisha vijana wetu wa *Immigration* eti waingie kuchukua *Passport* za ma-*concubine* wake ndani ya Ndege halafu wakagongewe wapelekewe, taratibu ambazo hata kimataifa hazipo, na mmoja anaye-*initiate* masuala haya ni Mheshimiwa Kinana.

Mheshimiwa Spika, tumekuta vijana pale *KIA* wanalalamika kwa mambo kama haya, Taifa letu tunalipeleka wapi? Watu wamepewa dhamana, lakini hawataki kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Kambi ya Upinzani, nikimwuliza Waziri kama angekuwepo, kuna mambo mengi sana ambayo tulihoji. Tulihoji ugawaji wa vitalu, tulihoji wanyama kusafirishwa, wakamtoa kafara hapa Mbangwa mpaka leo hawajasema kama ana makosa au hana makosa. Watu wanasingiziana tu, hatujapata ripoti. Tulizungumza jinsi ambavyo akina Msekwa wanavyovuruga Ngorongoro, lakini majibu hayajatoka mpaka leo ni mwaka mmoja. *Where are we going*?

Mheshimiwa Spika, mwanafalsafa mmoja anasema *insanity is keep doing the same thing in the same way,* yaani uendawazimu ni kufanya jambo lile lile kwa njia ile ile huku ukitegemea matokeo tofauti. Tunasema yale yale, yanafanywa kwa namna ile ile, tunamaliza kodi za wananchi hapa, lakini hakuna kinachotokea. *Why*? Kwanini tupoteze muda wa wananchi, tupoteze kodi za wananchi hakuna kinachobadilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina matatizo makubwa. Ukienda kwenye misitu, kuna matatizo makubwa sana, misitu inakatwa ovyo, ukienda kwenye tasnia ya wanyama ni matatizo, kwenye utalii ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, nasikitika na nasikia Mawaziri wengine wanasema hawagomi. Nasema kama hamgomi, *tsunami* inakuja huko barabarani, mtaondoka kwa aibu. Ni lazima mjiuzulu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kwenda kwenye maonyesho ya kibiashara kule *Las Vegas* ambayo wengine waliongea maneno mengi zaidi, nadhani ripoti imewapa majibu hapa. Lakini ningeomba Ofisi ya Spika ifanye juhudi za maksudi Wabunge au Kamati hii ipate nafasi ya kutembelea vitalu kwa sababu tasnia hii ni muhimu kwa Taifa letu. Kamati hii iende kwenye vitalu mbalimbali katika nchi hii. Tulibahatika kukutana na waonyeshaji karibu 20,000 kule wanavyofanya kutoka katika Mataifa mbalimbali, tuliwakuta wengine kutoka Botswana, wengine Namibia lakini

wanyama wetu ni bora isipokuwa Watanzania hawana utalaam na hawajui ni namna gani hii biashara inafanywa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria hii kuwa nzuri, lakini kilichofanyika katika sheria ya kuwa-*empower* wazawa ni sawa na meli kubwa uilazimishe ikate kona kwa *90 degree.* Meli itaanguka! Hii biashara inahitaji watu wenye pesa kuifanya, ni biashara ambayo inahitaji utalaam mkubwa. Kwa hiyo, pamoja na sheria ya mwaka 2009 kuwa nzuri, ni lazima tuwafundishe watu wetu ni namna gani tunaweza tuka-*adopt*.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika ugawaji wa vitalu, pamoja na nia nzuri ambayo waliokuwepo mwanzo walitaka kuwa-*empower* wazawa namna na mbinu zilizotumika kuvigawanya hivi vitalu havikufuata utalaam. Kwa sababu walivigawa vitalu hivi vingi sana bila utalaam na vimeathiri ile *ecology* ya wanyama.

Kwa mfano, vitalu vimegawanyika sehemu nyingi sana. Ukiangalia, naomba ninukuu hapa: "Ugawaji huu haukuzingatia ukweli kuwa baadhi ya wanyama wenye maeneo husika wanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya kuweka himaya *(territory)*, kwa mfano Simba dume anahitaji zaidi ya kilomita za mraba 50 mpaka 100 kwa ajili ya ngome yake, lakini walipogawa hivi vitalu hawakuzingatia mambo hayo kwa namna moja au nyingine imekuwa ikiathiri wanyama, wamekuwa wakipungua. Kwa hiyo, utalaam haukuzingitiwa matokeo yake wanyama wanapungua badala ya kuongezeka." Kwa hiyo, tumejali biashara bila kuhifadhi. Biashara hii hata tulipokuwa kwenye maonyesho kule, inazingatia uwindaji, lakini kuhifadhi wanyama. Kwa hiyo, hili suala nalo halikuzingatiwa kama ilivyopaswa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi, wenzangu wamezungumza jinsi ambavyo Waziri hakuweza kuzingatia taratibu na kanuni ambazo zilikuwa zimewekwa. Kuna taabu kubwa sana, kuna watu ambao hawakuomba vitalu walipewa, kwa Mfano, akina Said Kawawa, akina Malagarasi hawalipi kodi, na nchi inaendeshwa kwa kodi. Lakini Waziri aliamua kuwapa. Huu ni ukiukwaji wa wazi kabisa ambao hauwezi kuvumiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mawaziri mliopewa dhamana, kama hamna vitendeakazi, mjiuzulu! Mwondoke, mwachie ngazi! *Leaders are suppose to solve problems*. Nchi hii, *the President is complaining, the Ministers are complaining*, *The Wabunge* tuna-*complain*, nani ata-*solve* tatizo? Wananchi wana-*complain*, tupo hapa kwa ajili ya ku-*solve* matatizo ya wananchi. Mtu ambaye yupo kwenye ofisi na hawezi ku-*deliver,* aachie ngazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitalu hivi viligawiwa bila utaratibu na hawa wengine hawakuomba halafu wakapewa, hii imeleta matatizo makubwa. Tunaingia katika shida ambayo haina sababu.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hotuba yangu ya mwaka jana, nilizungumza jinsi ambavyo wanyama wanavyouawa. Leo takwimu zinaonyesha wanyama wanakwisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba Tanzania ni nchi ya kwanza kwa vivutio Afrika na ni nchi ya tano kwa vivutio duniani na hii ni kwa mujibu wa *New York Times.* Gazeti la *New York Times* ni gazeti ambalo linaaminika sana Marekani na duniani kwa wafuatiliaji wa mambo. Lakini *privilege* hii haijatusaidia namna gani inachangia katika kukuza uchumi wetu, na kitu ambacho kingetusaidia kuondoa umasikini wa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii kama zilivyo sekta nyingine kama za Kilimo ambazo mbolea inakuja wakati mahindi yameshakua yapo kiunoni, kule kwetu tunaita mberewele na vitu kama hivyo, na Sekta ya Utalii nayo imefeli kwa sababu ya usimamiaji mbovu tulionao, kitu ambacho kinachangia kuongeza umaskini kwa watu wetu. Tunashindwa hata kusimamia *privilege* ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu, tuna vitu ambavyo sehemu nyingine duniani hawana, lakini tumekaa halafu tunawaachia watu kama akina Ahmed Kamran, *somebody a Pakistan by Nation*, ambaye anakuja hapa anakaa, anafanya anavyotaka, ana vibali vya kukamata wanyama, wakati sheria inakataza kwamba mgeni haruhusiwi.

Sasa kama huyu Ahmed Kamran amekuwa Mtanzania au ameshapewa Uraia? Inabidi labda Waziri wa Mambo ya Ndani naye aingie katika hili atuambie *status* ya Utaifa ya Bwana Ahmed Kamran kwa sababu Ahmed Kamran jina lake limejitokeza sana. Hatujui tunachokifanya, hatujui tunapokwenda isipokuwa wachache wanajua wanachokifanya na wanajua wanapokwenda na wameamua kwa dhati kutuingiza mkenge kama Taifa ili tuzidi kupotea, matokeo yake tunapoteza hela nyingi, tunashindwa hata kuhudumia watu wetu kwa madawa na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, mara tunakuja kusikia mambo ya makampuni sijui kampuni inakuja inaitwa *Jungle International*, mara *Jungle International Ltd*, mara Kampuni ya Utalii, mara humo humo unasoma unaambiwa ni Kampuni ya *Auction Mart,* kampuni ya mnada. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vitu vyote vinafanyika kwenye macho ya nani? Watu wanatoka huko wanakuja hapa nchini kwetu wanafanya vitu bila kuzingatia taratibu zetu za nchi. Unabeba twiga wawili wanapelekwa Ulaya. Twiga walivyokuwa warefu, twiga ni warefu kuliko ndege walipakia kwenye ndege gani hawa twiga? Watu watajiuliza! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, waling'oa viti vyote wakang'oa na *floor* ili kupata *height* nafikiri. Twiga wawili, tembo wanne, sijui wanyama gani, kila kitu ambacho kinafaa kubebeka na kisichofaa kubebeka watu wanabeba wanakwenda kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni hatari sana kwetu sisi kama Taifa kwa sababu Watanzania wa leo sio Watanzania wa mwaka sitini na ngapi, wa mwaka sijui enzi ya *Afro-Shirazi Party,* enzi za TANU na kadhalika.

Watanzania wa leo ni Wanzania wa CHADEMA, Watanzania wa Vyama vingi, Watanzania wanafuatilia kuangalia nchi inakwendaje na kwa hili kama Taifa *we are not happy.* Wananchi hawako *happy*, sisi Wabunge hatuko *happy.* Sasa ninyi kama Mawaziri mpo *happy* pamoja na *President* kazi inakuja kama alivyosema Mheshimiwa Msigwa, hata kama mnasema hamtajiuzulu, mtakwepa, sijui mtakomaa, hiki ni kimbunga, ni lazima kitakuja, kitawang'oa, na kimbunga hiki hiki kisipong'oa nyumba, basi kitang'oa angalau bati na bati katika hili ni Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hamna mchezo! Wananchi wameshakasirika, wananchi wanatuandikia meseji nzito, kama tungefuata mizuka ya wananchi, hasira za wananchi, sasa hivi humu ndani hivi viti tungekuwa tumeng'oa. Tunapata uchungu sana katika hili Bunge! Tungeng'oa hivi viti turushiane, lakini humu ndani tunajenga hoja, tunaongea, wakiondoka Mawaziri wanasema haina tatizo. Tena kuna tetesi wanasema kwamba wakubwa wengine wamewaambia wale Mawaziri kwamba tulieni tu msijali, huo ni upepo tu wa kisiasa, utapita. Huu upepo haupiti. Huu siyo upepo, hii ni dhoruba kwa manufaa ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema imefika wakati, uwe Waziri wa nini, kama umeshindwa kama alivyosema Mheshimiwa Mrema Lyatonga kaa pembeni, achia ngazi, tupo watu huku tunaweza

tukafanya kazi hata kama siyo Madaktari. Kama tunaweza tukatoa bajeti mbadala, japokuwa tupo Upinzani na bado Serikali ikaikubali kwa asilimia 99, ina maana sisi tunafaa kufanya kazi. Tumieni mawazo yetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunakuja na mawazo mapya. Baada ya hawa watu kuondoka, kila kitu kinatakiwa kiangaliwe upya ili kuhakikisha masuala mazima ya utalii yanaleta *revenues* zinazostahili kwa faida ya Taifa hili na siyo vingine. Katika hili sasa imefika wakati kama ni Waziri huyu atapenya au Waziri mwingine atakayekuja; kwanza hawa Mawaziri mimi nawaonea huruma sana. Nilikuwa najaribu kufuatilia utendaji wa Mawaziri, nasikia hawawezi hata kuidhinisha bajeti huko, ni Makatibu Wakuu ndiyo wana nguvu, wao hawana nguvu. Nasikia hawawezi kuidhinisha bajeti, hawawezi kufanya nini. Kuna Waziri pale nje akaniambia Mheshimiwa, *sometime* hata nikitaka kusafiri kuja Mbeya, Katibu akikasirika anaweza asinipe hela. Sasa ni kwa nini tunafanya hivi? Kwanini tusiwe na mfumo kama wa Marekani ambako kuna *Secretaries* tu, Makatibu Wakuu ndiyo Wafanyakazi, Mawaziri kwanza wao ni Wabunge, tubaki nao humu ndani tupelekane mchakamchaka kati ya Chama Tawala na Chama Pinzani?

Mheshimiwa Spika, iwapo sisi ndio tutakuwa Chama Tawala kama tunavyotarajia na kama Taifa linavyotarajia, na hata kama kesho mnaondoka na kuwa Chama Pinzani, tunakomaa kwa sababu moja. Siyo kama tunawapenda sana, hatutataka tuwe madarakani halafu tuwe na Chama legelege cha Upinzani. Ndiyo maana tunawanyoosha ili mtakapokuwa hata Chama Pinzani muwe Chama Pinzani makini kwa ajili ya kusogeza mbele hii nchi. Hatuko kwa maslahi yetu binafsi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa basi, Waziri atakayekuja, inabidi aangalie utalii wa nchi hii. Utajiri wa utalii umetawanyika, hauko tu Moshi na Arusha na wapi, waje waangalie kule kwetu Mbeya, Nyanda za Juu Kusini, tuna Selou, tuna Ruaha ambayo inakwenda mpaka Liwale huko, kule kwa Mheshimiwa Mtoto wa Mkulima Waziri Mkuu, kuna Katavi, hivi vyote haviwezi kusonga kama hatufungui miundombinu ikiwemo Uwanja wa Ndege.

Mheshimiwa Spika, juzi tuliambiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe Mbeya ambao tunaamini ndiyo utakuwa *hub* kubwa ya kimataifa kwa ajili ya utalii kwa maeneo yale. Tuliambiwa kwamba ule uwanja unafunguliwa tarehe 31 Machi, na mimi nikasema kwamba, sasa hivi jamani nitakuwa nasafiri kwa ndege ndugu zangu, mtakuwa mnanisindikiza Mbunge *Airport*, lakini mpaka leo tarehe 31 Machi imepita, uwanja mpaka leo hakuna kitu, hakuna kinachoendelea. Sasa kwa

taarifa, sisi tunauhitaji huu uwanja, ukiacha mambo ya biashara, mambo ya ajira na nini, tunauhitaji uwanja wa Kimataifa wa Songwe kwa ajili ya kukuza utalii kwenye maeneo yale kitu ambacho tunataka kiambatane na ukuzaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna maeneo kule mpaka Kitulo. Nenda kule Kitulo, kuna maua kule, kuna vipepeo, ukienda msimu kuna vipepeo wanaruka utasema maua yanatambaa angani. Nani anajua hapa? Hamjui kwa sababu hamtaki kutembea wala hamtaki kujifunza. Kuna mandhari kule ukiangalia unasema hii mandhari ingekuwa Uswiss, sijui hii nchi ingekuwa wapi! Maana yake sisi tupo goigoi, lakini angalia nchi mimi napenda kutoa mfano wa Uswiss, nchi kama Uswiss, ni kati ya nchi tajiri duniani, lakini sifa yake ni katika vitu vitatu; kutengeneza saa, kutengeneza visu na kutengeneza *chocolate*.

Hawa mabwana wanakuwa nchi tajiri duniani kwa kutengeneza *chocolate* wakati hawalimi *cocoa*, nchi yao ni ya milima ya barafu, hawalimi hata mchicha hawa mabwana, lakini leo hii wanakuwa maarufu na tajiri duniani kwa ajili ya kutengeneza *chocolate* wakati cocoa hailimwi kule, inalimwa Afrika, *Ivory Coast* na kule Mbeya kwetu Kyela wanalima cocoa pia. Lakini sisi tumekaa, hatuna masoko, hatuna nini, udongo wetu unaruhusu kufanya kilimo cha *organic*, soko la *organis* kule *lets say* maharage ya kawaida kama yanauzwa dola tatu kwa kilo, maharage *organic* yanaweza yakauzwa hata dola nane mpaka dola kumi.

Mheshimiwa Spika, tunafanya vipi ili kuchukua huu ufahamu na kuupeleka kwa wakulima wetu ili tuwasaidie wajikite katika masuala ya kulima mazao ya *organic* kwa faida ya kukuza kipato chao kwa sababu hiki kilimo kina *deal* sana?

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Ni kengele ya pili?

**SPIKA:** Ndiyo ni kengele ya pili.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nishukuru kwa kufunga, nasema mimi ni Mkatoliki, sitaki wauawe, mimi ninachotaka tu wafungwe. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mtaomba mwongozo baadaye jioni.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Muda umekwisha mtaniuliza jioni.

Waheshimiwa Wabunge tutakaporudi saa 11.00 jioni nitamwita Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Daktari William Mgimwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Wakati huo huo, ningependa kutangaza kuwa Mheshimiwa Daktari Pudensiana Kikwembe, amepata PhD yake kuhusiana na *Economics Population Resources and Environmental Economics* huko China Chuo Kikuu cha *Sichuan.* Kwa hiyo, tunampongeza na tunamtakia heri awezi kutumia hiyo digrii yake vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Pendenciana Kikwembe alisimama na kuonyesha ishara ya kushukuru kwa pongezi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge saa ya kuahirisha kikao imefika, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha Shughuli za Bunge mchana niliwataja Wabunge wafuatao kama ndio watakaochangia jioni. Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Ezekia Wenje na Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa nampongeza Mwenyekiti pamoja na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuisimamia Serikali. Natangulia kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kutamka wazi kwamba na mimi nilikuwa mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati Ndogo ya Uchunguzi, tuliotakiwa kuchunguza jinsi ya utaratibu wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii ulivyofanyika pamoja na utoroshwaji wa wanyamapori hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi ya kuzungumzia, lakini mimi labda nianze kuzungumzia vituko nilivyokutana navyo. Wakati tukiwa Arusha tulikwenda kukagua mazizi wanapowekwa wale wanyamapori wanapokuwa wamekatwa kutoka kwenye mapori, tukaenda kukagua kampuni moja inaitwa *Mountain Birds and Trophies Export Company.*

Mimi nilitegemea kupelekwa kwenye zizi, lakini nikaona tunaelekea kwenye *residential area* wanakoishi watu, tukapelekwa kwenye nyumba nzuri ya kifahari, geti kubwa, nyumba ya kisasa walipofungua mlango tukapokelewa na vinyonga, mijusi, kuingia sebuleni, kobe kila mahali, sasa tuko pale tunasikia kama watu wanaoga bafuni. Kufungua, yale makobe makubwa wako kwenye *bathtub* kufungua katika kila *drawer* katika nyumba ile kulikuwa na nyoka wa kila *size* na wa kila aina. Kutoka nje wanyama wote walio katika Tanzania hii wako kwenye maeneo yanayozunguka ile nyumba.

Sheria ya wanyamapori inasema, ukishawakamata wale wanyama kama unasafirisha, basi usikae nao zaidi ya miezi mitatu. Kuna kobe wana zaidi ya miaka nane wako pale. Wana-*incubetter* mle ndani wanazalisha kobe wanachukua mayai kule nje wanazalisha. Tumekuta wanyama zaidi ya 5000 pale. Kuna mnyama anaitwa Mindu ambayo ni *species* inapatikana Tanzania tu, lakini yule mtu anayo. Wanasema ni biashara ya Mtanzania fulani, tukawakuta na Wazungu wawili, eti wale Wazungu ni watalaam wa yule Mtanzania. Ndugu zangu najiuliza, Idara ya Wanyamapori Arusha hawana taarifa ya hicho kinaendelea? Ni sheria gani ambayo inaruhusu kwamba tufugie kobe ndani ya nyumba, ndani ya *bathtub? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna madudu mengi yanafanyika, lakini mnakumbuka wazi kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana alisitisha biashara ya kusafirisha nje wanyamapori hai kwa muda. Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri kabla ile biashara haijafunguliwa, tungefanya uchunguzi na *research* ya kina kuweza kujua faida tunayopata sisi Watanzania. Tumegundua kwamba Idara ya Wanyamapori kila mwaka wanatoa *quarter* kwa kila mfanyabiashara, kila mfanyabiashara anapata maelefu ya wanyama, anaruhusiwa akishapata wateja kule aje akamate na kupeleka nje. Je, hawa wanyama wote wakishapelekwa nje, hizo *zoo* za kule zikajaa, sisi tutaendelea kupata wateja? Watalii watakuja kufanya utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa vitalu vya uwindaji unasimamiwa na sheria Na. 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009 na madhumuni ya sheria hii ni uhifadhi, usimamizi, ulinzi na matumizi endelevu. Lakini tofauti na sheria iliyokuwepo ya mwaka 1974 sheria hii inataka sasa Watanzania wengi waweze kushiriki katika tasnia hii, ndio maana wanasema katika ugawaji wa vitalu vya kitalii, basi asilimia 85 ya vitalu hivyo viweze kugawiwa kwa Watanzania. Zoezi hili lilianza kwa kuundwa Kamati.

Kamati iliyoundwa ilikuwa nzuri, imesheheni watu waliobobea na wenye uzoefu na sifa za kutosha. Matatizo yalianza pale Sekretarieti ilipoanza kupokea na kufungua maombi tofauti na kilichotegemewa kwamba maombi hayo yangepelekwa yakafunguliwa mbele ya Kamati na wale waombaji wakawepo na hiyo labda ingepunguza malalamiko, kila mtu akahakikisha kwamba *documents* zake zimeweza kufika mbele ya Kamati. Kitendo hiki kilitia shaka kwa sababu ile Sekretarieti yenyewe imejaa wale watu ambao walikuwa wanalalamikiwa kwamba wanajihusisha na vitendo vya utoroshwaji nje wanyamapori. Hao hao ndio walifungua *documents* za watu. *(Makofi)*

Kamati ilikaa chini ikafanya ikafanya kazi, ikapendekeza kwamba hawa jamani pamoja na kwamba katika kuangalia hizi *documents* wengine wamepata mpaka maksi 50 lakini tulipokwenda kuwakagua tumekuta wako tayari, hawana vifaa, hawalipi kodi. Lakini Mheshimiwa Waziri akaenda akakaa ofisini kwake akaamua akachukua kampuni tatu ambazo hazina sifa akawapa vitalu, vingine vina madaraja mazuri zaidi, *grade one* mpaka *grade two*. Wakati kulikuwa na kampuni nyingine za Kitanzania ambazo zilikuwa na sifa. *(Makofi)*

Pili, kinyume na ushauri wa Kamati, Mheshimiwa Waziri akakaa ofisini akachukua makampuni 16 akayagawia vitalu, tofauti na ushauri uliokuwa umetolewa na Kamati. Sasa sisi tunajiuliza, Waziri alishawishiwa na nini ili akiuke utaratibu na ushauri wa Kamati iliyokuwepo kisheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utangazaji wenyewe wa vitalu, nani alipata vitalu, ulikuwa umegubikwa na usiri mkubwa. Kilichotangazwa ni kwamba, nyie mmepata vitalu, hakuna aliyeonyeshwa ni nani amepata kitalu gani. Kwa hiyo, iliwachelewesha watu waweze kupeleka malalamiko yao. Tendo la Waziri kuwagawia watu vitalu nje ya ushauri wa Kamati ilisababisha matatizo makubwa sana mpaka sasa hivi makampuni zaidi ya 30 walipeleka malalamiko wakaomba wafanyiwe *administrative review,* lakini kilichotushangaza ni viwanja, hata vile vitalu ambavyo tayari vina mikataba kama vya *TAWICO* vina mikataba ya muda mrefu, lakini

waliviweka mezani wakavigawa upya. Hata vile vitalu ambavyo havina wanyama na vyenyewe viliwekwa pale vikagawiwa. Lakini matokeo yake, vitalu tisa mpaka leo havikupata watu wa kuviomba. Hii inaonyesha kwamba Wizara haikuwa imefanya utafiti wa kutosha kujua vitalu ni vipi vya kugawa. *(Makofi)*

Waziri kwa kutambua kwamba alikuwa amefanya makosa, aliwaita waliopata na waliokosa akawakutanisha baada ya kuwa Kamati yetu imeshaanza uchunguzi. Tunajiuliza, alikuwakutanisha ili wafanye nini, kama si kutengeneza mazingira kwamba wale Watanzania wenye mitaji midogo waweze kuuza vitalu vyao kinyemela kwa matajiri ambao wana mitaji mikubwa? Tunaomba vyombo vya dola viendelee kuchunguza vione kama wale waliopata vitalu kweli ndio wanaendelea kumiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini malalamiko yalishafika kwenye meza pale Wizarani tangu Novemba, mwaka jana, 2011 na tangu Novemba, Desemba walishafanya hiyo *administrative review.* Kwa nini Waziri aliona kigugumizi kutangaza matokeo na alishashauriwa na Kamati? *(Makofi)*

Tunachosema, kwa kuwa zoezi hili limegubikwa na usiri mkubwa, harufu ya rushwa na ukiukwaji wa mapendekezo ya Kamati, basi tunaomba zoezi hili lirudiwe upya ili haki itendeke. Wasio na sifa wanyang'anywe wenye na sifa wapate haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tembo wanne limezungumzwa. Huyu aliyekuwa amesimamia hapa kama mwakilishi wa Pakistan, Ndugu Ahmed Kamran, barua alijiandikia mwenyewe, niliiona anaiandikia Wizara anasema mimi ndio mwakilishi wa Pakistan na Wizara ikakubali, ikaingia mkataba. Huo sio ubabaishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *Memorandum of Understanding (MOU)* iliyoingiwa, haina muhuri wa pande yoyote ile, hakuna barua ya maombi, hakuna barua ya kupokea. Kinachoshangaza Wizara hiyo hiyo ilimtuma tena Bwana Madehele aende Karachi eti kuangalia wale tembo wetu watafikia wapi? Wewe ukishampa mtu zawadi, unamtuma tena kwenda kuangalia hiyo zawadi atakwenda kuiweka wapi, jamani! Ninachosema, tulikuwa tunaangalia, haya yalikuwa ni makubaliano na mahusiano kati ya nchi mbili. Hatukuwa na barua yoyote ambayo inatoka Wizara ya Maliasili kuweza kupitia hata Wizara ya Mambo ya Nje, hatukuona mahali popote ambapo labda Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa alikuwepo wakati wanakabidhiana. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Bado!

**SPIKA:** Nasikitika dakika 10 ni kidogo sana. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Wenje.

**MHE EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa na mimi niweze kuchangia kwenye hii hoja ya muhimu kwa ajili ya nchi yetu. Napenda nichukue fursa hii kupongeza sana Kamati kwa kazi kubwa na kazi nzuri ambayo mmefanya ya kuhakikisha kwamba raslimali za Taifa letu zinalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia moja kwa moja, naomba nisome kifungu 51 cha Sheria Na. 5 ya Wanyama ya mwaka 2009, nafikiri jinsi ilivyo kwenye ukurasa wa 21 kwenye hii ripoti. Kifungu cha 51 wanasema: "Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwa idhini ya Waziri wa Maliasili na Utalii anaweza kutoa kibali cha kukamata mnyamapori, ambacho kitatoa masharti ya namna ya kumkamata kwa idhini ya Waziri." Hiyo ni namba moja. (c) Kifungu cha 58 kinamruhusu Mkurugenzi baada ya kupata ridhaa ya maandishi kwa Waziri. Naomba m-*note* kabla sijaanza kuchangia. Halafu 34 kifungu cha 11 kinasema: "*the minister shall ensure that any moderate or system used in allocation of hunting blocks is transparent and is line with principle of good governance."* Sasa hakuna mamlaka inayopatikana bila wajibu, na wajibu tulionao kama viongozi na hususan Mawaziri tuliona, ni kulinda rasilimali tulizonazo na kuhakikisha kwamba rasilimali zilizopo zinatumika kwa manufaa ya Watanzania walio wengi. Huo ndio wajibu wa msingi, eajibu mkubwa kuliko wote tulionao.

Sasa ukisoma hii ripoti, sisi Wabunge hatukuwepo kwenye hii Kamati, lakini tumeletewa na Wabunge waliokuwepo. Sisi tunatoa mchango *based on this report*. Hatuji hapa ku-*intimidate,* tuko hapa kwa ajili ya kusahihisha na kushauri ili hii nchi iende salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ripoti inasema kwamba namba moja alivyosema Mheshimiwa Mama Mushashu, hii ripoti inasema Mheshimiwa Waziri alishauriwa na Kamati kwamba kuna makampuni kadhaa ambayo yalikuwa hayana sifa ya kupewa vitalu, sasa hii *technical committee* ambayo inamshauri Waziri, Waziri amepuuza. Naye akaendelea akawapa hawa watu ambao hawana sifa *hunting blocks* wakati ameshauriwa na timu ya watalaam, yeye akapuuza. Sasa tukirudi kwenye matatizo mengi kwenye nchi, turudi kwenye *Dowans*, kwenye Richmond, yote tu Mawaziri walikuwa wanaamua tu, wanapuuza tu, wanashauriwa *with technical committee's* wao wanapuuza. Sasa tumefikia wakati,

iliyoanza leo, inakuja Richmond, mnazuia hii inakuja *Dowans*, mnazuia hii imekuja *EPA*, mnazuia hii imekuja Rada, mmezuia leo imekuja wanyamapori, mnazuia hii, mara Wizara ya Uchukuzi. Sasa sisi tumeshasema misamiati yote mpaka tumechoka na Watanzania wanaona na Watanzania wameelewa.

Mheshimiwa Spika, *role* yetu kama Wabunge wa kushauri Serikali, misamiati yote tumeshatumia, tumeshashauri mpaka sasa tunaishiwa nguvu. Kilichobaki ni kwamba Watanzania tunarudisha hii ngoma kwenu sasa nyie ndio mtoe ushauri huko tunakoelekea. Sisi sasa tunaelekea kushinda. Kwa sababu tunatoa ushauri kwenye masikio ambayo hayasikii, kila siku tunasema hapa majamaa hayaelewi, sasa sisi tufanye nini*? (Makofi/Kicheko)*

Sasa kama ripoti inaonyesha, mara anakuja mtu anaitwa Kamran, kila ripoti Kamran, *who is Kamran? Who the hell is he?* Yeye ni *elephant* gani nchi hii Kamran, Kamran mtu tu! Sheria inasema hakuna mtu *foreigner* ambaye anatakiwa apewe kibali cha kukamata wanyama. W*ho is he?* Yeye ni nani nchi hii huyu Kamran? Halafu *no body cares!* Hakuna mtu anayesema chochote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa stahili hii mpaka wanyama wamesafirishwa, kuna skendo nyingi kwenye hiki kitabu na nilisoma zile sheria kuonyesha kwamba nani ana mamlaka makubwa kwenye hii Wizara, Wizara ipo chini ya Waziri, sisi kama Wabunge hatumteui Katibu Mkuu wa Wizara, Katibu Mkuu *appointing authority* ni *President*.

Sisi Waziri anakuja hapa kwenye Bunge pamoja na kuwa yeye pia ameteuliwa na Rais, lakini Waziri ndio tunao uwezo wa kumshauri humu, Waziri tunaye uwezo wa kumwajibisha humu, ndio maana kwa stahili hii mimi nashindwa kuelewa nchi yetu. Mtu ukiuzulu, kwa mfano ukaamua kuachia, *defeat is not signoff failure,* ni fursa ya kuangalia changamoto unazopewa na kujipanga upya namna yaku-*face the future.* Lakini sasa Tanzania hapa tuna Mawaziri ambao hata wakikosea hawataki kukubali kwamba wamekosea, wanataka mpaka wakamatwe wavutwe kwa mguu kwamba toka! Sasa tunaelekea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii kwa kweli mimi imenishinda. Ninachosema ni hivi, nchi hii, sikilizeni Wabunge hii ni *serious.* Nchi hii tuna *system* ya Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa ninavyoamini inatakiwa iwe timu ya *professionals* ambao wako wanasheria, wawepo *all team.* Lakini wao sijui wanatusaidia nini?

Nchi hii wanyama wanaondoka kwa njia ya panya, walipiga *EPA* mabilioni kadhaa wakaondoka nayo, imekuja dili za Rada za ajabu, kila

aina ya ufisadi na uozo upo kwenye nchi hii. Hivi Usalama wa Taifa wanatusaidia nini? Wao kazi wanayofanya nchini, wanafanya *political intelligence* tu, hawaifanya *economical or social intelligence.* Usalama wa Taifa wanatusaidia nini kama Taifa? Sasa nao ni mzigo, kwa sababu ndio walikuwa wanatakiwa watusaidie mambo kama haya! Hii nchi inakwenda! Wanachukua mpaka kobe leo, wanachukua kila kitu! Mheshimiwa Sugu hapa alibaki anashangaa, hivi twiga utamsafirishaje? Sijui walimweka kwenye gunia, sijui waliweka kwenye buti ya ndege! Ni mazingira ambayo hayaeleweki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba, nchi ilipofika leo na kwa ushauri tunaotoa, Mheshimiwa Waziri Maige *is my good friend*, ni rafiki yangu sana, lakini na yeye naomba nimpe *free advice* kama ile niliyompa Mheshimiwa William Ngeleja. Mheshimiwa Daktari Augustine Mrema amesema kwamba hata yeye ilifikia wakati alijiuzulu. Hii *politics is about perception.* Sasa kama imeshawekwa *perception* kwamba kuna ujanja ujanja na madili yanapigwa, ni vigumu tena kwa Watanzania kuwa na imani na wewe kuendelea kusimamia Wizara nyeti kuwaongozea. Hizi Wizara ni ngumu, *is about perception.* Sasa *if this is the perception* ambayo imeshajengeka uki-st*ep down does not mean* kwamba ume-*fail*, hizi changamoto tunazowapa. Ni fursa ya kujipanga upya na kuangalia ulianguka wapi na uchukue *stock of your past* ili ujue una-*face* vipi *future*.

Kwa hiyo, sisi tunawapa ushauri wa bure na kama mtakataa walivyosema akina Sugu, sisi tutarudi kwa Watanzania kuwaambia kwamba, sisi tulisema hawa jamaa hawatusikilizi na kinachofuata sasa Mheshimiwa Ngeleja akifika Mwanza pigeni mayowe, jamaa akifika Mwanza pigeni mayowe ili turudishe nchi kwenye msingi wa utawala bora. Sasa kama hiyo *good governance* yenyewe ndiyo haijafuatwa hapa, kwa sababu huwezi ukashauriwa na timu ya watalaam halafu wewe unafanya kinyume. *Good governance and transparency* iko wapi? Ndio maana tunasema kwa wakati huu ulipofika, *there is a political tsunami is coming.* Wazee lazima muachie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kusimama katika Bunge lako Tukufu. Lakini la pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii. Mimi pia ni Mjumbe wa Kamati Ndogo iliyochunguza kadhia hii ya utoroshwaji wa wanyama pamoja na ugawaji wa vitalu vya uwindaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nijikite katika hadidu rejea ya tatu ambayo tulitakiwa tuchunguze ushiriki wa watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika biashara ya wanyamapori hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua nichangie hili kwa sababu ninajaribu kuonesha upana au uzito wa suala lililomo katika Serikali. Unaweza ukategemea pengine labda matatizo haya ni Mawaziri tu lakini inaonekana ni mfumo mzima wa Serikali kwa kweli haufai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiondoa Mawaziri leo lakini ukitazama watumishi kuanzia Katibu Mkuu mpaka kuja chini huku ukichunguza Wizara zote mimi naamini utakuta matatizo. La msingi ziundwe Kamati katika hali hiyo utaona tu hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wafanyakazi/watumishi wa Wizara hii kuna aina mbili, ushiriki wao unaweza ukautafuta. Kwa sababu kawaida shughuli za wanyamapori zinafanywa kwa kupitia kampuni. Kwa hiyo, kampuni utazikuta usajili wake upo *BRELA* sasa tulipochunguza suala hili tulipokwenda *BRELA* hatukukuta majina ya wafanyakazi wa Idara ya Wanyamapori katika kampuni hizo. Lakini hii kwangu mimi kwa kweli naona haiondoi fikra na imani kwa kweli kwa wafanyakazi au watumishi wa Wizara hii hawashiriki katika biashara hizi. Hili utalikuta katika haya mambo ambayo yanafanywa utaona lazima hapa mfanyakazi kashiriki au mtumishi kashiriki kwa maslahi yake.

Mheshimiwa Spika, tuanze mwaka 2009 ambapo kila Mbunge ameshaelewa kuwa mwaka 2009 Wizara kwa kupitia Mkurugenzi aliyepita waliingia mkataba wa makubaliano na Ahmed Kamran. Sasa Mkurugenzi yule hatukujua sisi wale tembo wanne aliwapata wapi hata ikabidi awape Jiji la Karachi. Kwa sababu kama inavyoelezwa kuwa hakuna ombi kutoka Jiji la Karachi – Pakistan kuwa walihitaji tembo wanne. Kwa hiyo, kwangu mimi kutokuwepo ombi la kuomba lile kuiomba Serikali naamini kulikuwa na mazungumzo binafsi baina ya Mkurugenzi ndugu Tarimo wakati huo na Ahmed Kamran.

Kwa hiyo, kwangu mimi hilo tendo ni kuwa mfanyakazi kashiriki au mtumishi kashiriki katika biashara hii. Kwa hiyo, imani yangu mimi licha ya kuwa hawamo katika makampuni kwa sababu hakuna mtu ambaye ataanzisha kampuni katika Wizara ile kwa hiyo, hilo mimi nasema nina imani kabisa kuwa wafanyakazi/watumishi wanashiriki katika biashara hii moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine mwaka 2009 Ahmed Kamran alikutwa na *trappers card* yaani aende akakamate wanyama. Kwa

mujibu wa kifungu cha 80(2) cha Sheria ya Wanyamapori anayetakiwa kushiriki katika biashara ya wanyamapori hai ni raia wa Tanzania. Sidhani kama huyu afsa aliyetoa kibali hiki haielewi sheria hii. Lakini kwa msingi ule ule wa kuwa anashiriki katika biashara hii akampa kibali cha kukamata wanyama *(trappers card)* Ahmed Kamran huku akijua hakika huyu si raia wa nchi. Kwa hiyo, hili la pili kwangu mimi kwa kweli inanithibitishia kuwa kuna ushiriki mkubwa wa watumishi wa Serikali katika Wizara hii katika suala zima la biashara ya wanyamapori hai.

Mheshimiwa Spika, suala lingine mwaka 2010 kulisafirishwa twiga wawili pamoja na wanyama wengine wakiwemo viboko wawili, kudu wawili na *eland* wawili, hapa ni kesi kama iliyokuwa ya mwaka 2009 kuwa bado hakukuwa na ombi lakini bado wanyama hawa walitolewa. Kwa hiyo, naamini mimi katika suala hili bado wafanyakazi nasema tena wameshiriki na wanashiriki katika biashara hii na hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshiimwa Spika, lakini twende mwaka 2011 ambapo kulikuwa na barua ya tarehe 26 mwezi wa nne mwaka 2011 nayo hii *Jungle International* haikuomba wanyama kwa hiyo, ilipopewa wanyama ina maana ilikuwaje wakapewa wanyama bado inarudi pale pale halafu nililoligundua lingine panapotokea jambo lolote la kuvunja sheria basi wanaosaini barua zile ni kwa niaba ya Katibu Mkuu, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mwaka 2011 alipoingia ndugu Mohamed Madehele, mwaka 2010 alikuwepo ndugu anaitwa Midala, inaonekana ni mpango maalum unapangwa wewe tia saini mimi niko nyuma yako, mimi ndio tafsiri yangu kwa kweli. Kwa hiyo, hatuwezi tukaenda hivi na nasema tena hii nina imani Serikali ikichunguza Wizara zote tutakuta madudu kama haya watendaji wanafanya. Kwa hiyo, tunasema Mawaziri waondoke sawa, lakini tuone kama Wabunge/Bunge kutaka kusimamia Serikali basi twende chini zaidi. Kamati ziundwe ili kuchunguza na kuisafisha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine linalonithibitishia mimi kuwa wanashiriki katika biashara hizi watumishi wa Serikali ni kuwa hawa wafanyabiashara wa wanyamapori hai wanaomba leseni, baadaye wanapewa ugavi wa wanyama kwa mujibu ya aina ya wanyama ambao wanagawia ambao unaitwa *quota*.

Tulichokigundua ni kuwa kuna baadhi ya kampuni *quota* zao zinabakia Wizarani *Jungle International, Ham Marketing* tumegundua hili, wakati unapopewa wewe mfanyabiashara ile *quota* ni yako. Iweje leo ibaki Wizarani? Wana mtindo wanaita wenyewe kukatia, yaani

akishapatikana mteja huko basi wanatoa barua ili kuwapunguzia wale wanyama. Kwa hiyo, hii inadhihirisha vilevile kuwa suala hili kwa kweli watumishi wa Serikali wanashiriki.

Mheshimiwa Spika, tulipokwenda Arusha, Mheshimiwa Mushashu kaeleza inaonekana katika biashara hii ya wanyamapori Watanzania wanawekwa kama kimbele mbele lakini ukweli wa mambo wengi wao wanatumiwa.

Tulipokwenda *Mountain Bug* yalionekana Mheshimiwa Mushashu ameshaeleza lakini pale tukakuta wafanyakazi wananung'unika, alinijia mfanyakazi wa kike kwa kunong'ona maslahi yao madogo lakini usije ukasema wakanijua kuwa ni mimi. Sasa nikamuona pale hawa ambao wanaambiwa kuwa ni kiongozi wale wazungu wanaambiwa ni madaktari, sijui watalaam, sijui washauri, nikaamibiwa huyu mhusika wa kwanza Mtanzania mwenzetu hayupo anakuja lakini yupo Mtanzania mwenzetu mwingine pale mimi nikachukulia kuwa ni msaidizi nikanong'ona nikaambiwa mbona huyu jamaa Watanzania wanamlipa kwa malipo madogo, akaniambia Mheshimiwa hilo ndio tatizo letu. Kwa kweli nikashangaa yule ambaye ndio msaidizi naye anasikitika vilevile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inaonyesha wale wanaobabaisha kuwa ni madaktari wale ndio wenyewe hasa. Sasa hili lipo kwa Watanzania wanatumiwa katika biashara hii lakini wao hawafaidiki kiasi hicho. Kwa hiyo, inaonekana kuwa kuna ujanja unatumika katika suala zima la biashara hii kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, nikirudi huku nyuma tulimhoji Ndugu Tarimo kuhusiana na mkataba ule ambao ameingia na Ahmed Kamran yeye alikataa katakata akasema hamtambui huyu wakati kuna mkataba. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwa taarifa mbili zilizotolewa leo asubuhi. Lakini pili ningependa kuwapongeza sana Wenyeviti wote wa Kamati hizi mbili kwa kuwasilisha taarifa zao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza Bunge hili kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na ningependa kuchangia zaidi katika eneo hili. Wote tunafahamu umuhimu wa kilimo katika nchi yetu na umuhimu huu haukuanza leo wala jana. Toka tupate Uhuru kilimo

kimepewa kipaumbele na kilipewa kauli mbiu mbalimbali, kimeitwa kwa majina tofauti kwa wakati tofauti, kwanza kiliitwa kilimo ni uti wa mgongo kwa kutambua kwamba kinaajiri watu wengi sana hapa nchini asilimia 80 ya Watanzania na kinazalisha chakula cha kutosha kwa hiyo *food security* na kinatoa ajira vilevile. Baadaye kikaitwa kilimo cha kufa na kupona maana yake vyovyote vile iwavyo kilimo lazima kipewe umuhimu wake. Baadaye kikaitwa siasa ni kilimo na leo hii tupo na kauli mbiu nyingine kilimo kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika kauli zote hizi zilizotamkwa zote zilikuwa zinaonyesha umuhimu wa kilimo katika kuchangia katika Pato la Taifa kutoa ajira na kujitosheleza kwa chakula. Kilimo mpaka sasa kinachangia na kinakua kwa asilimia 4.2 tu kiasi ambacho hakitoshelezi kuinua uchumi wetu katika nchi yetu. Nini kilichotokea?

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo linajitokeza wazi ni kwamba hatujawekeza vya kutosha katika sekta hii ya kilimo. Mwenyezi Mungu ametupa rasilimali kubwa katika nchi hii hata katika maeneo ya maliasili pamoja na utalii lakini hatujavuna na kutumia hizo rasilimali inavyotakiwa, vivyo hivyo kwenye kilimo. Nchi za Umoja wa Afrika Kusini walikubaliana kwamba kila Serikali ijitahidi kuweka angalau asilimia 10 ya pato ghafi la Taifa ili kilimo kiweze kuchangia zaidi katika uchumi wa nchi hii. Sisi Tanzania kwa sasa hivi tunatenga takribani kiasi cha asilimia 6.5 tu kwa hiyo na mchango wa kilimo umezidi kushuka kutoka ilivyokuwa huko nyuma ikichangia karibu asilimia 40 leo hii kilimo kinachangia takribani asilimia 25 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna rasilimali ardhi kubwa sana. Tunalo eneo la hekta milioni 44 ambalo linafaa kwa kilimo yaani *arable land.* Lakini kiasi ambacho tunalima ni hekta milioni 10 tu sawa na asilimia 24 au 23.5 eneo lililo kubwa bado mpaka leo hii halijatumika ipasavyo. Halijatumika ipasavyo kwa sababu hatuna mipango mikakati ya kilimo yaani *Agriculture Development Master Plan* hatuna. Kwa hiyo, kila wakati tunakuja na mpango huu wakati mwingine tunakuja na mpango huu, mipango ambayo haioani pamoja ili kuweza kuleta tija zaidi katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ambacho tumekiwekea kipaumbele sana tunalo eneo la hekta milioni 29.4 hapa nchini ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Lakini eneo linalolimwa kwa umwagiliaji ni hekta 344.4 tu chini ya asilimia moja ya eneo ambalo lipo yaani *the potential area.* Yote haya kama yangewekwa na tukawekeza kamili katika maeneo haya ikiwa ni pamoja na utalaam wa kisasa wa *drip irrigation,* mimi nina hakika mchango wa kilimo ungekuwa ni mkubwa

zaidi kuliko ilivyo sasa. Ni mategemeo yangu kwamba baada ya kuanza na kilimo kwanza bila shaka tutasukuma tutapiga hatua ili kusudi kilimo kiweze kuchangia zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni upande wa mifugo, tumeshaeleza rasilimali mifugo tuliyonayo kwamba ni kubwa, Tanzania ina ng'ombe wengi, ni nchi ya tatu baada ya Ethiopia na Sudan lakini mchango wake umekuwa ni kidogo sana nako hatukuwekeza vya kutosha lakini Bunge hili limepitisha Sheria ya Utafiti, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo hapa nchini. Ni imani yangu kwamba baada ya kuanzisha taasisi hii na wakaweka bodi ambayo kweli inaweza kufanya kazi kwa kuchukua watu ambao wana muono wa mbali nina hakika mifugo yetu itabadilika, itakuwa na tija zaidi na mchango wake utakuwa mkubwa kuliko sasa ambapo inachangia asilimia 3.8 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo tumesikia kwa Mwenyekiti wa Kamati asubuhi akieleza matatizo yaliyopo kwenye Mkoa wa Kagera ambako wavamizi kutoka nchi za jirani wanaingia na mifugo kule kwenye ranchi, vile vitalu vina matatizo lakini vilevile kwenye ripoti hiyo tumeambiwa hata Wenyeviti wa Vijiji katika maeneo hayo wengine ni wageni wa kutoka nchi za jirani na tunashauri Serikali ifuatilie jambo hili ili kusudi iweze kuwatambua nani raia wa kweli ama wengine.

Kwa upande wa uvuvi imeshatolewa taarifa hapa kwamba samaki wetu katika maji baridi wanazidi kupungua siku hadi siku na yote hii imetokana na uvuvi haramu na hivyo kwa sasa hivi samaki hawatoshi. Kwa hiyo, inapendekezwa kwamba ufugaji wa samaki upewe kipaumbele na hususan *aquaculture* ili kusudi tuweze kuwa na samaki wengi na watu waweze kunufaika kutokana na hao samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mengi ambayo Mwenyekiti alieleza asubuhi juu ya kuendeleza sekta ya mifugo na matatizo mbalimbali yaliyopo, mimi nafikiri Serikali ijipange iweze kuwekeza vya kutosha katika sekta hii ambayo inaajiri watu wengi ambayo inatupa chakula cha kutosha ili kusudi iweze kuchangia zaidi katika Pato la Taifa la nchi yetu hususan ukiangalia kwamba kuna miradi mingine ambayo imekwishaanza kama *SAGCOT* ambayo kama mipango yake ikianza kutekelezwa vizuri nina hakika mchango wa sekta ya kilimo utakuwa ni mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache napenda kushukuru na naomba kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika taarifa hizi za Kamati. Awali ya yote niwapongeze Wenyeviti wa Kamati wote ambao wameweza kuwasilisha vizuri taarifa zao. Lakini mimi nitachangia katika Wizara tatu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia naomba uniruhusu ninukuu dua ambayo tunaiomba kila siku asubuhi katika Bunge hili Tukufu tunapoanza kipindi chetu cha Bunge. Katika ukurasa wa 22 wa Kanuni zetu inasema; "Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu, utuongezee hekima na busara sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utupe uwezo wa kujadili kwa dhati mambo yatakayoletwa mbele yetu leo ili tufanye maamuzi sahihi yenye manufaa kwa watu wote na kwa ustawi wa nchi yetu. Amina." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimependa kunukuu maombi haya katika Kanuni hizi kwa sababu moja tu, nayo ni kwamba tunaposema Waziri Mkuu ajiuzulu ni maamuzi sahihi kabisa na Wabunge tunaanza na maombi haya kila asubuhi, hatujakosea kutoa mapendekezo hayo. Mimi naomba yaendelee kuzingatiwa na niendelee kuomba Wabunge upande wa pili ambao wao wanafikiri kwamba kuungana na sisi wanaungana na wapinzani, waache tafakuri hiyo, waungane na Wabunge wote tuiwajibishe Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya maombi Mungu anayasikia, kama hatutasimamia Serikali hii na kama hatutamwajibisha Waziri Mkuu mambo hayatakwenda. Nilikuwa nasikiliza hotuba zilizopita, lakini pia nilikuwa naangalia kwamba, katika hotuba hizo labda tutapata Wizara moja ambayo ni nafuu. Katika Wizara zote zilizoguswa hakuna Wizara ambayo haivuji , kila Wizara kuna matatizo. Kwa nini Waziri Mkuu asiwajibishwe na Mawaziri wake?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili naona katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG)* walisamehe mirahaba, zile fedha ambazo walitakiwa wakusanye kutoka kwenye uvunaji wa misitu milioni 800 wamezisamehe, Waziri anafahamu hilo. Lakini wakati huo huo Wizara hii ndiyo inaongoza kwa madudu haya ambayo siku ya leo tumeona kutoka kwenye Kamati. Ni kwa nini Wabunge tusifanye maamuzi sahihi kwa mujibu wa dua tunayoiomba kila siku asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kampuni ya *Jungle International* ambayo iliomba kusafirisha hawa twiga wawili, nilikuwa nikisoma ripoti ya Kamati wameeleza vizuri. Kampuni yenyewe haikuomba, lakini Wizara ikawaandikia barua, hawa twiga wakachukuliwa. Lakini pia kibali

kilichotolewa, kimetolewa nje ya utaratibu, kibali hakitakiwi huyo mwindaji awinde katika Wilaya tatu, imetolewa Wilaya ya Monduli, Simanjiro na nyingine. Wamekwenda wametafuta hao twiga. Lakini ukifanya *tracking* kwenye ripoti hii hao twiga wala hawajasafirishwa nje ya nchi, wamepelekwa Shinyanga hapo.

Mheshimiwa Spika, ripoti inaonesha kwenye *zoo.* Hii nchi tunaipeleka wapi? Hii nchi tunaipeleka wapi kwa hali hii? Kodi hazikusanywi, vitalu vinagawiwa hovyo hovyo, lakini pia hakuna usimamizi wa rasilimali za Serikali. Kama Serikali imeshindwa kusimamia rasilimali hizi ni bora warudishe kwa wananchi nchi yao, chukueni jamani sisi tumeshindwa kuliko madudu haya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaopakana na hifadhi hizi wanapata adhabu nyingi sana. Wanapata matatizo mengi sana. Nitoe mfano hifadhi ya Tarangire, vijiji vya Gijedabug vinavyopakana na Hifadhi ya Tarangire, Mheshimiwa Waziri kila siku naongea naye, wale wananchi wameondoka kwenye Vijiji vile vitatu, Ayamango, Gijedabug, Gedamar. Kila siku wanahangaika vijiji vitatu, kaya 245 hifadhi imechukua maeneo yao hawapewi ni mwaka wa nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ni Watanzania waliowapa ridhaa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini kwa hali kama hii wale wananchi mpaka leo, nimekwenda kwa Mkuu wa Wilaya wanasema wamepewa shamba la *Gallapo Estate,* nikaenda kwa Waziri. Lakini wanasema wamepewa shamba la Hanadeko liko Babati Mjini wananchi wako Babati Vijijini. Hifadhi ya Tarangire imechukua maeneo yao, lakini wanazungushwa, tuliona kwenye magazeti wiki iliyopita, yameandikwa, wananchi wanakwenda kuishtaki Halmashauri, Halmashauri matatani Babati. Kaya 245, lakini hifadhi hizi bora zingekuwa zinawasaidia wananchi. Baada ya maeneo ya wananchi kuchukuliwa hawa wanyama wangesaidia Taifa, wanyama hawasaidii Taifa, wananchi maeneo yao yanachukuliwa, lakini madudu yanafanyika. Bado sisi tunasema kwamba Serikali hii ni makini, hapana. Watanzania wanatusikia, tumechoka na madudu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka niende Wizara ya Ardhi. Kati ya Wizara ambazo zina uozo ni Wizara ya Ardhi. Tumesoma kwenye ripoti kwamba ekari moja inakodishwa kwa wawekezaji shilingi 220 kwa heka, hii ni aibu. Mia mbili ishirini, wawekezaji shilingi 220 wanalipa kwenye Serikali kwa mwaka kwa eka. Watanzania wengi wanahangaika kwani Watanzania wengi hawana maeneo. Kamati imekwenda ikaangalia migogoro ya ardhi, lakini sana sana walikwenda kuangalia pesa zinazotolewa na Wizara kwenda katika Halmashauri katika suala zima la

upimaji. Lakini wamesema pia hata hizo pesa zinazotolewa na Serikali hazirudishwi Wizarani ili zitolewe kwa Halmashauri zingine.

Mheshimiwa Spika, siyo hayo tu, niombe Kamati kama kuna kazi ya kuifanya ni katika Wizara hii ya Ardhi. Wizara ya Ardhi huko kwenye Halmashauri zetu, Maafisa wa Ardhi wao wamejifanya ni Miungu watu. Maafisa wa Ardhi wao ndiyo wanajinufaisha na rasilimali za ardhi, upimaji shirikishi haupo. Mashamba yame-*expire. (Makofi)*

Nimeshaongea sana katika Bunge hili. Nikupe mfano mzuri, katika Mkoa wa Manyara kuna matatizo mengi ya ardhi. Lakini angalia mashamba tuliyonayo kuna shamba la *Sigino Estate* lililoko Wilaya ya Babati. Hilo shamba vijiji vitano kila siku wanahitaji kupewa lile shamba lilikuwa chini ya *Breweries.* Hilo shamba sasa hivi limeuzwa kwa mtu binafsi Halmashauri haifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vya Endasago**,** Sigino na Arri, wanatafuta hilo shamba haliko *Breweries,* limeuzwa wananchi hawajui, Halmashauri hawajui, lakini kuna Wizara, kuna Maafisa wa Ardhi, hii nchi tunaipeleka wapi? Tunaongea kwa uchungu. Nilikuwa naongea na Wabunge wenzangu kwamba hivi unapochangia unashika wapi? Huku kunavuja, huku panavuja, huku panavuja. Fanyeni *overhaul,* nyumba ikianza kuvuja, mfanye *overhaul service*, Serikali nzima panavuja, kila Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shamba la *RIVACU*, ekari zaidi ya 3,000, wananchi wanahangaika mpaka vijiji vya Endasago Babati, wananchi hawapewi. Mashamba ya *NAFCO* wananchi hawapewi. Lakini wawekezaji wanalipa shilingi 200. Hii ni aibu, *it is shame for our nation.* Tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee Wizara ya Maji. Nilikuwa naangalia ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, milioni 58 hazikupelekwa Wizara ya Maji. Lakini nizungumzie miradi ambayo imezungumzwa katika Kamati hii, miradi ya *World Bank.* Nilikuwa naongea na ma-*Engineer* wa Maji wa Halmashauri. Jamani hiyo miradi haitekelezwi ya vile vijiji 10, tena cha kusikitisha sasa hivi wamepunguza kutoka vijiji 10, wanaelekea sasa vijiji sita. Serikali haipeleki hata fedha.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi? Hii nchi tunaipeleka wapi? Ni kwa nini kama Serikali imeshindwa kuongoza nchi hii na wasio wazalendo waseme tu kwamba, mambo hayaendi. Miongoni mwa maswali mengi yanayoongoza katika Bunge hili ni maswali ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Kiufupi nitazungumza mambo matano. La kwanza, nitazungumza hali halisi ya takwimu ya kilimo katika nchi hii. La pili, nitazungumza kwa ufupi juu ya uwezeshaji. La tatu, huduma za fedha zilivyo na uhusiano na umaskini tulionao na la tano, nitazungumza ninavyoona juu ya nini kinahitaji kwa ajili ya *an effective Government.*

Mheshimiwa Spika, mpaka dakika hii katika miaka 10 kuanzia 2000 mpaka 2010 kilimo kimekuwa kwa wastani wa asilimia 4.3 katika miaka kumi. Lakini *percentage* ya *share to GDP* imepungua kutoka iliyokuwa 29.1 mwaka 2000 mpaka sasa ni 24.1 ya *percentage* ya *GDP.* Takwimu hizi zinakubalika ikiwa uchumi ulikuwa katika sekta zingine ambazo nazo zinaongeza mapato na kuongeza *employment.* Lakini ukitazama sekta kubwa ya msingi sekta ya viwanda ilikuwa sana, sekta ndogo ya *construction* na *finance*. Lakini haziajiri watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo ukuaji mdogo wa kilimo umekuwa na hitilafu na wenye hasara katika uchumi. Kwa sababu ulikuwa unateremka badala ya kuleta mbadala kukua kwa upande wa viwanda. Pili, ukitazama mazao ambayo tumekuwa tukilima kutoka mwaka 2000 mpaka sasa 2010, takwimu zinatuonesha kwamba mwaka *2000 percentage share to GDP* ya mazao ilikuwa *69.5 percent.* Lakini mpaka mwaka huu 2010, mwaka uliopita ilipanda kwa *only 00.4 percent* maana yake kufikia *69.9 percent*. Huu ni ukuaji ulio mdogo kwa sababu upande wa sekta zingine zilikuwa zinakua ambazo haziongezi *employment.*

Suala la pili, ni suala la uwezeshaji. Nitazungumza kidogo suala la kilimo kwanza. Kama walivyozungumza waliopita, kilimo kwanza kimekuja kama Sera mbadala ili kuhakikisha kwamba tunaongeza *efficiency* ya kilimo na kuongeza *rate* ya *employment* katika *population.* Lakini kilimo kwanza kilitaja mambo ya msingi. La kwanza, kilisema lazima tuwe na kilimo cha kisayansi. Mpaka dakika hii hatuna kilimo cha kisayansi ambacho kinatumia teknolojia ya kisasa. Tumekuwa tukipeleka mbolea na pembejeo ambazo tayari walio wengi wameshaeleza kwamba zina matatizo makubwa na kwa ukweli hakuna *impact* katika kilimo. *(Makofi)*

La tatu, kilimo kwanza kilikuwa kina-*advocate* kwamba tuongeze bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji, ku-*target* eka milioni saba, lakini kilichofikia sasa hivi hakuna. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba. tuna mpaka eka 29.4 milioni ambazo tungeweza tukamwagilia,

lakini bado hatuoneshi *effort* ya kwamba tuna mkakati kuelekea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kilimo kwanza kilieleza kwanza, kwamba Wakuu wote wa Mikoa pamoja na Wilaya wahakikishe kwamba wanatenga ardhi ambayo ardhi hiyo itakuwa kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo. Hilo liliamuliwa kutoka 2009 mpaka leo hii sera hiyo bado ni goigoi na hatujafika mahali popote kuona kwamba tumetenga ardhi kiwango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine lililoamuliwa katika kilimo kwanza ni kwamba, wale Maafisa Ugani, *Agriculture Officers* kila Wilaya wawezeshwe na wawe na mashamba ya mfano ili wananchi waweze kujifunza kimfano na katika hali hiyo baada ya kujifunza na wenyewe walime kilimo cha kisayansi kutokana na mifano inayooneshwa na vijana wa ugavi. Hakuna mambo yanayofanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na sera zinaeleza mazuri, lakini hakuna utekelezaji. Katika upande wa uwezeshaji mwingine nchi hii tunaagiza mafuta ya chakula na tunatumia jumla ya mafuta ya chakula takriban tani laki tatu na tuna-*import almost 55 perc*ent ya tani laki tatu kwa ajili ya kula mafuta. Lakini pesa hizo nyingi tunatumia hela za kigeni wakati nchi hii ina mazao ambayo tungeweza tuka-*process* tukapata mafuta hayo hayo. Tuna mazao ya pamba, tuna alizeti, tuna mawese, hayo yote tungeweza tukaweka *agro based* industries katika nchi hii na ku-*process* na tukaepuka *misuse* ya *foreign exchange* ambayo tuna-*import* kitu ambacho tungeweza tukalima hapa nchini.

Ya nne, suala la uhusiano wa kutotumia huduma za fedha ili ziweze zikarahisisha kuboresha kilimo vijijini. La kwanza, *only 12.4 percent* ya wananchi wa nchi hii wako na *access* kwenye *formal financial services.* Kwa hiyo, *impact* kwenye kilimo hamna. Asilimia *56 they have no access at all to financial services* ya *population* ya nchi hii na *only three percent* ya *rural population* wana *access to financial services. Only three percent,* sasa utaona kwamba *impact* ya *financial intimidation* kwenye *rural sector* haipo. Tukiendelea namna hii *financial deepening is so poor* katika *East Africa, we are the last.* Ukiacha Kenya inaongoza, *Uganda is better* kuliko sisi. Sisi tuko last kwa sababu *access to financial services to the rural population is only three percent.*

Mheshimiwa Spika, sasa tunahitaji mkakati wa kufungua *microfinance* ambazo zinalenga kupeleka huduma hii vijijini ili tuunganishe huduma ya fedha na uzalishaji kiuchumi katika *rural sector.* Nashauri yafuatayo kwa sababu kengele imeshagonga, nangojea

kengele ya pili. Tunahitaji utekelezaji wa Serikali ambayo itakuwa *committed* kwa sababu haya yote yanajulikana, *we need a committed Government* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaelekea huko kwenye mafanikio.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, *we need an accountable Government,* Serikali ambayo inawajibika. Unaweza kuwa *committed but you are not accountable,* tunahitaji Serikali inayowajibika. La mwisho, hatuwezi kuwa na Serikali inayowajibika isiyo na viwango vya utekelezaji. *We need performance measures* kwa *all Ministers* na *Chief Executives* wa *Institutions* za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mwisho wa mwaka tuone kwamba nani alifanya nini na alifanya kwa kiwango gani? Je, kile alichofanya ndicho kinachokidhi *performanc*e ya Serikali. Bila *performance measures*, bila *performance indicators, we don't go anywhere*. Huu uwe wakati wa kuanza upya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Mimi nitazungumzia Kilimo, Mifugo, Maji, Uvuvi na Ushirika.

**SPIKA:** Dakika ni kumi tu.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, kilimo kwa maana ya nchi hii, tunasema ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa kwa maana kwamba ndiyo kinachukua ajira kubwa sana ya Watanzania walio wengi. Lakini Serikali kama Serikali bado haijatilia maanani namna ya kuboresha kilimo katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imetamkwa kwamba, hekta 29 milioni zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini ni eneo dogo tu ambalo mpaka sasa linalimwa. Huwezi kuamini Watanzania wapo wengi ambao wanajitahidi kwa kila namna kuendeleza maeneo hayo ya kilimo cha umwagiliaji, lakini ni kwa shida mno. Hawa wananchi wanapoamua kwamba sasa eneo fulani waliendeleze kwa kilimo, taratibu sijui mpaka akaombe kibali wapi, akafanye nini, wakati bado kuna hekta 29 milioni hazijaendelezwa. Sasa hivi vikwazo tunavyoviweka je, tutafika kwenye hizo hekta milioni 29? Kwa uzoefu kule Mbarali wananchi wanajitahidi sana katika kilimo cha umwagiliaji, lakini kupata kibali cha kuwa na mfereji wa kumiliki umwagiliaji ni kazi kubwa mno. Si rahisi mpaka ukaombe sijui wapi na visingizio vinakuwa ni vingi mno kiasi kwamba kama ndivyo hivi basi eneo hili tunalolitamka hatuwezi kulifikia.

Mheshimiwa Spika, tunapotamka kilimo ili tukiboreshe, maana yake ni lazima Serikali ihakikishe miundombinu ya kuwasaidia wakulima inafanikiwa kwa mfano, wakulima wetu hawana barabara za kwenda mashambani. Wakulima wetu wanahangaika peke yao. Wakulima hawa wakishalima mazao yao wanapewa masharti namna ya kuyauza. Wakulima wanaweza wakawa wanajua soko mahali fulani nje ya nchi ambalo lingewapatia mapato mazuri, lakini wanambiwa hakuna kupeleka huko. Wakulima hawa ndiyo wanaolisha Watanzania asilimia kumi ambao hawalimi wako mijini, lakini karibu asilimia 80 wako vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa muda huu wote wakulima hawa wanapolima bila kusaidiwa, lakini mwisho wa yote mazao yanapofika wanaambiwa kwamba hamuwezi kuuza kwa bei mnayotaka mpaka Serikali idhibiti na msipeleke nje ya nchi mahali ambako pengine mmesikia pana soko zuri. Mfano, Sumbawanga na maeneo mengine ambayo mahindi yalirundikana walikuwa wana nafasi ya kupeleka nje ya nchi wakauza, lakini ilishindikana. Ilishindikana kwa sababu ya masharti ambayo hayakuzingatia hasara na faida ya kuzuia mazao ambayo watu wamehangaika wenyewe, lakini unakuja kuwapa masharti wakati wa kuuza.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kule Mbarali. Kule Mbarali, tuna maeneo ya mashamba ambayo tunalima mpunga ambao tunalisha karibu Dar-es-Salaam; mchele mzuri ukisikia, unatoka Mbeya na Mbeya sehemu kubwa ni Mbarali. Lakini wale wananchi ukiangalia barabara za mashambani hakuna, hata ile barabara kubwa inayotoka Igawa kwenda Mbarali, ambayo hata ilileta mgogoro mpaka watu wakapoteza maisha bado inajengwa kiwango cha lami, lakini kwa polepole mno. Sasa hivi ina miaka mitano kilometa 18, lakini mpaka leo bado haijafikiwa na wakati najua kule ndiko mazao mengi na mchele mwingi unatoka kule kulisha nchi hii. Hivi kweli, Serikali haiwezi kuona umuhimu wa kuiimarisha barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, naomba ndugu zangu, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, aliniahidi kwamba, barabara ile atajitahidi ahakikishe inafikiwa; nakushukuru sana ndugu yangu. Ndugu zangu ukienda maeneo ya Mwanavala…

**SPIKA:** Lakini uwe na uhakika unai-*discuss report* ya Kamati, wameandika barabara za Mbarali kweli? *(Kicheko)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Haya tuendelee, lakini nadhani sio hivyo. *(Kicheko)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, hasa ninachotaka kusema ni kwamba, ili tuweze kuboresha kilimo ni lazima tuimarishe na miundombinu ya barabara. Sasa barabara ya Igawa–Ubaruku ni barabara muhimu sana kwa kusafirisha mazao. Ukiangalia barabara za wakulima kuelekea mashambani, hazishughulikiwi. Nina mfano, barabara za kwenda Mwanyungu, Mnazi, barabara za kuelekea Mwatenga, barabara za kuelekea Ruango, Ipwani, maeneo hayo yote ni maeneo mazuri ya kilimo, lakini barabara hizo ukiziangalia utaona huruma; watu wanahangaika, hazipitiki muda wote na mazao yako kule, wakulima wanahangaika.

Mheshimiwa Spika, labda nizungumzie suala la mifugo. Wafugaji katika nchi hii wanahangaika utadhani kwamba, hawana maana; ndugu zangu hivi wafugaji kama watasema hawataki kuuza mifugo kwa wiki moja tu, nadhani maandamano yatakuwepo kwa sababu, kitoweo hakitapatikana kabisa. Lakini katika nchi hii, tumesimama imara sana kuweka Hifadhi za Taifa maeneo kwa maeneo, lakini hatutengi maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo, hivi tuna matatizo gani? Wakati mifugo, ndio rasilimali ambayo tunaitegemea sana kwa ajili ya kitoweo, kwa ajili ya wanyama kazi, lakini hakuna mpango hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, maeneo yanayochukuliwa kuwa hifadhi mengine ni ya kilimo, mengine ni kwa ajili ya mifugo. Ndugu zangu niwaambie, Tanzania hii yote inafaa kuwa hifadhi, kwa hiyo, kama tutasema eneo hili linafaa kuwa hifadhi tutenge, tutatenga nchi yote itakuwa hifadhi. Bahati mbaya sana, wakulima wa Mbarali wamekumbwa sana na adha hii. Mbarali tulivyo sisi, wengi mnaitafsiri vibaya, sisi tuko eneo la Bonde la Ufa, tumezungukwa na milima pande zote. Mvua zote zinazonyesha zinakwenda pale Mbarali, bondeni. Sasa tunasingiziwa kwamba, sisi pale ni vyanzo vya maji, ndugu zangu Mbarali, hakuna chanzo cha maji hata kimoja, maji yote yanatoka milimani. Lakini tunaambiwa Mbarali, sisi ni chanzo cha maji na hata juzi juzi hapa, imekwenda Tume nyingine kuchokoza wale wananchi, wanasema na huku kunafaa kuwa hifadhi, wananchi wananipigia simu wanasema bwana tumeingiliwa tena; ndugu zangu nataka niwahakikishie, Mbarali si sehemu ya chanzo cha maji isipokuwa sisi tuko bondeni, maji yanatoka mlimani yanakuja pale, tufanye nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kusema Mbarali ni hifadhi, basi inafaa yote kuwa hifadhi, mtuondoe basi mhifadhi; tumechoka bughudha ya hifadhi, hifadhi. Tumeipokea vizuri sana Hifadhi ya Ruaha na naahidi tutashirikiana nao vizuri; lakini hii kesho, leo, mpaka hapo, walisema Ihefu, tukakubali. Ihefu imetunzwa vizuri na inalindwa na hakuna anayekwenda kule, tumeikabidhi *TANAPA.* Wakasema na vijiji vinavyozunguka

tuviondoe, tukakubali vikaondoka, leo tena wanakuja kusema kuna ndege imepita, mpaka unajua umeonesha mpaka kwa wananchi tena, jamani tutafika kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wana Mbarali tumechoka. Hatutakubaliana tena na Kamati yoyote kuja kule kusema hapa panafaa kuwa hifadhi. Hata hii Dodoma ukitaka iwe hifadhi, hata zamani kulikuwa na wanyama hapa. Hata Dar es Salaam pale, kulikuwa na wanyama, sasa napo tugeuze hifadhi tuondoe watu? Maeneo ya hifadhi, ndugu zangu, nchi hii sasa basi, tujaribu kuangalia na mifugo yetu tunaiweka wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, tumesema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nachukua nafasi kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi, Mheshimiwa Shah, kwa kazi nzuri aliyoifanya. Ameonesha umahiri wake yeye pamoja na Wajumbe wenzake wote walioshiriki kwenye Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujikita kidogo kwenye kilimo. Mwaka 1964 Watanzania tulikuwa milioni saba, tulilikuwa tunazalisha katani tani 234,000; leo katani kwenye nchi hii tunazalisha tani 34,000 tu, tuko watu milioni 42, nataka kujua mkakati wa Wizara. Katani ndio mkombozi wa Watanzania sasa hivi. Kwa bei ya katani ya dola 1,500 kwa tani, tukiweza kuwa na mkakati wa kulima tani 1,000,000 kwa mwaka, tunapata trilioni mbili na milioni mia nne na ajira za watu zaidi ya 1,000,000 katika nchi yetu, lakini Wizara imekaa kimya, haina mpango wala mkakati wowote. Wizara imekuja na Mpango wa Kilimo Kwanza, hakuna hata malengo ya Kilimo Kwanza. Hakuna hata kauli ya kusema Kilimo Kwanza mwaka huu tunahitaji tuwe na tani 500,000 za mahindi, kila mtu anaogelea. Kilimo Kwanza hapa ni kununua matrekta, kununua pembejeo na matokeo yake unakuta mambo hayaendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunashindwa ku-*champion* kilimo, Serikali inatumia bilioni 32, mahitaji ya Magereza kulisha wafungwa ni bilioni 32. Tunashindwa kuwa na mkakati wa kuwafanya wafungwa hawa kuzalisha chakula chao na cha kuuza maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, tatizo liko wapi? Nahisi baadhi ya Watendaji wa Wizara ya Kilimo, siku zote wanaomba nchi hii iwe na ukame ili waweze kuagiza chakula nje, ili waweze kufanya *deal* katika

vibali vya kuagiza sukari. Leo, tumehimiza watu Mikoa ya Kusini, wamelima mahindi mpaka maeneo ya kuhifadhi hakuna, hakuna hata mtu mmoja Wizarani, kutafuta soko la mahindi, soko la korosho, ambazo mpaka sasa hivi zinaharibika na soko la pamba. Sioni Kiongozi wa Serikali, kuanzia Waziri, Katibu, anayekwenda kutafuta masoko ya bidhaa hizi. Tunawalazimisha wakulima wetu, wakulima wetu wanajitolea kulima, lakini hakuna chochote kinachopatikana, wala hakuna msaada wowote wa masoko kutoka huku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma tulikuwa tunalima, mpunga ulikuwa unavunwa mara tatu kwa mwaka, wale waliopita *JKT* wanajua. Lakini leo hakuna *strategy* yoyote, watu wako *exited* na viti walivyonavyo, watu wako *exited* na madaraka waliyonayo, watu wako *exited* na magari waliyonayo, wanashindwa kabisa kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hili inawezekana halipo kwenye ripoti, lakini ni mahali pake hapa. Rais, alitoa mahindi Mkoa wa Dar-es-Salaam kupunguza mfumuko wa bei, tani elfu ngapi zimetoka, hatujui mahindi haya kapewa nani, amelishwa nani, ameuziwa nani na yamemfikia nani? Hatujui na bado tatizo la mfumuko wa bei liko pale pale. Haiwezekani agizo la Rais, la mahindi ya Dar-es-Salaam kupunguza mfumuko wa bei, mahindi haya yapotee mitaani, ni dhambi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa Wizara ya Uvuvi, leo suala la uvuvi linachangia asilimia moja ya pato la Taifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, aibu.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, samaki wanaoliwa Ulaya asilimia sitini ya samaki hao wanatoka kwenye Bahari zetu na hii asilimia sitini ni samaki waliovuliwa katika mazingira haramu. Hakuna udhibiti wa kupata mapato kwenye samaki, tunakosa *almost* bilioni 200 kwenye kipato halali kwenye mchango wa samaki katika nchi hii. Ndio maana tukaishauri na Serikali, kuunda *Economic Defence;* Vyombo vyote vya Ulinzi vikiweza kuwa na vyombo madhubuti ambavyo vinaweza vika-*patrol,* vitafanya kazi ya ulinzi na vitafanya kazi ya kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukitazama watu wanaolima, wote wameshafikia umri mkubwa sana, hakuna mpango wowote wa Wizara kuhamasisha vijana kupenda kulima. Hii itatufikisha katika hatua mbaya sana. Ni lazima Serikali iwe na programu ya kuhamasisha vijana kupenda kilimo kwani watu wanasahau walipotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwasahau wale watu waliotuweka kwenye madaraka, kama hatutawajali waliotuweka na kutuingiza humu ndani, hatima yetu haitakuwa nzuri. Ni lazima sasa tuanze kuwa na programu za kuweza kuwahamasisha vijana kuingia katika suala la kilimo. Nimezungumzia suala la Magereza na kwamba, Wizara hii ishirikishe Magereza katika suala la kilimo, ili kuweza kuokoa pesa za Serikali, ambazo nyingi sasa hivi zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia malengo ya Kilimo Kwanza, ni lazima tuwe na mpango wa kuhakikisha kuwa Wizara inapotoa pembejeo zake na haya matrekta kwenye Kilimo Kwanza, ni lazima tuwe na mipango na malengo ya kitu gani tunalima. Vietnam, mwaka 1994 mpaka 1995, ilikuwa inaagiza chakula nje, leo Vietnam ina *surplus* ya mchele zaidi ya tani 8,000,000 kwa mwaka. Leo Vietnam, wana mbegu ya korosho imetoka Tanzania, wanasafirisha, wao ndio *the highest,* wana-*produce* korosho kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona liko tatizo; malengo tunayo, mipango tunayo lakini katika *commitment* kuna tatizo. Mipango yetu hii yote, hata ile iliyozinduliwa na Rais, mwaka jana, leo inafanya kazi katika nchi jirani; ukienda Rwanda, ndio hiyo hiyo wanaifanyia kazi, sisi tunashindwa nini? Kuna kitu gani ambacho watu tumeshindwa kuelewa? Tuna Wataalam wazuri sana, *the best* wataalam wako kwenye nchi hii, lakini hawatumiki kwa sababu, tunapeana kazi kimkandamkanda. Kwa hiyo, nataka kuzielekeza Wizara zote hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la uvuvi. Namwona Waziri huyu wa Uvuvi, kazi kubwa aliyoifanya hapa Wizarani ni kuchoma hizi nyavu. Naelewa umuhimu wa ku-*preserve* samaki wadogo na elimu itumike, kuelimisha watu kwamba, hawa samaki wakiwa *depleted,* hatutaweza kupata samaki siku za mbele. Hivi hizi nyavu haziwezi kuchomwa madukani? Kuwe na mpango wa kuzikamata hizi nyavu madukani, mimi sikubaliani na uvuvi wa kutumia nyavu hizi, lakini kuwe na mpango mzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema siku yenyewe ndogo, fupi sana; kwa hiyo, Wabunge kama 20 na zaidi bado, hawawezi kufikiwa. Kwa hiyo, naomba nianze kumuita kwanza Waziri wa Mifugo, atafuatia Waziri wa Maliasili na utalii, halafu Waziri wa Kilimo na dakika zenu ni kumi kumi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na mchango wangu huu katika Kamati ya Sekta ya Kilimo na Maji, lakini pia tutatoa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nachangia katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti za taasisi kwamba ni ndogo, ni kweli zilikuwa ndogo hapo nyuma. Lakini mwaka huu wa 2011/2012 kupitia *COSTECH,* taasisi zimepatiwa jumla ya shilingi bilioni 3.22 kwa ajili ya vituo vile vya utafiti kwa maana ya miradi 14 ambayo iko kwenye taasisi zetu hizi za utafiti na vituo vya utafiti, pamoja na kukarabati miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa vya utafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tuna upungufu wa Maafisa Ugani wa Mifugo 11,711, lakini tunaendelea na programu ya kuwaelimisha Maafisa Ugani wa Mifugo, ili angalau kwa muda wa miaka minne au mitano, tuweze kufikia 16,500 ambalo ndilo hitaji letu la kuwa na Afisa Ugani mmoja kwa kila kijiji. Katika uvuvi ni vivyo hivyo, tuna upungufu wa Maafisa Uvuvi 15,746 na kwa sasa tuna 754 tu. Lakini kwa sasa hivi tumeshaanza, tunaongeza idadi na kwa mwaka huu tumesomesha Maafisa Uvuvi na Ufugaji 2,327. Katika suala la upungufu wa wakufunzi ni kwamba, waliopo kwa sasa ni 179, lakini tuna upungufu wa 148 ambao bado tunaangalia uwezekano wa kuongeza, kuweka vivutio kusudi wakufunzi hawa waweze kubaki katika maeneo haya baada ya kuwa tumewaajiri.

Mheshimiwa Spika, Maabara ya Magonjwa ya Mifugo, Temeke, sasa hivi ni Taasisi. Kamati ilishauri kwamba, iwe Taasisi lakini sasa ni Taasisi. Pia Vituo vyote vya uchunguzi wa magonjwa katika Kanda zote, sasa hivi viko chini ya Taasisi hii ya *Tanzania Veterinary Laboratory Agency* na Maabara kuu ya Temeke pia iko chini ya Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji wa samaki. Wizara inashirikiana vizuri na Halmashauri zote kwa kuhamasisha sekta binafsi pamoja na wananchi kujiingiza katika ufugaji wa samaki. Sasa hivi tuna Vituo vyetu vya Kingolwira, Mtama, Mbegani pamoja na Luhila ambao wanaandaa vifaranga wa samaki. Tunahamasisha na tunaendelea kuhamasisha sekta binafsi kujiingiza katika shughuli hii ya kuzalisha vifaranga zaidi kwa ajili ya kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye maji ya baridi na maji ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uvuvi katika Bahari Kuu. Mwaka 2010 tulianzisha Mamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu na Mamlaka hii,

Kanuni zake za 2009 zinafanya kazi, lakini kutokana na kwamba, uwezo wa Watanzania bado ni mdogo, bado hatuna wavuvi wanaovua katika bahari kuu. Lakini tunawahamasisha kwamba, kwa sasa hivi Mamlaka hii ina mpango wa kupeleka wavuvi nchi ya Sri Lanka pamoja na Moldova kusudi waweze kujifunza kwenye Shamba Darasa, jinsi gani ya kutumia vyombo vidogo kuvua katika Bahari Kuu. Mamlaka imeanzisha vyombo vinavyoitwa *Fish Aggregating Device,* yaani vyombo ambavyo vinakusanya samaki, vinavyovutia samaki, samaki wanajikusanya pamoja kwa urahisi wa uvuvi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunawashauri wafugaji waweze kujiunga katika vikundi vidogo vidogo vya kuwekeza na kukopa, kusudi waweze kupata mikopo. Vile vile *MACEMP* ilishaanzisha *project* mbalimbali za kuanzisha benki za wananchi katika Wilaya za Mafia, Kilwa pamoja na Rufiji, ili Benki hizi ziweze kuwasaidia katika kupata zana za uvuvi. Lakini wawekezaji wenzetu wenye viwanda kule Ziwa Victoria, wao wameanzisha programu za kuwakopesha wavuvi zana pamoja na pembejeo za uvuvi na hizi zinawasaidia sana. Wamewakopesha fedha nyingi sana na kwa kweli, zinawasaidia katika kubadilisha hali zao za maisha katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuongeza thamani katika mazao ya uvuvi, katika Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003; Mtu yeyote au mfanyabiashara yeyote ambaye anataka kusafirisha samaki nje ya nchi au mazao ya uvuvi, ni lazima na ni sharti aweze kupata leseni kutoka kwa Mkurugenzi wa Uvuvi. Leseni hii, sharti la kwanza ni kwamba, lazima awe na eneo la kuchakata. Kwa hiyo, haturuhusu kabisa na Sheria hairuhusu kuuza samaki ambao hawajachakatwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeanzisha Vituo vya Doria kwenye maeneo ya Mipakani, ili iweze kukagua na kuangalia kwamba, mazao ya uvuvi hayasafirishwi bila kuchakatwa na hayasafirishwi bila msafirishaji kuwa na leseni.

Mheshimiwa Spika, katika suala la *Ranch* tano za Mkoa wa Kagera, mambo mengi ambayo Kamati imeyazungumzia kimsingi tunakubaliana na kwa sababu eneo hili lina matatizo ambayo kusema kweli ni makubwa kwa sababu yameanza zamani lakini pia yanahusisha Wizara nyingi na idara nyingi. Lakini yale ambayo yanahusu Wizara yetu nitayatolea majibu lakini mengine naweza kuyasemea kama ifuatavyo.

Sisi katika *ranch* zile tayari zilishapitiwa na mipaka inajulikana, wananchi ndiyo wanaotakiwa waheshimu mipaka ile ambayo imewekwa

kwa sababu *ranch* hizi maeneo yake yamepimwa na ranch hizi zina ranchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu JKT kuimarisha kambi ya Kaboya pamoja na kutumia JKT kwa ulinzi wa mipakani, ni jambo ambalo ni zuri na linaweza likaangaliwa kwa ukaribu. Hatua za kurejesha amani ni kweli kabisa, ni lazima mahusiano kati ya wawekezaji na Serikali na pamoja na wananchi yawepo na kuna juhudi za kuboresha mahusiano hayo na ni pamoja na kuimarisha Kamati za mahusiano na ujirani mwema. Kwa mfano, katika *ranch* ya Kagoma yenyewe ina Kamati ambayo inahusisha wawekezaji, wanavijiji pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Watendaji wa Vijiji pamoja na wanasiasa wengine wanatakiwa kusema kweli, kuchunguza na kuangalia wao pia ni vyanzo vya migogoro katika *ranch* hizi za Mkoa wa Kagera kwa sababu kuna wanasiasa wengine pia wanachukua nafasi hizi kuchonganisha na kuwapiga vita wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha kodi cha shilingi 220 kwa ekari kwa mwaka nakubaliana nacho kwamba ni kidogo sana, kwa kweli idara zinazohusika inabidi zipitie kusudi kiwe *realistic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesi nyingi kusema kweli ziko Mahakamni lakini tutaendelea kuwasiliana na mahakama kusudi waweze kumaliza kesi hizi kwa uzito unaostahili kwa sababu kesi hizi zimekuwa ni za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mashamba ya miwa yatazamwe upya, Serikali itaendelea kulifanyia kazi suala hili kuendelea kuangalia kama kuna uwezekano mashamba haya yakatoa nafasi kwa ajili ya shughuli za malisho ama malisho ya mifugo. *NARCO* iwezeshwe kupata mtaji.

Mheshimiwa Spika, *NARCO* ni shirika la kibiashara linaendeshwa kibiashara pamoja na kupata fedha au ruzuku kutoka Serikalini, lakini wao wanaweza wakakopa kwenye mabenki ya biashara na kuweza kufanya biashara kwa faida.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza maeneo haya, tumeshaanza kufanya kazi hii hasa tumeanzia katika maeneo ya mipakani kama wameshindwa na kwa kweli tutawanyang'anya ili tuweze kuwapa wawekezaji wengine. Kwa sababu haiwezekani mwekezaji achunge kawaida na wakati kwenye *business plan* aliahidi kuweka miundombinu na kufuga kisasa, kwa hiyo hilo suala tumeanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, *NARCO* inaendelea kutafuta wawekezaji na sasa hivi tuna wawekezaji watatu Afrika Kusini, Amerika na Kenya kwa ajili ya kuwekeza katika *NARCO*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wenzangu wanisikilize na naomba wanisikilize kwa makini hasa wale wanaopenda kutenda haki. Naomba kabla ya kuzungumzia mambo ambayo yametolewa kama taarifa na Kamati, nitoe tu masikitiko yangu kwenye baadhi ya maeneo, la kwanza ni suala la *Natural Justice,* ripoti ina tuhuma nyingi, lakini sijashirikishwa. Kanuni inasema Waziri anakuwa mjumbe pale ambapo suala la Wizara yake linapojadiliwa. Kanuni ya 114(17) inasema Waziri na Naibu wake atapatiwa ripoti ya mambo ya msingi ya mambo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Novemba, 2011 Kamati ilikutana na wasafirishaji wa wanyama hai nje yaani TWEHA, wakawasilisha tuhuma nyingi dhidi ya Wizara, lakini katika kikao kile hakuna Afisa wa Wizara wa Maliasili na Utalii aliyekuwepo. Baada ya kupokea taarifa hiyo Kamati ikaazimia kuunda uchunguzi, au ikaunda Tume ya Kuchunguza bila hata ku-*inquire* kwamba tumeletewa barua na TWEHA hapa ya tarehe 29 Aprili, Waziri unasemaje kuhusu barua hii. Kilichokuja kutokea ni Wizara inataarifiwa kwamba tumeunda Kamati tunachunguza.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi niliitwa kwenye Kamati ya Uchunguzi ya kina nikaulizwa, Mheshimiwa Msigwa naomba kwa hili tuzingatie zaidi Mchunguzaji zaidi ya Mbunge, niliwauliza kwenye Kamati mmeniita kama nani, wakaniambia kwamba tumekuita kama rafiki wa Kamati. Niliitwa kama mtu wa tatu mwanzoni nikawaambia sawa, kwa sababu kama mmeniita kama Waziri, natakiwa nije mwisho baada ya kuwa mmeshasikiliza kero zote, mnafanya *exit interview*, hata kwenye *audit*, mkimkagua mtu mkapata tuhuma mnamuuliza anajibu, lakini halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, tarehe 19 Aprili, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilikutana kupokea taarifa ya Kamati Ndogo ya Uchunguzi. Kanuni 113(1) inasema Waziri awepo lakini sikuwepo. Katika mazingira hayo, taarifa ya Kamati hii nimeiona leo hii asubuhi, ndiyo maana Mheshimiwa Msigwa aliuliza Maige yuko wapi, tuliambiwa kwamba ripoti hii inakuja kujadiliwa mwezi Juni, nimekuja kushtuka kwenye *order paper* suala hili lipo. Nikatafuta ripoti siioni, nimeipata saa tano, wahudumu humu Bungeni wanajua na Mungu

anajua ndiyo nikakimbia kwenda kuanza kujiandaa. Ule muda unaniuliza nina jibu katika mazingira haya, nina dakika kumi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana pengine Mheshimiwa Lukuvi uibue hoja ya kuahirisha mjadala huu nikaandae majibu mazuri ambayo yatasaidia kwenye utetezi kama kweli tunataka kutenda haki hasa pale kwenye suala la uwajibikaji linapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika masikitiko yangu ni muundo wa taarifa moja, ripoti imewasilishwa Bungeni baada ya kujadiliwa kwenye Kamati bila Wizara kushirikishwa kama nilivyosema. Pili, ripoti imewasilishwa ghafla kama tulivyokuwa tunajua kwamba inakuja Juni, nimeipata saa tano ndiyo nikakimbia kujiandaa na matokeo yake maandalizi hayajakuwa ya kutosha.

La tatu, naomba kwa wote mlioisikiliza *focus* ya ripoti, ripoti ina kurasa 91, ukurasa mmoja tu umezungumzia ardhi na mazingira, kurasa 90 zote ni maliasili kana kwamba haitoshi si tatizo lakini nazungumzia hasa suala la *focus*, kwa sababu baadaye litakuja kutusaidia kujenga maamuzi katika mapendekezo yaliyokuja kutokea.

Pili, ripoti inavyoelezwa hapa ni ripoti ya mwaka ya Kamati, lakini ukiangalia kurasa 13 tu, ndiyo zimezungumzia mambo ya kazi ya Kamati, kurasa 77 ni ripoti ya uchunguzi, *fine* si *issue* vilevile. Suala la tatu, ni mawasiliano kati ya Wizara na Kamati, tatizo nafikiri ripoti kwenye mawasiliano kwa sababu kama nilivyosema baada ya Kamati kuwa imewasilishiwa ile taarifa na *TWEHA* tarehe 29 inayozungumzwa kwamba wanyama walisafirishwa. Kamati haikuiuliza Wizara, kana kwamba haitoshi kwenye hadidu za rejea ikaweka suala la vitalu. Sasa katika mazingira hayo suala la vitalu sisi kama Wizara tumekuwa tukiendelea kulishughulikia. Ukisoma vizuri suala la vitalu lina mkondo wake wa kisheria. Kwa mujibu wa Sheria namba tano ya mwaka 2009, kifungu cha 38(14) hadi (16) kinasema: "Baada ya Waziri kuamua wale ambao hawajaridhika wanakata rufaa kwa Waziri baada ya wao kutokuridhika na majibu ya Waziri wanakwenda Mahakamani si Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, mimi najiuliza hivi, kama kuna malalamiko hivi anayelalamika anayapelekaje Bungeni ambapo anaweza akayapeleka Mahakamani ambako ndiyo sheria inasema yapelekwe ndiyo kunakokwenda kutafsiriwa kama tumetafsiri sheria vibaya. Katika mazingira hayo niseme tu kwamba, hilo na lenyewe limekuwa ni changamoto. Kubwa zaidi katika masuala yote ya msingi yaliyokuwa yanachunguzwa suala la kwanza la wanyama waliosafirishwa, Kamati bila kutafuna maneno imesema haijapata

ushahidi wa wanyama kukamatwa wala kusafirishwa nje, majibu ambayo tulikuwa nayo wangetuuliza, ilikuwa ni suala dogo tu la ku-*clarify* basi wala lisingehitaji *investigation*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 34 wa taarifa ya kaka yangu Mheshimiwa Lembeli, unaanza kwa kusema kwamba, kwa ujumla Kamati inasema kwamba utaratibu wa kisheria ulizingatiwa. Sasa refa unasema kwamba ujumla mechi ilikwenda vizuri, sheria zilizingatiwa, halafu baada ya hapo unasema hata hivyo kwa sababu mechi ilikuwa inakwenda kidogo sana na refa alikuwa anapuliza kipenga mno, kwa hiyo, refa anyongwe. Wakati mwanzo umesema sheria zimefuatwa, haya yaliyobainishwa ni mapungufu madogo madogo ambayo kimsingi nilitegemea kwamba yangeenda.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni suala la *lobbying*, kumekuwepo na vikundi vinafanya *lobbying,* vinafanya semina kwenye Kamati, vinakuja hapa katika mazingira hayo, kwenye gazeti la Mtanzania la tarehe 20 Aprili, 2012 limeripoti kwamba mfanyabiashara amefanya semina tarehe 16 *Saint Gasper*, akiwahamasisha wajumbe wa Kamati hii waje wakatae. Ukiangalia michango ya Wabunge karibu wote wa Kamati imekuwa *extremely negative* kwenye Wizara hii. Waliochangia wengine kama rafiki yangu Wenje na Mzee Mrema wamekuwa *courage away* kwa sababu ya sura ya taarifa iliyotayarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hoja ambazo zimewasilishwa, la kwanza kuhusu ugawaji wa vitalu mchujo wa awali uliofanyika ulionesha kwamba kampuni 91 ziliomba vitalu na orodha ninayo hapa, hakuna kampuni hata moja ambayo iligawiwa vitalu bila kuomba. Pili, kigezo kilikuwa ni kuvuka alama 50 kampuni zote zilizogawiwa vitalu zilivuka alama 50. Kamati katika ushauri wa awali ilipendekeza kwamba kampuni 42 za Kitanzania na kampuni 16 za kigeni zipewe vitalu. Kwa kufanya hivyo ilimaanisha kwamba tuvunje sheria kifungu cha 39, ambacho kinasema wageni wapewe asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, nikawaita Kamati nikawaambia haiwezekani tukavunja sheria, ndiyo wakasema basi tupunguze Kamati za kigeni, tuongeze Kampuni za Kitanzania, tukaongeza kampuni za Kitanzania, tukapunguza kampuni za kigeni saba. Hizi tisa tulizoziongeza zote zimevuka alama hamsini na hili tumelifanya na Kamati yenyewe. Kuna dai la kwamba kampuni 16 zimepewa vitalu bila kuomba, si kweli. Mheshimiwa Lembeli tumpende Mungu na tumche Mungu, kampuni ya *FOA adventures* kwa mfano, mmesema kwenye orodha ya kampuni 16, si kweli kwamba hizi kampuni zote zimepewa vitalu bila kuomba zote zimeomba na zote zina sifa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana sijui tutaamuaje, lakini mawazo yangu ni hayo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Kamati zangu zina uwezo wa kufanya kazi, kwa namna walivyofanya. *(Makofi)*

Sisi tulishatangaza kwamba taarifa zote zimekuwa *tabled* hapa, fikra yangu ni kwamba Serikali mmeshachukua na hata kama tumesema tutajadili mwezi wa Sita, lakini Serikali ilipaswa mchukue hizi taarifa muwe tayari mmejibu. *(Makofi)*

Bado pia mnadaiwa kujibu kwa maandishi na mpelekeeni Waziri Mkuu ndiyo utaratibu huo, sisi tutakutana na hizo taarifa kwa *coordinator* wa Serikali ambaye ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, msije mkaenda ku-*relax* hamjamaliza kazi, haya maana yake ni maneno yaliyoletwa na taarifa zimeandikwa, kwa hiyo, mkaanze kufanya kuanzia sasa. Itakapofika Juni, itakuwa tatizo zaidi. Kwa hiyo, naomba nimuite Waziri wa Kilimo, dakika zako ni kumi tu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi, nitachangia kidogo katika hoja chache ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, moja hii ni ya pembejeo. Katika mchango wangu wiki iliyopita nilieleza kidogo kwa nini katika mfumo wa kutoa ruzuku ya pembejeo kupitia kwenye vocha, vocha zinachelewa. Kwa sababu kwa utaratibu wa manunuzi uliowekwa, kampuni ya kuchapisha vocha inateuliwa baada ya bajeti kupitishwa. Hivyo, mwaka jana bajeti ilipitishwa tarehe 25 Julai na hivyo mchakato ndiyo ukaanza pale. Kwa hiyo zilichelewa, lakini tulitumia utaratibu mbadala wa kufikisha pembejeo kwa wakulima, halafu vocha zilipofika ndiyo wakulima wakapewa kuzisaini ili Mawakala waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu mbadala ulihusu fomu ambazo wakulima walikuwa wanapewa na kuziweka saini baada ya kupewa pembejeo. Aidha, pembejeo zilikuwepo nchi, ambacho kilichelewa ni vocha. Sasa katika mikoa ambayo Mawakala waligoma kutumia utaratibu huo ndiyo ambapo pembejeo hazikuwafikia wakulima kwa urahisi na kwa wakati muafaka. Kutokana na hali hiyo, kama nitakavyoeleza tutabadili mfumo wa kutoa pembejeo mwaka huu ili tusitumie vocha kwa sababu zinachelewesha kufikisha pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja kwamba katika maeneo mengine kunakuwa na udanganyifu na uchakachuaji wa pembejeo. Pembejeo zinazoingia nchini za mbolea na mbegu zinaingizwa kwenye

soko na makampuni ambayo yamepewa leseni kwa ajili ya kufanya hivyo. Hapa kwetu ni pamoja na kampuni ya Tanzania *Fertilizer Company Minjingu* na kadhalika. Mbolea ikishaingia kwenye soko anayechukua sampuli kuhakikisha kwamba ina ubora unaotakiwa ni shirika la *TBS*. linachukua sampuli bandarini, mbolea inavyoingia na linategemea lichukuwe pia mikoani na kwenye *farm gate*, yametokea matatizo. Kuna wakala mmoja wa pembejeo amechanganya *DAP* ile ambayo ni *phosphorus* na sementi na kuna ambao mwaka huu wamechanganya mbolea ya *UREA, CAN* na chumvi hii ya mezani. Wote hawa ambao tuliwapata wamekamatwa na wako Mahakamani wamefunguliwa kesi za kuhujumu uchumi*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ili kukabiliana na matatizo haya, tumekuwa tukijadiliana namna ya kubadilisha mfumo huu wa kupeleka pembejeo kwa wakulima. Tulichoamua makampuni yanayotengeneza mbolea yenyewe au wale wanunuzi wa mbolea wakubwa kama *TFC* watapeleka mbolea mpaka Makao Makuu ya Wilaya. Mbolea ikishakabidhiwa pale utawala wa Wilaya ile uka-*clarify* kwamba kweli hiyo mbolea imekuja, Mawakala wa kampuni ile iliyopeleka mbolea pale watapeleka mbolea mpaka kijijini. Tunatengeneza utaratibu wa *TEHAMA* ambao utatuwezesha, mkulima anachopokea ni pembejeo siyo pesa na wala siyo vocha ili kuhakikisha Mawakala hawakimbizi vocha wanakimbiza pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na malalamiko kidogo hapa kuhusu masoko ya mazao na kwamba Wizara hazitafuti masoko. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika kipindi hiki Wizara yangu imeliona tatizo kubwa la masoko hasa ya mahindi na katika kutafuta masoko Wizara yangu imekubaliana na *World Food Program* kununua mahindi yenye thamani ya dola za Kimarekani 56,000,000 katika msimu huu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, mauzo ya mahindi katika soko la Dar es Salaam, Mheshimiwa Azzan Zungu amelalamika kidogo kwamba, ni nani anauziwa na kwa sababu mauzo haya yanafanywa kwa uwazi, ningemwomba sana Mheshimiwa Zungu afike kwenye ghala unapofanyika uuzaji huo ili aweze kukagua na kuona uwazi ambao unatumika. Wanaouziwa ni wasagishaji wadogo wa mahindi na bei inayouziwa inajulikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ningependa nitoe maelezo mengine kwa haraka haraka. Kumekuwa na hoja kwamba Serikali iongeze bajeti ya Kituo cha Utafiti cha Maruku ili kiweze kutekeleza

majukumu yake kikamilifu. Aidha, Serikali inashauriwa kukirejesha kituo na majengo ambayo yalichukuliwa awali katika kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mpango wa kuimarisha huduma za utafiti nchini kupitia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo. Kupitia programu hiyo taasisi zote za utafiti nchini zimekuwa zikifanyiwa ukarabati hatua kwa hatua. Kituo kile nimekitembelea mwezi uliopita na pamoja na mambo mengine tutakijengea uwezo wa kuweza kuzalisha migomba misafi ambayo haina magonjwa kwa ajili ya kuwapatia wakulima. Nafasi hiyo ya kujenga ipo na kituo hicho kitaanza kujengwa kuanzia bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali itenge bajeti ya kutosha ya kununulia chakula na kukarabati maghala ya kuhifadhia chakula. Serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imeshakabidhiwa maghala ya kuhifadhi mahindi yaliyokuwa yanamilikiwa na *NMC*. Maghala hayo ni ya Mwanza yenye uwezo wa kuhifadhi tani 15,000, Iringa tani 17,000 na utaratibu unaendelea kwa maghala ya Arusha tani 38,000 na Dodoma tani 30,000. Maghala yote hayo yanahitaji kukarabatiwa na bajeti ya kukabarati imewekwa kwenye bajeti ambayo inapangwa kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wakala wa Kuhifadhi Chakula yaani *National Grain Reserve* utakarabati maghala yaliyopo Manyoni ambalo lina uwezo wa kuchukua tani 4500, Musoma tani 4500 na itaendeleza ukarabati Singida tani 4500 na *NFRA* pia katika mwaka wa fedha unaokuja imepanga kuyafanyia tathmini maghala 30 nchini ambayo yana uwezo wa kuhifadhi tani 241,000 za nafaka.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na mchango kuhusu …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira. Bahati mbaya na wewe una dakika kumi tu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii niweze kuhitimisha hoja ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimtoe hofu ndugu yangu Mheshimiwa Maige kwamba Mungu ni mmoja, yupo kwa ajili ya watu wote na kazi yake ni kusimamia haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Maige badala ya kujibu hoja…

**SPIKA:** Naomba labda useme Waziri wa Maliasili.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Amezungumzia *procedure*. Kamati yetu imefanya kazi kwa mujibu wa kanuni na yote yaliyowekwa mbele ya Bunge hili tuna hakika ni ya kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mengi ambayo hatukuyasema, moja, ni kwamba Kamati yetu inasimamia Wizara tatu na kati ya Wizara hizo tatu Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira. Wizara ambayo inaipa shida Kamati hii ni Wizara ya Maliasili na Utalii, imejaa watendaji walio na jeuri na pengine ndiyo maana Mheshimiwa Maige hajaweza kupata taarifa ya Kamati yetu. Nashindwa kuelewa, mikutano yote ya Kamati hutangazwa na wewe Mheshimiwa Spika ndani ya Bunge hili Tukufu, sijaona kanuni inayosema kwamba Mwenyekiti amtaarifu Waziri *in person* kwamba leo tuna kikao kuhusu jambo hili. (*Makofi*)

Semina ya juzi *Saint Gasper* Kamati ilipewa taarifa kwamba kuna Mtanzania anataka kuongea na Kamati na sisi kama wajibu wetu tumekutana naye. Lakini napenda kusema kwamba ukiona mtu anaongeaongea sababu nyingi sana anaficha ukweli. Siku ya Alhamisi ukurasa mzima katika gazeti la Mtanzania Kamati yangu imeshutumiwa kwamba imepokea rushwa, imepewa mapesa lakini ukweli umedhihirika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kwanza niwapongeze Wajumbe wa ile Kamati ya uchunguzi ambao wakati nikiwasilisha sikuwapongeza. Nao ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa na Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu. *(Makofi)*

Aidha, niwapongeze Katibu wa Kamati Ndugu Mswige Disckon Bisile, Hellen Stephen Mbeba, Mjumbe wa Sekretarieti, Ndugu Erick Sosthenes Maseke, Mjumbe wa Sekretarieti na Ndugu Rahel Nyambuli Nyega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imefanya kazi katika mazingira magumu sana, kuna maeneo Wizara ilikataa katakata kuwapa nyaraka ambazo zingeweza pengine kuboresha taarifa hii. Lakini kwa jitihada kubwa na kwa sababu Mungu alikuwa nao kwa sababu walikuwa wanatafuta haki wameweza kufanya kazi yao vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu imechangiwa na Wabunge kwa ujumla wao 28, lakini Wabunge 14 kwa maandishi na 14 kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwashukuru na kuwapongeza. Wengine wamechangia hoja ya taarifa yetu ikimaanisha kwamba imewagusa lakini ni wajibu wa sisi Wabunge kuyasema yote haya ambayo yapo kwenye taarifa yetu. Naomba niwapongeze na niwatambue…

**SPIKA:** Hapana, usiwataje kwani muda hautoshi.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, hoja za Kamati hii kimsingi sisi tumeliomba Bunge liiagize Serikali, aidha, itake maelezo kutoka kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, tumeliomba Bunge liitake Serikali iwawajibishe maafisa ambao wamejihusisha kwenye masuala ya rushwa, ufisadi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri anahoji kwamba baadhi ya taarifa tulizozitoa hapa zina walakini. Nataka niseme kwa mfano, haya makampuni 16 yaliyoainishwa kwamba yamepewa vitalu bila yenyewe kuwa yameomba hivyo vitalu na kwamba yapo makampuni ambayo Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu ambayo yapo kisheria, mapendekezo yake Waziri aliyaweka mfukoni na badala yake akaleta yake.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, Kampuni ya Malagalasi *Hunting Safari Limited*, kampuni hii imekuwa ikifanya uwindaji kwa muda mrefu hapa nchini. Hivi tunavyozungumza Kampuni hii ina kesi na Serikali na aliyeishika ni Wizara yenyewe ya Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

Katika mapendekezo ya Kamati ya ushauri walipendekeza katakata watu hawa wasipewe vitalu na si Malagalasi pekee zipo na kampuni nyingine nazo ni *Coastal Wilderness Safaris.* Hii kampuni inamilikiwa na famili ya Marehemu Sokoine nayo ni miongoni mwa kampuni ambazo hazikupendekezwa. Sasa cha ajabu, kwa nini achukuliwe *Malagalasi Hunting Safaris* ambaye hakupendekezwa apewe na *Coastal Wilderness Safari* ambaye na yeye hakupendekezwa anyimwe, kimetumika kigezo gani? Zipo nyingi kama kampuni inayoitwa *Mwanauta Hunting Safari, African Trophy, Wide Sport Prints,* zote hizi

Kamati ya Ushauri ilikuwa imesema hazikidhi kupewa vitalu na kampuni hizi nyingine zina madeni hazijalipa kwa Serikali na wengine wanadaiwa na wateja ambao wamekuja kuwinda na hawajapelekewa *trophies* zao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii kwa maandishi na kwa kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba sasa ni wakati wa Serikali yetu kuwajibika kwa majukumu ambayo wamepewa na wananchi, muda wa kujitetea haupo. Tanzania ina raslimali nyingi ambazo zingelitoa Taifa hili kwenye umaskini. Raslimali za nchi hii na maliasili sasa zimegeuzwa kuwa shamba la mjane aliyefiwa na mume wake kwamba kila mtu anaweza akaja akavuna, akadai huyu alikuwa ndugu yangu, akaondoka. Tembo wanaondoka…

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ambayo niliiwasilisha asubuhi.

Mheshimiwa Spika, ningependa niwashukuru Wabunge wote ambao walichangia na ambao hawakuchangia. Nina imani wale ambao hawakuchangia ni kwa sababu walikubaliana na shughuli ambazo tulikuwa tume-*report* hapa.

Waliochangia kwa kusema Bungeni ni Wabunge 10 na waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 15.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba katika michango yote walikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kilichofanyika ni kuboresha tu maeneo fulani. Nitambue jedwali la marekebisho ambalo tumelipata kutoka Mheshimiwa Halima Mdee ambalo hatuna matatizo nalo na tunalichukua kama lilivyo kuweza kuboresha mapendekezo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote waliochangia kama nilivyosema walichangia kwa kuboresha yale tuliyopendekeza na mimi nitakachofanya ni kuzungumzia maeneo mawili au matatu ambayo

yamezungumzwa sana ili kuweka msisitizo katika yale ambayo tulitoa kwenye *report* yetu na vile vile yale ambayo wenzangu walitusaidia kuweka msisitizo ili Serikali iweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la Kamati Ndogo iliyokwenda Kagera. Kule kuna matatizo, kuna matatizo amani haipo, wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka *ranch* wanakuwa kama wageni na tulipoongea nao kwenye mikutano ya hadhara wengi walikuwa wanalia, walikuwa wanaongea jinsi wanavyonyanyaswa kwa hisia kali sana. Walikuwa wanalia na kwa bahati mbaya tuliongozana na Mbunge ambaye sitamtaja jina, naye alilia.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kusisitiza kwa Serikali kwamba, hali kama hii wale watu hawalimi, ni kukimbiakimbia na wale watu wanam-*suspect* kila mtu. Tumependekeza kwamba kwa sababu inaaminika kwamba baadhi ya wamiliki wa vile vitalu siyo wamiliki hasa, wamiliki wako nje ya nchi na wengi wao siyo Watanzania. Wazo tulilolipendekeza kwa Serikali ni kwamba uhakiki ufanyike haraka tujue nani mmiliki halali na wale ambao siyo Watanzania waondoke mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Bunge lisisitize kwa Serikali kwa sababu mapendekezo ya namna hii yamewahi kutolewa huko nyuma lakini yanaishia kwenye makabati hayajafanyiwa kazi. Ifike mahali tuseme sasa basi!

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji limezungumzwa na watu wengi. Wote tunaamini na kujua kwamba nchi yoyote ambayo imefanikiwa kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yake kuhusu suala la umwagiliaji limejitokeza na kupewa hadhi kubwa kubwa sana. Mvua hazitabiriki, lakini zipo hapa nchini, baadhi wana msimu mmoja na wengine misimu miwili lakini wote tunajua kwamba mvua zinaponyesha ni kiasi kidogo tu cha maji kinabaki mashambani lakini mengine yanatiririka kwenye mito au bahari. Baadhi tumetoa takwimu kwamba ardhi inayoweza kumwagiliwa ni zaidi ya hekta milioni 26 lakini zilizomwagiliwa mpaka sasa ni hekta 344.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kufanya hesabu ili nijue ni asilimia kiasi gani, niliona kuna masifuri mengi baada ya nukta lakini ninachosema ni kwamba, ni kiasi kidogo sana. Lakini sera ya umwagiliaji ipo na Serikali inayo hiyo sera na unajiuliza kwamba tunaipa kipaumbele gani? Wakati mwingine tukiwauliza Serikali wanasema hawana fedha, fedha hazitoshi, ndiyo maana haijatekelezwa lakini kupanga ni kuchagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vifaa vya umwagiliaji pia tunapendekeza vifutwe kodi. Tulitembelea scheme moja inaitwa Nyida Shinyanga, tukapewa *report* nzuri na wakaishia kusema kwamba utekelezaji umekuwa mbovu kwa sababu hakuna mvua za kuridhisha. *Definition* ya umwagiliaji ni kwamba uweze kumwagilia hata wakati wa kiangazi na hawana bwawa mahali popote, wanaweza wakapata maji na hii wanaita ni *scheme* ya umwagiliaji, lakini siyo *scheme* ya umwagiliaji hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililojitokeza wamechangia watu wengi ni kilimo kwanza. Kwanza, dhana yenyewe ya kilimo kwanza haijaeleweka vizuri na watu, ni *document* nzuri lakini haiko wazi. Watu hawajui kwamba mifugo na uvuvi imo katika kilimo kwanza na kwa Mswahili wa kawaida ukizungumza habari ya kilimo yeye anajua ni jembe na ardhi basi imekwisha, lakini hatujui kwamba kuna *mechanisation*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna *agro processing* ambavyo vipo pamoja katika kufanikisha hili suala zima la utaratibu wa pembejeo, tumetoa mapendekezo yetu na Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba wanabadilisha mfumo. Sisi tulikuwa tumesema kwamba, mfumo huo haufai na kwamba ni lazima ubadilishwe na tumewahi kukaa na Waziri tukimueleza yale yanayojiri huko kwa wananchi wenyewe ambao ni walengwa hawafaidiki kabisa. Tumeelezwa kwamba, ukaguzi maalum wa pembejeo umeanzishwa na *CAG*. Tungependa hili liletwe haraka ili tujue nini kinajiri.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi limezungumzwa sana. Vilevile tuna bahati tuliyopewa bure na Mwenyezi Mungu lakini hatujaitumia vizuri, tuna *fresh water*, bahari yenye eneo la urefu wa kilomita 1,000 lakini pia tunakwenda ndani kabisa. Namshukuru Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Zungu wametoa *data* hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la *deep sea fishing* limejitokeza kwenye Kamati yetu. Hata hivyo, hatuoni kama kuna *seriousness* katika ku-*exploit* hilo. Wajapan walikuja kuvua kidogo sijui Wakorea, sasa ikawa ndiyo nongwa. Sasa kama samaki hawavuliwi na sisi wenye samaki, wafanye nini? Ndiyo imekuwa matatizo.

Sisi tunaishauri Serikali kuwa na mikakati inayoeleweka tunaweza kweli kutumia hazina ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu ili tuweze kupata kile kinachowezekana kutoka kwenye bahari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia pia kwamba Ziwa kama Victoria nusu ya Ziwa kama siyo asilimia 48 ni ya Tanzania. Kenya ni asilimia 15, lakini wanaofaidika zaidi ni Kenya. Wanakuja kununua samaki,

tuna viwanda sisi lakini wao wanakwenda kusindika na kuboresha mapato. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumeomba kwamba mikopo kwa wavuvi iwezekane, kuwe na doria kwa sababu samaki wengi wanasafirishwa kwenda nchi za nje. Tumeshauri pia kuwe na mabwawa binafsi, kodi kwenye vifaa vya uvuvi iondolewe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa toa hoja.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Ahsante!

**SPIKA:** Toa hoja. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki mapendekezo yote ya Kamati mbili yapelekwe Serikalini kwa hatua zilizopendekezwa)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa mtakubaliana na mimi kwamba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mliochangia, Wenyeviti wa Kamati na Mawaziri waliopata nafasi kuweza kujibu hoja. Kama nilivyosema hizi taarifa zetu ni ndefu, zimeandikwa kwa kirefu na mapendekezo yao yako *very precise*. Nawaomba Serikali wapokee taarifa hizi zote; zile zilizojadiliwa na zisizojadiliwa lakini zote zimekuwa *laid on the table*. Kwa hiyo, nategemea kila Waziri atatafuta hizi taarifa za mwaka za Kamati kusudi waingie kwa undani kujaribu kujibu hoja na mapendekezo ambayo Kamati zimetoa. Majibu yenu mtapeleka kwa Waziri Mkuu na nakala nyingine mtapeleka kwa Katibu wa Bunge ambaye atazirudisha kwenye Kamati na Kamati zina wajibu wa kufuatilia yale majibu mliyotoa. Huo ndio wajibu wa Kamati. Kamati itafuatilia kwa undani yale majibu mliyotoa. *(Makofi)*

Kwa Waheshimiwa Wabunge kuishika Serikali kwa mfumo wa Kamati zetu ni rahisi. Kila Kamati ina sekta zake na ina Wizara mbili au

tatu. Sasa kama nyie hamuishiki Serikali ni kosa lenu wenyewe. Kwa hiyo, msianze kulalamika, kwa sababu mnazo nyenzo za kufanyia kazi na kila Wizara hapa ipo chini ya Kamati mojawapo. Sasa kama nyie mmekaa vibaya msilalamike hapa, mnatoa maneno yenu na Bunge litaamua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaombeni sana mlizingatie hili. Hakuna sababu ya kulalamika kwa sababu kila Kamati inashika Wizara na mnatakiwa kufanya nao kazi kila siku ukiacha zile Kamati za *watch dogs*. Kwa hiyo, naomba sana muelewe namna ambavyo mnatakiwa kufanya kazi. Hilo ndiyo ambalo ningependa kuwaambia. *(Makofi)*

Sasa napenda kuwahoji kuhusiana na mapendekezo haya, bahati nzuri mapendekezo aliyoleta Mheshimiwa Halima Mdee ile karatasi imesambazwa. Inaonekana Mwenyekiti hakuwa na matatizo nayo kwa hiyo, tutayapitisha kama alivyopendekeza Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanaokubali mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira waseme ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote wamekubali mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Halima Mdee waseme ndiyo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Hakuna aliyesema siyo, wote wamekubali. Kwa hiyo, mapendekezo yetu ni maazimio kwa Serikali kwamba yatekelezwe. Mtafuatiliwa na Kamati hizo hizo kwa mambo mliyofanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache. Kwanza kabisa ni Naibu Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, anasema niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa leo tarehe 23 Aprili, 2012 baada ya kuahirisha kikao hiki, sasa hivi, kutakuwa na kikao kwenye ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Halafu mmegawiwa vitabu vya namna hii vinaitwa Mapendekezo ya Mfumo wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2012/2013.

Wote mmegawiwa kwa hiyo, kesho vitabu hivi vitatumika katika shughuli tutakayoifanya kesho katika Ukumbi wa Msekwa. Baada ya kusema hayo Katibu.

**NDG. JOHN JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zilizopangwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge sasa zimekamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, sasa nitamuita mtoa hoja ya kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza majukumu yote yaliyopangwa kwa ufanisi mkubwa katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioanza tarehe 10 Aprili, 2012. Tumefanikiwa kufanya hivyo kutokana na maandalizi mazuri ya Mkutano, ushirikiano miongoni mwetu na Waheshimiwa Wabunge wote kujiandaa vizuri katika kuchangia hoja mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu tumepata Waheshimiwa Wabunge wapya wawili wote kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge Mpya wa Jimbo la Arumeru Mashariki. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge kupitia Viti Maalum (CHADEMA), kipekee kabisa nawapongeza wananchi wa Arumeru Mashariki kwa kutumia haki yao ya Kidemokrasia vizuri. Lakini kwa dhati kabisa, nakipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kukubali matokeo ya uchaguzi mdogo wa Arumeru Mashariki. Kitendo hicho kinaonesha uungwana na ukomavu wa kisiasa na demokrasia katika nchi yetu. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa na vyama vingine vyote vya siasa nchini. *(Makofi)*

Kwa Waheshimiwa Wabunge wapya, tunawatakia mafanikio na tunawaahidi ushirikiano wetu ndani ya Bunge na katika kujenga Taifa letu. Vilevile napenda kutumia nafasi hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Madiwani wote waliopata ushindi katika chaguzi zilizofanyika katika Kata za Vijibweni (Temeke), Kiwangwa (Bagamoyo), Kirumba (Mwanza), Logangabilili (Bariadi), Chang'ombe (Dodoma), Kiwira (Rungwe), Lizaboni (Songea) na Msambweni (Tanga). Tunawatakia wote

waliochaguliwa afya njema na maisha mazuri ili muweze kuwatumikia wananchi waliowachagua na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge tulifanya uchaguzi wa wawakilishi wa nchi yetu katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza wafuatao kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge hilo; Mheshimiwa Makongoro Nyerere; Mheshimiwa Abdullah Hassan Mwinyi; Mheshimiwa Nderakindo Kessy; Mheshimiwa Angela Kizigha, Mheshimiwa Adam Kimbisa, Mheshimiwa Twaha Issa Taslima, Mheshimiwa Bernard Murunya, Mheshimiwa Shy-Rose Bhanji na Mheshimiwa Mariam Ussi Yahya. *(Makofi)*

Kwa dhati kabisa tunawapongeza wote hawa kwa ushindi walioupata. Tuna imani kubwa kwamba watatuwakilisha vyema katika Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa maslahi ya Tanzania kiuchumi na kijamii na nchi zote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kuhitimishwa kwa Mkutano wa Sita wa Bunge lako Tukufu, kumekuwepo na matukio mbalimbali ya kuhuzunisha na yenye majonzi makubwa yaliyosababishwa na misiba na ajali ambazo zimesababisha vifo na kujeruhi Watanzania wenzetu wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Napenda kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa salaam za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Watanzania wote waliopoteza maisha. Tuwaombee Marehemu wote ili Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Vilevile nawapa pole majeruhi wote walionusurika na kupata majeraha kutokana na ajali mbalimbali zikiwemo ajali za magari, pikipiki, baiskeli na vifaa vingine vya barabarani pamoja na ile ya Shirika la Ndege nchini *(ATCL)* iliyotokea kule Kigoma.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kwamba katika kipindi hiki tumekuwa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamekuwa wakisumbuliwa na maradhi mbalimbali. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusikia maombi yetu. Wote tumefarijika kutokana na kurejea kwa Mheshimiwa Daktari Harrison George Mwakyembe ndani ya Bunge lako Tukufu akiwa na afya njema. Tunaamini afya yake itazidi kuimarika katika siku zijazo. *(Makofi)*

Vilevile ni matumaini yetu makubwa kwamba wenzetu wengine akiwemo Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya, Mbunge wa Jimbo la Rungwe Mashariki na Waziri wa Maji; Mheshimiwa Daktari John

Pombe Magufuli, Mbunge wa Chato na Waziri wa Ujenzi; pamoja na Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela ambao bado wako katika matibabu watapata nafuu haraka itakavyowezekana ili waweze kuungana na sisi tena ndani ya Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naungana na Watanzania wote kuipongeza timu ya Simba kwa kufikia mzunguko wa tatu wa mashindano ya kombe la mabingwa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunawatakia maandalizi mema ili wazidi kufanya vizuri katika mechi zijazo kwa kuwa ushindi wao ni ushindi wa nchi yetu wote. Kwa wachezaji na viongozi wao, nawaasa sasa wasibweteke na ushindi walioupata, ila mnatakiwa kuelewa kuwa safari bado ni ngumu na ndefu na hivyo lazima kuongeza juhudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za Serikali, katika Mkutano huu wa Saba tunaouhitimisha leo jumla ya maswali 131 ya msingi na mengine 315 ya nyongeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge yalipata majibu ya Serikali. Vilevile jumla ya maswali 16 ya msingi na tisa ya nyongeza kupitia utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yalijibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Miswada, katika Mkutano huu Miswada ifuatayo ilisomwa na kujadiliwa:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Biashara wa Mwaka 2011 *(The Business Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011 *(The Tanzania Livestock Research Institute Bill, 2011);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012);* na

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2011).*

Vilevile Muswada wa Sheria ya Haki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea wa Mwaka 2012 *(The Plant Breeder's Rights Bill, 2012)* ulisomwa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa mbalimba, Bunge lako Tukufu lilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Taarifa za Kamati za Bunge zinazosimamia Fedha za Umma; na

(ii) Taarifa za Kamati za Bunge za Kisekta na zisizo za Kisekta.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika siku zote za Mkutano huu zikiwemo kujadili na kupitisha Miswada niliyotaja hapo juu. Nawashukuru pia kwa michango yenu wakati wa kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nitumie nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Bunge zilizowasilisha taarifa mbalimbali mbele ya Bunge lako Tukufu. Ni dhahiri kuwa utaratibu huu unatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia kwa kina masuala mbalimbali ya kisekta na kutoa ushauri kwa Serikali. Aidha, utaratibu huu unatusaidia kuwepo kwa *checks and balances* ndani ya nchi yetu. Niwashukuru pia Wabunge wote kwa jinsi walivyochangia kwenye mjadala wa kujadili taarifa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameonesha hisia zao katika kujadili masuala yote haya muhimu na mengineyo hasa katika mwenendo wa matumizi ya fedha za Serikali kwenye Wizara, Taasisi za Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nawashukuru sana kwa kujadili taarifa zote kwa uwazi na hatimaye kutoa mapendekezo kwa Serikali namna ya kushughulikia matatizo yaliyojitokeza kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yapo katika makundi muhimu kadhaa na ninaomba tu nitaje baadhi ya makundi hayo ambayo yalijitokeza waziwazi:-

Kwanza ni uimarishaji wa uongozi na utendaji katika Wizara, Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Mikoa na Serikali za Mitaa;

Pili, ni usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusu masuala ya mapato na matumizi ya fedha;

Tatu, ni uimarishaji wa hatua za kupambana na rushwa, ubadhirifu na wizi wa mali za umma;

Nne, ni uendelezaji wa hatua za kubana matumizi yasiyo ya lazima ndani ya Serikali na vyombo vyake; na

Tano, ni ulinzi wa rasilimali za nchi kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, siku zote Serikali imekuwa tayari kupokea ushauri wa Bunge lako Tukufu na baada ya kusikiliza mjadala na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali inawaahidi itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa ushauri na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hizo. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itachukua hatua stahiki kuimarisha usimamizi na utendaji ndani ya Wizara na Serikali za Mitaa na vyombo vyake na kuhakikisha viongozi na watendaji wake wanafanya kazi kwa umakini na uadilifu zaidi na pale ambapo hapana budi hatua za kuwadhibiti wale wote watakaobainika kuwa hawakutimiza wajibu wao vizuri zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu hii ningependa kuzungumzia kwa kifupi mambo machache yanayohusu hatua zilizofikiwa katika mchakato wa kutekeleza Sheria ya Mabadiliko ya Katiba; dhana ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; matokeo ya shule za msingi na kidato cha nne mwaka 2011; maendeleo ya viwanda; sensa ya watu na makazi na mwisho mpango wa kutoa kifuta machozi cha mifugo.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa katika mchakato wa kutekeleza Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, katika Mkutano wa Sita mwezi Februari, 2012 Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Sura ya 83). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mara baada ya marekebisho hayo kupitishwa, Mheshimiwa Rais Daktari Jakaya Mrisho Kikwete kupitia Tangazo la Serikali Namba 66 la tarehe 24 Februari, 2012 alialika vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, jumuiya za dini, asasi za kiraia, taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kuwasilisha kwake majina ya watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume itakayoratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo hilo, siku ya mwisho ya kuwasilisha mapendekezo ya majina ilikuwa tarehe 16 Machi, 2012. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa zoezi hilo na ili kutoa fursa zaidi kwa wananchi na taasisi au makundi yaliyopo mikoani, Mheshimiwa Rais kupitia Tangazo la Serikali Namba 101 la tarehe 16 Machi, 2012 aliongeza muda huo hadi tarehe 23 Machi, 2012. Mapendekezo ya majina yaliyopokelewa yalikuwa mengi na hivyo kumpa Mheshimiwa Rais uwanja mpana zaidi wa kufanya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Aprili, 2012 Mheshimiwa Rais baada ya kushauriana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliteua Wajumbe 32 wa Tume itakayoratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba. Pamoja na Wajumbe hao, Mheshimiwa Rais aliteua Katibu na Naibu Katibu wa Tume hiyo. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe, Katibu na Naibu Katibu wa Tume waliapishwa na Mheshimiwa Rais tarehe 13 Aprili, 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Tume hii katika historia ya nchi yetu, naomba niwataje Wajumbe wote wa Tume walioteuliwa ni Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba – Mwenyekiti; Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu, Augustino Ramadhani - Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Daktari Salim Ahmed Salim – Mjumbe; Ndugu Abubakar Mohammed Ali – Mjumbe; Ndugu Ally Abdullah Ally Saleh – Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir (Mb.) – Mjumbe; Ndugu Awadh Ali Said – Mjumbe; Daktari Edmund Adrian Sengondo Mvungi – Mjumbe; Ndugu Esther P. Mkwizu – Mjumbe; Ndugu Fatma Said Ali – Mjumbe; Ndugu Humphrey Polepole – Mjumbe; Ndugu Jesca Sydney Mkuchu – Mjumbe; Ndugu John J. Nkolo – Mjumbe; Ndugu Joseph Butiku – Mjumbe; Ndugu Kibibi Mwinyi Hassan – Mjumbe; Ndugu Maria Malingumu Kashonda – Mjumbe; Ndugu Muhammed Yussuf Mshamba – Mjumbe; Ndugu Mwantumu Jasmine Malale – Mjumbe; Profesa Mwesiga L. Baregu – Mjumbe; Ndugu Nassor Khamis Mohammed – Mjumbe; Ndugu Omar Sheha Mussa – Mjumbe; Profesa Palamagamba J. Kabudi – Mjumbe; Mheshimiwa Raya Suleiman Hamad – Mjumbe; Ndugu Richard Shadrack Lyimo – Mjumbe; Ndugu Riziki Shahari Mngwali – Mjumbe; Alhaj Said El- Maamry – Mjumbe; Ndugu Salama Kombo Ahmed – Mjumbe; Ndugu Salma Maoulidi – Mjumbe; Ndugu Simai Mohamed Said – Mjumbe; Ndugu Suleiman Omar Ali – Mjumbe; Ndugu Ussi Khamis Haji – Mjumbe; Ndugu Yahya Msulwa – Mjumbe; Ndugu Assaa Ahmad Rashid – Katibu; na Ndugu Casmir Sumba Kyuki – Naibu Katibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Mheshimiwa Augustino Ramadhani, Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Vilevile, napenda kuwapongeza Wajumbe wote wakiwemo Katibu na Naibu Katibu kwa kuteuliwa kuunda Tume hii. Ni matumaini yangu na ya Watanzania wote kwa ujumla kuwa Wajumbe wa Tume watatumia ujuzi, maarifa na uzoefu wao katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu waliyopewa kwa mujibu wa sheria na kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilivyojipanga (Maandalizi ya Tume). Wakati wa hafla ya kuwaapisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe, Katibu na Naibu Katibu wa Tume, Mheshimiwa Rais aliihakikishia Tume kuwa Serikali itaipa kila aina ya ushirikiano ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Kwa niaba ya Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kwa mara nyingine tena nikuhakikishie kuwa Serikali imejipanga kwa kuweka mazingira yatakayoiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kama Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Sura ya 83) inavyoelekeza. Hivi sasa Serikali inakamilisha maandalizi muhimu kuiwezesha Tume kuanza kazi tarehe 1 Mei, 2012 kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwaomba wananchi wote kuipa Tume ushirikiano wa kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile napenda kuwasihi wananchi wajitokeze kwa wingi katika mikutano itakayoitishwa na Tume na watoe maoni yao kwa uhuru na utulivu bila vikwazo vyovyote. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanashiriki kikamilifu bila ubaguzi wowote katika mchakato huo wa kuandika Katiba Mpya ili nchi yetu iweze kupata Katiba itakayokidhi mahitaji ya karne hii na miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa siku ya kuwaapisha Wajumbe wa Tume kwamba mchakato huu wa Mabadiliko ya Katiba siyo mchakato wa kuwepo au kutokuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huu ni mchakato unaolenga kukubaliana namna bora ya kuendesha nchi kwa kuzingatia uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uwepo wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, uwepo wa mihimili mitatu ya dola yaani Bunge, Mahakama na Serikali na namna nzuri ya kuboresha utendaji kazi wa mihimili hiyo. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi juu ya kuzingatia mambo haya ya msingi wakati wa kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Namba 8 ya mwaka 2008 ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Umuhimu wa Hifadhi ya Jamii nchini unatambuliwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 11(1) inayosomeka, nanukuu: "Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi." Mwisho wa kununukuu.

Hivyo, hifadhi ya jamii ni nguzo muhimu katika kutekeleza dhana ya utawala bora katika jamii na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kuwa na mipango ya hifadhi ya jamii ni kuondoa umaskini wakati wa uzee na kutoa kinga ya kiuchumi na kijamii pale panapotokea matukio na majanga mbalimbali yanayosababisha kupungua kwa kipato. Hivi sasa kuna Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii ambayo inatoa mafao ya muda mfupi na muda mrefu kulingana na taratibu zilizopo katika Sheria za Mifuko husika. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF);* Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma *(PPF);* Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF);* Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa *(LAPF);* Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Serikali *(EGPF)* na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, ni asilimia 5.9 tu ya nguvukazi ya Watanzania waliopo katika sekta rasmi ndiyo wanaopata huduma ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Takwimu hizi ni kielelezo tosha kuonesha changamoto inayoikabili sekta ya Hifadhi ya Jamii katika kuhakikisha Watanzania wengi wanajiunga na kunufaika na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, changamoto hii si kwa wananchi wanaojishughulisha katika sekta isiyo rasmi tu bali hata kwa wale waliopo katika sekta rasmi ambao kwa namna moja au nyingine hawajajiandikisha katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine zinazokabili Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ni pamoja na kupishana sana kwa mafao kati ya mfuko mmoja na mwingine japo kiwango cha kuchangia kinalingana yaani asilimia 20 ya mshahara wa mtumishi. Lipo pia tatizo la pensheni isiyoendana na gharama za maisha, gharama kubwa za uendeshaji wa mifuko, huduma hafifu kwa wanachama wa mifuko, kukosekana kwa kanuni za uwekezaji zinazolingana pamoja na idadi kubwa ya wananchi kutoelewa umuhimu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizopo kwenye sekta hii ya hifadhi ya jamii, Serikali imechukua hatua mbalimbali. Moja ya hatua hizo ni kuanzisha na kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 ambayo ni dira ya shughuli zote za Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Vilevile mwaka 2008 Serikali ilianzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii, jukumu kubwa la mamlaka hii ni kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwamo mifuko yote ya hifadhi ya jamii nchini. Ni matumaini yangu kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii itatusaidia kuzifanyia kazi changamoto nilizozitaja hapo juu na nyingine ili kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanajiunga na kupata Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, Serikali ilileta katika Kikao hiki cha Bunge Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Nichukue fursa hii kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Muswada huu. Muswada huo uliopitishwa na Bunge unalenga kuwianisha Sheria za Mifuko na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii. Lengo ni kuipa mamlaka uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake; na kuiwezesha mifuko kutoa huduma bora kwa wanachama wake. Muswada huu unaiwezesha pia mifuko kutambua uwezo wa mamlaka kuleta mageuzi kwenye sekta kwa kutoa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwakumbusha waajiri wanaokiuka sheria kwa kuwachagulia wafanyakazi wao wapya mifuko ya kujiunga nao kinyume na matakwa ya wafanyakazi hao waache kufanya hivyo. Kila mwajiri anatakiwa kuweka mazingira yatakayomwezesha mfanyakazi kuchagua mfuko anaoupenda. Mazingira hayo ni pamoja na kuialika mifuko yote kutoa maelezo husika, maelezo kuhusu mafao na huduma zao na kuwapa fursa wafanyakazi kufanya maamuzi ya kujiunga na mfuko wanaoupenda. Ni matumaini yangu kuwa mamlaka itaweka kanuni zitakazowezesha mifuko kuandikisha wanachama kwa utaratibu unaokubalika na unaomlinda mwanachama. Kwa upande wa uwekezaji mamlaka imekamilisha tathmini ambayo itawezesha kutengeneza miongozo kwa mifuko kuwekeza katika uchumi mbalimbali. Vilevile mamlaka itaweka mkakati kabambe wa kuelimisha umma ili wananchi wengi zaidi waweze kujiunga na mifuko hii kwa kuwa sasa wanaruhusiwa kujiunga na mifuko hiyo bila kujali kama wako sekta rasmi au isiyo rasmi.

Napenda pia kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kutoa ushirikiano stahiki kwa mamlaka ili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tuboreshe, tuimarishe na kuwa na sekta ya hifadhi ya jamii iliyo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya Sheria yanaipa mamlaka nguvu za kuangalia upya suala zima la ukokotoaji wa mafao ya wanachama na hasa mafao ya pensheni ambayo hivi sasa hutolewa na mifuko hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko husika. Kila mfuko una utaratibu wake hivyo kusababisha viwango vya mafao kutofautiana kwa kiwango kikubwa na kuleta kero kwa wanachama wa mifuko inayolipa mafao madogo. Kutokana na Mabadiliko ya Sheria yaliyofanyika, mchakato wa ukokotoaji wa mafao utazingatia miaka ambayo mtumishi ametumikia, muda wa kuishi baada ya kustaafu, thamani ya pensheni ikilinganishwa na kushuka kwa thamani ya fedha na mfumuko wa bei. Vilevile mamlaka itaangalia namna ya kuunganisha kipindi cha

mtumishi alichokuwa kazini katika sehemu mbalimbali. Mageuzi haya yanakusudia kuboresha mafao yatolewayo na mifuko na kuleta ufanisi katika uendeshaji wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa Marekebisho ya Sheria hii kutaiwezesha mamlaka kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaoingia kwenye ajira kwa mara ya kwanza na wale ambao wapo kwenye ajira wanaamua kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wanaoupenda kwa utashi wao bila shinikizo au kulazimishwa na mtu yeyote. Hatua hii ni muhimu katika kukuza haki za kiraia hususan haki zinazohusiana na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwakumbusha waajiri wanaokiuka sheria kwa kuwachagulia wafanyakazi wao wapya, mifuko ya kujiunga nayo kinyume na matakwa ya wafanyakazi hao waache kufanya hivyo. Kila mwajiri anatakiwa kuweka mazingira yatakayomwezesha mfanyakazi kuchagua mfuko anaoupenda. Mazingira hayo ni pamoja na kuialika mifuko yote kutoa maelezo kuhusu mafao na huduma zao na kuwapa fursa wafanyakazi kufanya maamuzi ya kujiunga na mfuko waupendao. Ni matumaini yangu kuwa mamlaka itaweka kanuni zitakazowezesha mifuko kuandikisha wanachama kwa utaratibu unaokubalika na unaomlinda mwanachama.

Kwa upande wa uwekezaji, mamlaka imekamilisha tathmini ambayo itawezesha kutengeneza miongozo kwa mifuko kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali. Vilevile mamlaka itaweka mkakati kabambe wa kuelimisha umma ili wananchi wengi zaidi waweze kujiunga na mifuko hii kwa kuwa sasa wanaruhusiwa kujiunga na mifuko hiyo bila kujali kama wako sekta rasmi au isiyo rasmi.

Napenda pia kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kutoa ushirikiano stahiki kwa mamlaka ili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tuboreshe, tuimarishe na kuwa na sekta ya hifadhi ya jamii iliyo endelevu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 wanafunzi 983,545 wa darasa la saba walifanya mtihani wa Taifa. Kati yao wanafunzi 567,567, sawa na asilimia 58.28 ya waliofanya mtihani walifaulu. Kiwango cha ufaulu cha mwaka 2011, ikilinganishwa na kile cha mwaka 2010 unaonesha kupanda kwa asilimia 4.76 kutoka asilimia 53.52 ya mwaka 2010 hadi 58.28 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha ufaulu kimasomo umeongezeka kwa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi.

(i) Kiwango cha ufaulu kwa somo la Hisabati kilikuwa asilimia 39.4 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 24.7 mwaka 2010;

(ii) Kiwango cha ufaulu kwa somo la Kiingereza kilikuwa asilimia 46.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 36.5 mwaka 2010; na

(iii) Kiwango cha ufaulu kwa somo la Sayansi kilikuwa asilimia 61.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 56.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa masomo ya Kiswahili na Maarifa ya Jamii kilishuka kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na mwaka 2010. Kwa mfano, ufaulu kwa somo la Kiswahili ulikuwa asilimia 68.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 71.0 mwaka 2010; na kiwango cha ufaulu kwa Somo la Maarifa ya Jamii kilikuwa asilimia 54.8 mwaka 2011 ikilingnishwa na asilimia 68.0 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa muda mrefu tumekuwa na matatizo ya ufaulu katika masomo ya Sayansi nchini, lakini matokeo ya mwaka 2011 yanaonesha kuwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kukuza masomo hayo zimeanza kuzaa matunda. Napenda kuwapongeza wanafunzi, wazazi, walezi, walimu na watendaji wote walioshiriki katika kuleta mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi wa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2012, jumla ya wanafunzi 515,187, sawa na asilimia 90.1 ya wanafunzi waliofaulu walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule za sekondari za Serikali. Idadi hii iliongezeka kwa asilimia 12.49 kutoka wanafunzi 456,350 mwaka 2010. Taarifa nilizopokea kutoka mikoa 12 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mara, Morogoro, Mwanza, Lindi, Kilimanjaro, Pwani, Ruvuma na Tanga, zinaonesha kuwa wanafunzi wote waliofaulu wamejiunga na kidato cha kwanza. Nitumie nafasi hii kuipongeza mikoa hii kwa kuhakikisha kuwa hakuna wanafuzi waliofaulu na kushindwa kujiunga na sekondari.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya mikoa niliyoitaja inaonesha kuwepo kwa uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa na madawati. Naomba kwa mara nyingine tena kusisitiza kuiagiza mikoa yote kuhakikisha mapungufu haya yanashughulikiwa katika Bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, mikoa iwe na mipango endelevu ya kujenga vyumba vya madarasa na kutengeneza madawati badala ya kusubiri matokeo ya mtihani na kuchaguliwa kwa wanafunzi ndipo ianze kuweka mikakati

watumie maoteo yanayofanywa na wataalam kuhakikisha kwamba mipango yote ya maandalizi inakamilika kabla ya mitihani.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2011 yanaonesha kuwa wanafunzi 181,880, sawa na asilimia 53.6 ya wanafunzi 339,330 waliofanya mtihani walifaulu. Kiwango hicho kimeongezeka kutoka wanafunzi 177,011 waliofaulu mwaka 2010 ikiwa ni sawa na asilimia 50.4 ya wanafunzi 351,214 waliofanya mtihani.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2008, asilimia ya wanafunzi wanaofeli mitihani ya kidato cha nne imekuwa ikiongezeka na kufikia asilimia 16.3, mwaka 2009 asilimia 27.5, mwaka 2010 asilimia 49.6 na kushuka tena hadi asilimia 43.3, mwaka 2011. Sababu za kushuka kwa ufaulu huo ni pamoja na upungufu wa walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuimarika kwa udhibiti wa uvujaji wa mitihani ya kidato cha nne. Vilevile inaelezwa na wanataaluma na watafiti kwamba kuondolewa kwa mtihani wa kidato cha pili kwa kiasi fulani kumechangia sana matokeo mabaya ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaofeli mtihani wa kidato cha nne, Serikali imechukua hatua kadhaa zikiwemo za kuongeza na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya *capitation grant* ili kupunguza tatizo la upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia shuleni; kutekeleza mikakati ya kuongeza idadi na ubora wa walimu na kujenga uwezo wa wakuu wa shule kusimamia ufundishaji na ujifunzaji wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba tukiyafanya haya, tutaweza kufikia azma yetu ya kuwa na matokeo mazuri katika siku zijazo. Niwaombe wadau wote wa elimu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, viongozi, walimu, wazazi, walezi na wanafunzi kila mmoja atimize wajibu wake katika utoaji wa elimu kuanzia nyumbani, shuleni na vyuoni ili tuweze kuinua kiwango cha ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 hadi 23 Septemba, 2011 nilifanya ziara Mkoa wa Mara na kutembelea Kiwanda cha Nguo cha *Musoma Textile (MUTEX).* Tarehe 2 hadi 4 Desemba, 2011 nilifanya ziara nyingine fupi Mkoa wa Mwanza na kutembelea Kiwanda cha kutengeneza Nguo cha *Mwanza Textile (MWATEX).* Kwa kweli nilikuta viwanda hivyo vinakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za kukosekana kwa umeme wa uhakika, wataalam na teknolojia ya kisasa. Nilielezwa kuwa changamoto hizo zinavikabili viwanda vingi vya nguo nchini.

Mheshimiwa Spika, sote hapa tunafahamu kuwa maendeleo makubwa na ya kasi kwenye nchi mbalimbali ulimwenguni yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya viwanda vya nguo na mavazi. Viwanda hivi hutoa soko la uhakika kwa zao la pamba linalolimwa hapa nchini; huajiri kiasi kikubwa cha wafanyakazi na hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kupunguza tatizo la ajira na umaskini hasa miongoni mwa vijana. Pia huchangia mapato kwa Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kutofanya vizuri kwa viwanda hivi kunaikosesha Serikali na wananchi mapato na kuongeza tatizo la ajira nchini. Niliona kuna umuhimu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizo ndani ya uwezo wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali natumia madaraka yangu ya kuongeza muda kwa kutumia kifungu cha 28(5) nitaongeza muda mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu amalize hotuba yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Machi, 2012, niliitisha mkutano wa wadau wa sekta ndogo ya viwanda vya mavazi na nguo ili kwa pamoja tuweze kuainisha changamoto zinazoikabili sekta hiyo na kupata mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Kufuatia mkutano huo, iliundwa timu ya wataalam ili iweze kuangalia changamoto hizo kwa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Serikali pamoja na wadau wote ili kukabiliana na changamoto hizo. Timu hiyo ilipewa mwezi mmoja na wakati wowote kuanzia sasa itawasilisha taarifa yake Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Aprili, 2012 nilipata fursa ya kutembelea viwanda vya *Sunflag Tanzania Ltd.,* Kiwanda cha *A to Z* na *Minjingu Mines and Fertilizer Limited* vyote vya mkoani Arusha. Katika viwanda vya nguo vya *Sunflag* na *A to Z* nilifarijika sana kuona idadi kubwa ya watumishi walioajiriwa na kwamba zaidi ya asilimia 80 walikuwa ni akinamama, tena vijana wenye umri kati ya miaka 18 mpaka 30. Nawapongeza viongozi wa viwanda hivi kwa jitihada ambazo wanazifanya kuendeleza uzalishaji na hivyo kuchangia mapato kwa Serikali na ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *Sunflag* ni Kiwanda pekee nchini kinachozalisha nguo kuanzia hatua ya pamba kutoka kwa mkulima hadi nguo za kuvaa. *Sunflag* wamekuwa ni soko zuri na la uhakika la pamba ya wakulima. Nawapongeza kwa uamuzi wao huo ambao una faida kubwa kwa wakulima wa pamba. Viongozi wa viwanda hivyo walinieleza changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo. Serikali itafanya kila lililo ndani ya uwezo wake kuimarisha viwanda vinavyotumia pamba ya Tanzania na kuweka mazingira yatakayoendelea kuvutia uwekezaji katika sekta hii ya nguo na mavazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa ya timu niliyoitaja hapo awali, Serikali itachukua hatua zitakazoondoa changamoto zinazovikabili viwanda vya nguo na mavazi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanda cha *Minjingu Mines and Fertilizer Limited* nilielezwa kuwa wamefanikiwa kuzalisha mbolea ya Minjingu Mazao ambayo ni bora kuliko mbolea aina ya *DAP* kwa kuwa ina virutubisho vya *Nitrogen, Phosphorous, Sulphur, Calcium* na rutuba kama *Magnesium, Zinc* na Boroni. Aidha, Minjingu Mazao ina bei ndogo kuliko *DAP.* Kiwanda kwa sasa kina akiba *(stock)* ya tani 5,600 ya *Phosphate* na tani 7,100 ya Minjingu Mazao. Nilielezwa kuwa matumizi ya mbolea ya Minjingu nchini yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka kutokana na matatizo mbalimbali ikiwemo hujuma inayofanywa kwenye mfumo wa ruzuku za pembejeo.

Napenda kuhimiza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ione namna ya kukikwamua Kiwanda cha Minjingu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuongeza matumizi ya mbolea za Minjingu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akitoa hotuba yake ya kumaliza mwaka 2011 alitangaza rasmi dhamira ya Serikali kufanya sensa ya watu na makazi ambayo imepangwa kufanyika nchini kote tarehe 26 Agosti, 2012. Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa sensa ya watu na makazi pamoja na vitambulisho vya Taifa ni mojawapo ya vipaumbele vya Taifa kwa mwaka huu wa 2012.

Tarehe 12 Aprili 2012, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuhudhuria semina kuhusu sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Katika semina hiyo yalitolewa maelezo ya kina kuhusu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya sensa ya watu na makazi. Nina imani kuwa baada ya semina hiyo ya tarehe 12 Aprili, 2012, hivi sasa Waheshimiwa Wabunge wana uelewa mpana kuhusu umuhimu wa taarifa zitokanazo na sensa na kwamba watatumia uelewa huo kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kujiandikisha.

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 madhumuni yake makubwa ni kupata takwimu kuhusiana na idadi ya watu na kukusanya taarifa za kina za kiuchumi, kijamii na maelezo ya makazi. Taarifa hizi hutumiwa na Serikali na taasisi nyingine kwa shughuli mbalimbali za mipango na maendeleo. Serikali pia hutumia takwimu zitokanazo na sensa katika kutunga sera, kufanya maamuzi juu ya utawala wa umma kwa kuzingatia mahitaji halisi na vigezo vingine kama vile umri, jinsia na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sensa ya mwaka 2012 ina umuhimu wa kipekee kwa kuwa taarifa zitakazokusanywa zitatumika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na mwaka 2020 kwa Tanzania Zanzibar. Vilevile taarifa hizo zitatumika kutathmini Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umaskini Tanzania Bara (MKUKUTA) na Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania Zanzibar (MKUZA). Takwimu hizo zitatumika pia kutathmini utekelezaji wa malengo ya milenia ifikapo mwaka 2015; mpango wa maendeleo wa miaka mitano wa 2011/2012 – 2015/2016 pamoja na kubuni mikakati ya utekelezaji wa mpango elekezi wa miaka 15 wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo hadi mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi yanayoendelea hivi sasa, mafanikio ya sensa yatategemea sana ushiriki wa umma na wadau wengine. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa Kamati za sensa za Wilaya na Halmashauri zetu na moja ya majukumu ya Kamati hizo ni kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa sensa ya watu na makazi ili kuhakikisha kuwa kila mtu atakayelala nchini usiku wa kuamkia siku ya sensa yaani tarehe 25 Agosti, 2012 kuamkia tarehe 26 Agosti, 2012 anahesabiwa na kwamba anahesabiwa mara moja tu.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ni la Kitaifa hivyo linahitaji uhamasishaji na ushirikishwaji wa wananchi wote. Natoa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la sensa ya watu na makazi na kutoa ushirikiano mkubwa kwa makarani wa sensa watakaofanya kazi ya kuhesabu watu siku ya tarehe 26 Agosti, 2012.

Vilevile naomba nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na viongozi wengine kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za sensa katika Wilaya na Halmashauri kwa kuhakikisha kuwa elimu kwa wananchi inatolewa. Nawaomba pia Waheshimiwa Wabunge kutumia nafasi zao kama wawakilishi wa wananchi kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kushirikiana na makarani wa sensa wakati wa kipindi cha kuhesabu watu kwa kutoa takwimu sahihi na hivyo kupata taarifa sahihi kwa ajili ya mipango endelevu ya maendeleo. Kaulimbiu yetu kila wakati iwe ni Sensa kwa Maendeleo ya Taifa, Jiandae Kuhesabiwa. Napenda kuwatakia mafanikio mema katika kazi hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009, mikoa ya Kaskazini hasa mikoa ya Arusha na Manyara ilikumbwa na ukame mkubwa ambao ulisababisha vifo kwa mifugo. Kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa kifuta machozi kwa kuwapatia mifugo ya mbegu wafugaji waliopoteza mifugo yao yote katika Wilaya za

Longido, Monduli na Ngorongoro. Katika kutekeleza ahadi ya Rais, Serikali iliunda kikosi kazi ambacho kilibaini kuwepo kwa vifo vya ng'ombe 403,839; mbuzi 211,201 na kondoo 121,118 katika wilaya hizo.

Vilevile kikosi kazi kilibaini kwamba jumla ya kaya 6,127 katika Wilaya hizo zilipoteza mifugo kutokana na ukame. Wilaya ya Longido ilikuwa na jumla ya kaya 2,852; Monduli kaya 1,484 na Ngorongoro kaya 1,791 zilizoathirika na ukame ulioambatana na vifo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali ilitoa tamko Bungeni kuhusu kutekeleza ahadi ya kutoa kifuta machozi kama mbegu *(seed stock)* kwa kaya zilizopoteza mifugo yote ili ziweze kurudi katika hali yao ya awali kama wafugaji. Aidha, mradi maalum ulianzishwa kwa ajili ya kununua mifugo (ng'ombe na mbuzi) kwa ajili ya Wilaya husika. Ununuzi wa mifugo hiyo utafanyika katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuundwa kwa Kamati mbalimbali (mkoa, halmashauri, kata na vijiji) za kusimamia utekelezaji wa mpango wa kusambaza mifugo ya kifuta machozi, halmashauri za wilaya zilielekezwa kutangaza zabuni za kuwapata wanunuzi wa mifugo ndani ya maeneo ya wilaya husika katika kipindi cha siku 90. Utekelezaji wa zoezi hili utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, awamu ya kwanza itaanza kwa kununua ng'ombe 500 kwa kila Wilaya. Lengo ni kukamilisha zoezi hili kabla ya kiangazi kuanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uzinduzi wa mpango wa kutoa kifuta machozi ulifanywa na Mheshimiwa Rais, Daktari Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 19 Februari, 2012 katika Wilaya ya Longido ambapo Serikali ilitumia shilingi milioni 213 kwa kununua na kusambaza ng'ombe 500.

Aidha, ununuzi wa mifugo kwa ajili ya Wilaya za Monduli na Ngorongoro utakamilika mara Serikali itakapokamilisha taratibu za kutuma fedha kwa Halmashauri za Wilaya hizo. Kiasi cha shilingi milioni 206 zimetengwa kwa ajili ya Wilaya ya Monduli na shilingi milioni 218 kwa ajili ya Wilaya ya Ngorongoro ili kuwezesha ununuzi wa ng'ombe 500 kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, matumaini yangu ni kuwa zoezi la kutoa kifuta machozi kwa wananchi wa Wilaya za Monduli na Ngorongoro litakamilika katika muda mfupi ujao kwa kuwa mifugo hiyo ipo tayari kwa wazabuni, kinachosubiriwa ni malipo ya fedha. Natoa wito kwa wafugaji na

wananchi walioathirika na ukame ambao wanasubiri awamu ya pili kuwa na subira wakati Serikali inatafuta fedha za kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kusisitiza maeneo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, tumeanza mchakato wa utekelezaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, mchakato ambao ni msingi wa utawala bora. Natoa wito kwamba tuwaelimishe wananchi kuhusu mambo ya msingi wakati wa kuchangia maoni na kwamba Mabadiliko ya Katiba siyo mchakato wa kuwepo au kutokuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pili, tunayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo tukiitumia vizuri, ni kinga na kichocheo muhimu cha kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Tushirikiane na Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa faida yao kwani hivi sasa haijalishi kama uko kwenye sekta rasmi au isiyo rasmi.

Tatu, bado tunazo changamoto nyingi katika sekta ya elimu hasa katika miundombinu na ubora wa elimu kwa ujumla. Tushirikiane katika kutekeleza mikakati ya kutuwezesha kuwa na elimu bora kwa watoto wetu. Tuwajengee utamaduni wa kujiamini na kushiriki kikamilifu katika kuboresha miundombinu muhimu kuanzia shule za msingi, sekondari hadi vyuo.

Nne, kuwepo kwa viwanda nchini ni muhimu kwa maendeleo yetu na uchumi wa nchi. Pamoja na changamoto zilizopo ni vizuri kuweka umuhimu wa kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu.

Tano, tarehe 26 Agosti, 2012 itakuwa ni siku ya sensa ya watu na makazi nchini. Tuwahamasishe wananchi waelewe umuhimu wa kuhesabiwa siku hiyo na utaratibu utakaotumika ikiwa ni pamoja na kila mtu kuhakikisha anahesabiwa na kwamba anahesabiwa mara moja tu.

Mheshimiwa Spika, tunapohitimisha Mkutano huu wa Saba, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu, tunao wajibu wa kiungwana kuwashukuru pia wote walioshiriki katika kutoa huduma muhimu katika kufanikisha Mkutano huu. Hivyo basi, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza vizuri na hatimaye kukamilisha vikao vyote kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Vilevile namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri. Niruhusu nimshukuru Daktari Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa kutuwezesha kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa. Niwashukuru pia wataalam wote ambao mchango wao kwetu umekuwa ni muhimu sana. Niwashukuru askari, madereva, wanahabari kwa kushiriki kikamilifu katika kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapohitimisha Mkutano huu wa Saba, tunapata fursa ya kujiandaa kwa ajili ya Mkutano wa Nane ambao ni mahsusi kwa ajili ya Bajeti ya mwaka 2012/2013.

Napenda kuwatakia maandalizi mema kwa ajili ya Bajeti ya Serikali. Ni dhahiri kwamba bado tuna changamoto nyingi. Naomba niwasihi kila mmoja wetu kujiwekea malengo ya kutimiza wajibu wake katika kufikia yale yote tunayoyatarajia kuyafanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nisisitize kwamba pengine jukumu hili ni kubwa zaidi kwa upande wa Serikali kuliko kwa pande nyingine zozote. Hivyo ni wajibu wetu viongozi wote ndani ya Seirkali kuhakikisha tunatimiza wajibu wetu ipasavyo. Nimalizie kwa kuwatakia nyote safari njema ya kurejea katika maeneo yenu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 12 Juni, 2012 saa 3.00 asubuhi, litakapokutana kwenye Ukumbi huu hapa Mjini Dodoma kujadili Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, kabla sijawahoji naomba na mimi pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kipindi hiki cha Bunge la Kumi na Mkutano wa Saba. Ninachowaomba kabisa muendelee kusoma na kukariri Kanuni zetu, itawapa uhuru sana wa kujadili kuliko mlivyofanya sasa. Kwa sababu kulijitokeza wengi wameleta hoja wanataka kuunda Kamati Teule kwa barua. Hatufanyi hivyo, someni Kanuni zetu vizuri kusudi mambo yetu hapa vile ambavyo tunatakiwa kufanya katika Kanuni zetu.

Naomba wote mrudie kusoma Kanuni, kadri tunavyokwenda mnaanza kuona kwamba Kanuni fulani umekosea, Kanuni fulani. Kwa hiyo someni tena Kanuni vizuri, nyingine ni wazi kabisa lakini kwa namna moja au nyingine msichukulie urahisi kwa sababu humu ndani tunaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

Lakini la pili, katika kufanya kazi zetu humu ndani kiti hiki huwa hakiondoki bila lawama yaani kazi ya kiti hiki lazima ubebe lawama, maana mnaweza mkajiorodhesha 50 kuzungumza mimi naishia kumi, wale wengine 40 watalalamika na kulaani na kufanya nini. Basi haya yote ndiyo mambo ya humu ndani ndiyo maana tunapiga kengele, ndiyo maana tunafanya hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa wale wote walioudhiwa kwa namna hiyo waelewe tu hakuna nia mbaya ya Spika wala Naibu Spika wala Wenyeviti. Ni hali halisi kwamba tunabanwa na wakati. Lakini yote yaliyojadiliwa humu ndani wote muamini kabisa mmejadili kwa nia njema. Isiwe ni kiini cha kuanzisha uadui, chuki na kutokuelewana kwa sababu watu wamejadili hapa. *(Makofi)*

Mnapojadili hapa ni uwazi, msibebe chuki ndani ya roho zenu kwamba fulani kanisema, fulani kanisema. Hapa anajadili tu, yaishie humu ndani ondokeni na urafiki wenu uwe pale pale. Kwanza kama wewe huusiki watakusemaje? Watakusema kwa sababu wewe ni Spika basi unasemwa. Watakusemaje kama wewe sio Spika, kama wewe ni Waziri utasema, asemwe nani kama wewe ni Waziri na ndiyo maana tunakataa kutaja majina hapa. Tunataka mtu atajwe kwa cheo chake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kabisa ndugu zangu tuchukue hii dhana ya kwamba mtasemana lakini mtaondoka pale nje mkiwa marafiki na hakuna ugomvi wowote. Mliopewa changamoto hapa ndiyo majukumu yenu. Vyeo ni dhamana ungekuwa sio Waziri wa kitu chochote nani akuseme hapa. Lakini kwa sababu wewe ni Waziri wa kitu fulani lazima watakusema tu. Kwa hiyo, msichukue kabisa kama hasira mpaka mnapasuka na mifupa, hapana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa huko ndiko kuwajibika kwenyewe, kitu cha maana unachotakiwa utokenacho hapa kwamba nitakwenda kufanya vizuri zaidi kuliko kipindi kilichopita. Kwa hiyo, maneno haya yote yachukuliwe kama unaambiwa namna ya kufanya kazi yako vizuri.

Mimi sioni kama hapa ni ugomvi, ni kwamba tunakukumbusha fanya vizuri zaidi kuliko ulivyofanya. Kwa hiyo, hili naomba mlichukue kwa moyo mkunjufu na mlichukulie *positive,* msichukulie uadui. Waliosema wamesema na wameenda zao wala hata hawakumbuki. Kwa hiyo, mimi nawaombeni sana msiyachukue hayo mambo ndani ya roho zenu yakawaumizeni.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kipindi hiki, someni vizuri, tafuteni vizuri namna ya kujifunza na kufanya *research*. Hivyo hivyo nawashukuru ndugu zangu wanahabari, hata ninyi fanyeni *research* kidogo mnapoandika vitu vyenu, maana wakati mwingine mnaandika bila *research*, unasoma unashangaa hivi kweli huyu ni mwandishi kweli huyu? Sasa tafadhali msiandike ushabiki wetu sisi, andikeni kile mlichokifanyia *research* vizuri, kitapendeza kusoma na machoni mwa watu watafurahia sana kukisoma.

Natambua uwepo wa Mke wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Tunu Pinda, yupo na familia yake na msaidizi wake. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusimame kwa Wimbo wa Taifa.

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Tukae, Waheshimiwa Wabunge sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka tarehe 12 Juni, 2012, saa tatu asabuhi hapa Dodoma. *(Makofi)*

*(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 12 Juni, 2012 saa tatu asubuhi)*